# Nipashe

Jumatano Novemba 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580068

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Deni la taifa lafikia tril. 52/-, Waziri Mpango aeleza

UKURASA 2




UKURASA 15

## UCHAGUZI MITAA:

# KILIO UPINZANI

**WAGOMBEA** wote majimbo ya Mbowe, Sugu wakatwa, Chadema yaahidi kuchukua uamuzi mgumu, ofisi ya mtendaji yavunjwa... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MBOWE AKANA KUWAPO KWENYE MAANDAMANO**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amedai...

**UKURASA WA 4**

**VIGOGO WA SIMBA WAREJEA URAIANI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imewaachia kwa dhamana vigogo wawili wa Klabu...


## MTENDAJI MBARONI TUHUMA RUSHWA

UKURASA 3



Aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Juma Mussa Assad (kulia), akiongozana na mrithi wake, Charles Kichere, kabla ya kufanya makabidhiano ya ofisi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CAG Assad ampa angalizo mrithi wake

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



**MICHEZO** ZAHERA AMWAGA UPUPU AKITIMULIWA UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Kilio upinzani uchaguzi wa mitaa

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya vyama vya siasa nchini vimedai kuhujumiwa na watendaji wa serikali katika mchakato unaoendelea wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, huku Jeshi la Polisi likiwashikilia baadhi ya wafuasi wa vyama hivyo kwa tuhuma za kuvunja ofisi za serikali.

Kutokana na hali hiyo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ambacho ni chama kikuu cha upinzani nchini, kimesema kitachukua hatua ngumu kukabiliana na ukiukwaji wa kanuni za uchaguzi huo.

Baadhi ya vitendo vinavyolalamikiwa na vyama hivyo, ni kukatwa kwa majina yote ya wagombea wa vyama vya upinzani katika baadhi ya mikoa, hivyo wagombea wa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupita bila kupingwa.

Hali hiyo imeripotiwa katika mkoa wote wa Simiyu ambao inadaiwa majina ya wagombea wote wa Chadema yamekatwa, sawa na majimbo ya Mbeya Mjini na Ubungo na Hai.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kuchukua hatua dhidi ya ukiukwaji huo wa kanuni, aliodai unaendelea licha ya kupeleka malalamiko kwa maandishi katika ofisi ya waziri huyo.

"Tutaitisha vikao vya dharura haraka iwezekanavyo leo (jana) au kesho (leo) ili tutoe msimamo wa pamoja kuhusu uchaguzi huu, serikali na CCM wasifikiri tutakaa kimya na kulia na wanaijua nguvu yetu, tutachukua hatua ngumu," alisema.

Alisema chama kimeshangazwa na uamuzi wa wagombea wake kuenguliwa kabla ya siku ya uteuzi kufika kwa madai ya kukosa sifa.

Mrema alidai yapo maeneo mengi nchini ambayo tayari wasimamizi wameshatoa orodha ya wagombea waliofanikisha kuteuliwa na ambao hawakufanikiwa kuteuliwa huku wagombea wote wa upinzani wakiwa wameenguliwa kwa madai ya kukosa sifa za kugombea.

Akitoa mifano ya maeneo ambayo wagombea wa Chadema wameenguliwa, Mrema alisema ni pamoja na Mkoa wa Simiyu ambao wagombea wao wote wameenguliwa, Jimbo la Ubungo ambalo wagombea wote 47 na wagombea wote 192 wa Jimbo la Mbeya Mjini, ambao alidai walishaenguliwa tangu juzi usiku kabla ya siku ya uteuzi kufika.

JIMBO LA MBOWE

Wakati Mrema akiyasema, katika Jimbo la Hai linaloongozwa na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, hadi jana mchana, wagombea wa upinzani katika vijiji 12 kwenye nafasi ya Mwenyekiti wa Serikali za Vijiji, walidaiwa kutokujitokeza kuchukua fomu hadi kufikia Novemba 4, mwaka huu.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Juma Masatu, alidai jana wagombea wa vyama vya upinzani hawakuji

INAENDELEA UK 26



Mshtakiwa Geoffrey Nyange maarufu kama Kaburu (katikati), akiwa na ndugu na marafiki, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuachiwa kwa dhamana. Kaburu ambaye alikuwa mmoja wa viongozi wa klabu ya Simba na wenzake, wanakabiliwa na mashtaka saba ikiwamo kughushi, kula njama, matumizi mabaya ya madaraka, kutoa nyaraka za uongo, na kutoa maelezo ya uongo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CAG Assad ampa angalizo mrithi wake

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amekabidhi ofisi kwa CAG mpya, Charles Kichere na kumshauri asikimbilie kufanya mabadiliko ya watendaji.

Ametahadharisha kuwa mabadiliko ya haraka yatakuwa na athari hasi kwa taasisi hiyo nyeti.

Prof. Assad alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi ofisi kwa Kichere.

"Hii ni taasisi na makabidhiano ya taasisi yanaenda kwa maandishi. Kwa hiyo, makabidhiano kwa maandishi yatafanyika Dodoma kwa sababu ndiko kule makao makuu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi," alisema.

Hata hivyo, Prof. Assad alisema ameona ni vizuri kufanya mfano wa makabidhiano jijini Dar es Salaam kwa kuwa kuna ofisi ya taasisi hiyo.

"Kimsingi nakabidhi taasisi ya taifa ya ukaguzi na taasisi ina mifumo yake, sheria zake, sera zake na namna zake za kuiendesha, hayo yote yanasimamiwa na watu ambao wapo mbele yetu niliokutambulisha.

"Ni watu ambao unatakiwa kuwatazama vizuri kwa maana ya utendaji kazi, ukiangalia taasisi zote za ukaguzi, wanachokifanya vizuri sana, ni ujengaji wa uwezo wa watu, wanawachukua watu vyuo vikuu na kuwajenga ili wafanye kazi vizuri," alisema.

Aliongeza kuwa ni muhimu kuzingatia jambo hilo kwa kuwa taasisi hiyo haina mfano mwingine katika Tanzania na pia mrithi wake anapaswa kujenga uhusiano mzuri na nchi nyingine.

Alisema kila miezi miwili, kuna mkutano huwa unafanyika nje ya nchi, hivyo ni muhimu kupeleka watumishi wake ili kuwajengea uwezo.

Prof. Assad alisema alipokea ofisi kutoka kwa aliyekuwa CAG, Ludovick Utooh miaka mitano iliyopita na anaamini anaiacha ofisi hiyo ikiwa salama.

"Naamini sikufanya uharibifu wowote, mimi huwa nina amini 'changes' (mabadiliko) huwa zinaweza kutokea, lakini zitokee katika namna ambayo zimepangwa vizuri.

"Mimi si mwaminifu wa ule mfumo wa kutoa watu wote na kuweka watu wengine. Ni gharama kubwa kwa taasisi kama hii ambayo mtu amejifunza kwa muda mrefu, unakuta mtu ana miaka 15 ndiyo anapewa nafasi kwa hiyo uzoefu wake unasaidia kwenda kwa mwingine," alisema.

Prof. Assad alimtahadharisha Kichere kwamba, akifanya mabadiliko kwa haraka, ataharibu historia nzuri ya taasisi hiyo.

"Kichere namjua vizuri, kwanza tumejuana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wakati ule mimi nafundisha wanafunzi

INAENDELEA UK 26

# Mbowe akana kuwapo kwenye maandamano

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amedai mahakamani siku ya tukio hakushiriki na hakuwapo kwenye maandamano ya wafuasi wa chama hicho waliokuwa wakielekea kwenye ofisi za msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Kinondoni.

Mbowe anaendelea siku ya pili na ushahidi wa utetezi katika kesi inayomkabili na vigogo wenzake wanane wa Chadema dhidi ya mashtaka 13 ikiwamo uchochezi.

Ushahidi huo unasikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Akiongozwa na wakili wa utetezi, Peter Kibatala, Mbowe alidai kuwa pamoja na kutajwa na kuhusishwa na maandamano hayo, lakini hakuwapo eneo la tukio na kwamba ilikuwa na hisia tu.

Alidai kuwa baada ya kumaliza mkutano wa kufunga kampeni katika viwanja wa Buibui, Mwanyamala aliondoka uwanjani hapo akiongozwa na askari polisi kuelekea Makao Makuu ya Chadema, Kinondoni.

Alidai siku hiyo wafuasi wa Chadema wakiwa njiani walikutana na wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika makutano ya Barabara ya Morocco na Mwananyamala wakiwa na mgombea wao wakisindikizwa na ngoma aina ya mdundiko.

Mbowe alidai kuwa wanachama hao walikuwa wakiongozwa na polisi kuelekea Barabara ya Morocco na hakujua kilichoendelea nyuma kwa kuwa aliendelea na safari yake ya kuelekea Makao Makuu ya Chadema.

Akizungumzia kufikishwa kwake mahakamani, Mbowe alidai kwa mara ya kwanza alipokea wito wa kuitwa polisi kupitia mkutano wa waandishi wa habari ulioitishwa na Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Pia, alidai kuwa kamanda huyo alitoa wito kwa viongozi wa Chadema kuripoti polisi kuhusu tukio hilo la maandamano.

Vile vile, alidai kupata taarifa kuhusu kifo cha Akwilina

INAENDELEA UK 26

HABARI KITAIFA

# Deni la Taifa lafika Tril. 52/-

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SERIKALI imesema hadi kufikia Agosti mwaka huu, Deni la Taifa lilifikia Sh. trilioni 52.303 kulinganishwa na Sh. trilioni 49.283 katika kipindi cha Agosti, mwaka jana.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mpango, aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma, alipowasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21.

"Deni la serikali hadi Agosti 2019, lilifikia Sh. bilioni 52,303.04 ikilinganishwa na Sh. bilioni 49,283.44 Agosti 2018," Dk. Mpango alisema.

Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la Sh. trilioni tatu katika kipindi cha mwaka mmoja.

Waziri huyo alibainisha kuwa kati ya deni hilo, Deni la Ndani lilikuwa Sh. trilioni 14.075 na Deni la Nje Sh. trilioni 38.227, akieleza kuwa ongezeko la deni lilichangiwa na kupokewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba mwaka jana, ilionyesha Deni la Serikali bado ni himilivu katika muda mfupi, wa kati na mrefu kwa viwango vya kimataifa.

Dk. Mpango alisema serikali inaendelea kuhakikisha deni linakuwa himilivu kwa kuhakikisha mikopo inayokopwa inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye tija kwa taifa.

Kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi, Dk. Mpango alisema uchumi wa taifa umeendelea kuwa imara, akibainisha kuwa katika kipindi cha muongo uliopita (2009 - 2018), Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka.

Alisema mwenendo wa thamani ya shilingi uliendelea kuwa tulivu katika kipindi cha mwaka unaoishia kipindi cha Agosti 2019, kwamba Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh. 2,289.1 ikilinganishwa na wastani wa Sh. 2,273.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Kuhusu maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka 2020/21, Dk. Mpango alisema matumizi ya serikali yanakadiriwa kuongezeka hadi Sh. trilioni 34.36, sawa na asilimia 21.7 ya Pato la

INAENDELEA UK 26

# Mtendaji mbaroni tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma, inamshikilia Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mapanga wilayani Chamwino, David Tengeneza (50), kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 300,000 toka kwa mfugaji ili amruhusu kuingiza ng'ombe 48 aliowatoa Kijiji cha Segala.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alidai ofisa huyo wa serikali alimtisha mfugaji huo kwamba asipotoa fedha hizo, angechukuliwa hatua za kisheria kwa kukosa kibali cha kuingiza mifugo kijijini kwake.

Kibwengo alisema kushawishi na kujaribu kupokea rushwa ni kosa kwa mujibu wa Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Alidai Takukuru imekuwa ikipokea tuhuma kadhaa dhidi ya ofisa mtendaji huyo kujihusisha na vitendo vya rushwa na kuamua kuanza kumfuatilia katika kituo chake cha kazi.

Alisema baada ya kupokea taarifa mbili tofauti dhidi yake wiki iliyopita, taasisi hiyo iliamua kufuatilia na ilipochunguza ilibaini aliomba rushwa ya Sh. 300,000 kutoka kwa mfugaji huyo.

Kwa mujibu wa Kibwengo, Oktoba 30, mwaka huu, Ofisa wa Takukuru alifuatana na mtoa taarifa hadi ofisini kwa ofisa huyo na mtuhumiwa huyo akamwelekeza mfugaji apeleke fedha chooni ndipo ampatie barua ya kumruhusu kuingiza ng'ombe hao katika Kijiji cha Mapanga, vinginevyo angechukua hatua dhidi yake kwa kutokuwa na kibali.

"Alipomwona mtoa taarifa akiwa na mtu mwingine, alianza kumhoji huku akisisitiza kwamba yeye ni mzoefu na mara kadhaa amekoswakoswa na Takukuru, hivyo kumtaka akaweke fedha hizo chooni.

"Mtoa taarifa alitoka kwenda chooni, lakini hakuacha fedha hiyo ya rushwa na walipoondoka, mtuhumiwa alienda chooni kuangalia na akagundua kwamba fedha hizo hazipo.

"Mtuhumiwa aliamua kumfuata mtoa taarifa na kumtaka arudi na akahoji iweje fedha haipo, naye akamweleza kuwa hawezi kuacha fedha bila kupewa barua, ndipo akaelekezwa aiweke chini ya jiwe lililo chini ya mti nje ya ofisi ya mtuhumiwa na aingie ndani kuandikiwa barua," alisema.

Mkuu wa Takukuru huyo alisema baada ya kuweka fedha chini ya jiwe,

INAENDELEA UK 26

Distributed via ippmedia




SIDO

## SALAM ZA PONGEZI

**UONGOZI pamoja na wafanyakazi wa shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)** tunaungana na watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dk. John Pombe Magufuli** kwa kutimiza **miaka 4 madarakani** kwa mafanikio makubwa.

*Sisi kama SIDO tunajivunia kuwa na Rais mchapakazi, anayejali wananchi wake na anayetaka maendeleo ya nchi yake.*

**Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO**
**P.O.Box 2476, Mfaume Road, Upanga, Dar es SalaamTanzania**
**Tel: Direct +255 222 151 948.**
**E-mail: dg@sido.go.tz. Website: http://www.sido.go.tz.**

215502702



ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

*Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za Sekta za Nishati na Maji iliyoundwa na Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.*

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Perango Group S.L.P 4878 Tanga | Kiwanja Namba 1, Kitalu "A", Kijiji cha Lukozi, Kata ya Lukozi, Wilaya ya Lushoto, Mkoa wa Tanga | Peter Ramsoni Ngowi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Iyegu Filling Station, S.L.P. 37, Kongwa, Dodoma | Kijiji cha Mlali, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma | David Yona Mngurumi (mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | Dominic Filling Station S.L.P. 1007, Mkalama, Singida | Kijiji cha Dominic, Wilaya ya Mkalama, Mkoa wa Singida | Stephano Mlawa Danka (mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 4. | Blue Oil Limited S.L.P 5297 Dar es salaam | Kiwanja Na. 720, Kitalu 11, Mtaa wa Azikiwe, la Dar es salaam | Mohamed Gulam Yasin (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 5. | Encod Limited S.L.P3259 Dar es salaam | Kiwanja Na. 370, Kitalu A, Eneo la Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni, Jiji la Dar es salaam | John Mghanga Hanti (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |

215500802

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU

# Azaki 16 zachangia bil. 236/- kwa miaka mitatu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Twaweza, Aidan Eyakuze, amesema katika utafiti walioufanya kwa kipindi ya miaka mitatu 2016-2018, mchango wa Asasi za kiraia 16 kwenye uchumi wa nchi ni kiasi cha Sh. bilioni. 236.

Eyakuze aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wanahabari baada ya kuwasilisha mada ya mchango wa Asasi za kiraia kwenye uchumi wa nchi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya Azaki inayoendelea jijini hapa.

Alisema kiasi hicho cha fedha kilichopatikana kutokana na Asasi za kiraia kwa kipindi cha miaka mitatu ni sawa na kilo 2,181 za dhahabu zinazosafirishwa na kuuzwa nje.

"Lakini pia kiasi hicho cha fedha ambacho kimechangiwa na Asasi hizi 16, kwa kipindi hicho ni sawa na serikali kuingiza watalii 42,316 na kukaa nchini kwa wiki moja au ni sawa na lita 247 milioni za petroli, dezeli na mafuta ya taa,"alisema Eyakuze.

Pia, Eyakuze alisema katika kipindi cha miaka mitatu 2016/18 kiasi cha kodi ambayo imelipwa na Azaki hizo 16 kwa serikali ni Sh. bilioni 19.

Alifafanua kuwa kiasi hicho cha kodi kilichokusanywa kwa kipindi hicho ni sawa na mapato yatokanayo na maji ya kunywa, vinywaji laini na sigara ya mwaka 2018/19 ambayo yalikuwa ni bilioni 18.8.

"Au kiasi hicho cha kodi kilichokusanywa unaweza kulinganisha kabisa na kodi iliyokusanywa na Mamalaka ya Mapato Tanzania (TRA) 2018/19 katika mikoa ya Rukwa, Lindi, Simiyu, Songwe na Katavi kwa pamoja ambayo makusayo yao ni Sh. bilioni 21," alifafanua Eyakuze.

Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation For Civil Society, Francis Kiwanga, alisema katika wiki ya Azaki moja kati ya shughuli zitakazofanyika ni kongamano linalojumuisha wadau wengine ikiwamo serikali.

Naye Mratibu wa Asasi za kiraia nchini kutoka Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali a Mitaa (Tamisemi), Denis Londo, alisema Asasi la kirai zina mchango mkubwa kwa taifa.



Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, akiangalia michoro iliyoko kwenye mapango ya Kondoa Irangi ambayo ni moja ya urithi wa dunia huko Kondoa, mkoani Dodoma juzi. Mbele ya Kaimu Balozi ni Meneja wa eneo hilo, Zuberi Mabie, akimwonyesha baadhi ya michoro hiyo na historia yake, pamoja na umuhimu wake katika uchumi wa Tanzania kwenye sekta ya utalii. Dk. Patterson yuko mkoani Dodoma kikazi. **PICHA: UBALOZI WA MAREKANI**

# Vigogo Simba waachiwa kwa dhamana

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imewaachia kwa dhamana vigogo wawili wa Klabu ya Simba, Rais wa zamani Evance Aveva na makamu wake, Godfrey Nyange maarufu kama Kaburu, baada ya kutimiza masharti ya dhamana.

Distributed via ippmedia

Aveva na Kaburu wameachiwa baada ya kutimiza masharti ya dhamana kwa kuwa na wadhamini wawili waliotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 30 kwa kila mmoja pamoja na vitambulisho.

Hatua hiyo ilifikiwa jana na mahakama hiyo chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, baada ya kutupilia mbali pingamizi la Jamhuri kwamba mahakama hiyo haiwezi kutoa dhamana mpaka rufani ya kupinga watuhumiwa kuonekana washtakiwa hawana kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka ya kutakatisha Dola za Marekani 300,000 baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha.

Hakimu alisema mahakama yake baada ya kupitia hoja za pande zote mbili kuhusiana na pingamizi la awali la Jamhuri kupinga washtakiwa kuondolewa mashtaka hayo na kwamba wana nia ya kukata rufani, hivyo kesi hiyo isiendelee kusikilizwa.

"Kitendo cha serikali kukata rufani kupitia mawakili wake wa Jamhuri, hakizuii washtakiwa kupata dhamana. Rufani hiyo haiondoi uamuzi wa mahakama hii dhidi ya washtakiwa," alisema Hakimu Simba wakati akitupilia mbali pingamizi hilo na kuruhusu mchakato wa dhamana.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Shadrack Kimaro na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru), Upendo Temu, ulidai kuwa haujaridhika na uamuzi huo, hivyo utakata rufani.

Mapema mahakamani hapo, mahakama hiyo ilisema washtakiwa hao pamoja na mwenzao Zacharia Hansppope wamekutwa hawana kesi ya kujibu katika mashtaka saba ikiwamo kughushi, kula njama, matumizi mabaya ya madaraka, kutoa nyaraka za uongo na kutoa maelezo ya uongo.

Alisema bila kuacha shaka mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa Jamhuri imewaona washtakiwa hao hawana kesi ya kujibu katika makosa ya kutakatisha fedha.

"Ushahidi wa Jamhuri umeshindwa kuleta mashahidi wa kuelezea namna washtakiwa walivyotakatisha fedha hizo. Mahakama yangu inawaona hamna kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka hayo," alisema.

"Washtakiwa mahakama yangu imewaona mna kesi ya kujibu katika makosa ya kughushi, matumizi mabaya ya madaraka na kuwasilisha nyaraka za uongo," aliongeza. Baada ya kuondolewa mashtaka ya kutakatisha, fedha mahakama hiyo imewapa washtakiwa masharti ya dhamana kwa sababu mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo yaliwanyima dhamana hayameondolewa.

Alisema baada ya kuchambua ushahidi wa mashahidi 10 wa upande wa Jamhuri, kwa kuacha shtaka la tano na sita, mahakama imeona washtakiwa wana kesi ya kujibu katika shtaka la kwanza hadi la nne na la saba hadi la tisa isipokuwa katika shtaka la tano na sita la utakatishaji fedha.

Wakili wa utetezi, Nehemia Nkoko, aliomba mahakama kuwapatia wateja wake dhamana kwa kuwa mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo yaliyokuwa yanawanyima dhamana washtakiwa hayapo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri ulidai kuwa haujaridhika na uamuzi huo una nia ya kukata rufani.

Katika kesi ya msingi, shtaka la kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Katika shtaka la pili, Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Kimarekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

Aveva na Kaburu, katika shtaka la tatu, wanadaiwa kwa pamoja kughushi nyaraka iliyokuwa ikionesha Simba inalipa mkopo wa USD 300,000 kwa Aveva kitu ambacho sio kweli.

Pia katika shtaka la nne Aveva anadaiwa katika benki ya CRDB anadaiwa kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa USD 300,000

Aveva anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni alijipatia USD 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Katika shtaka la sita, Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia USD 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na Hans Poppe wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya USD 40,577 huku wakijua kwamba siyo kweli.

Katika shtaka la nane, Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya USD 40,577

Shtaka la tisa, Aveva, Kaburu na Hanspope wanadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kuonesha kuwa Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya USD 40,577.



## HABARI KITAIFA

# Wilaya tatu zapewa mil. 110/- sekta za elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya elimu na afya zimewezeshwa kwa msaada kwa lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Katika kukabiliana nazo, zimepewa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 110 katika wilaya tatu.

Benki ya NMB ndiyo iliyofanya uwezeshaji huo na wilaya zitakazonufaika ni Songea mkoani Ruvuma, Tabora na Ukerewe mkoani Mwanza. Thamani ya misaada hiyo ya vifaa vya ujenzi na vifaa tiba, vinaifanya benki hiyo kutumia zaidi ya Sh. milioni 900 kununulia na kukabidhi vifaa hivyo kwa shule za msingi, sekondari, zahanati na vituo vya afya nchini kwa mwaka 2019.

Wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, imekabidhiwa misaada ya vifaa vya ujenzi, elimu na afya yenye thamani ya Sh. milioni 75 kwa shule 14 za msingi na sekondari, Chuo cha Ualimu Marutunguru na Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe.

Msaada huo, ulitolewa na Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Augustino Abraham na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, (DC), Corneli Magembe, ambaye aliishukuru benki hiyo kwa uwezeshaji huo, alioutaja kama unaoenda kumaliza tatizo la uhaba wa vifaa kwa taasisi husika.

Mkoa wa Tabora, umekabidhiwa viti na meza wenye thamani ya Sh. milioni 30 kwa shule sita za Manispaa ya Tabora, tatu zikiwa ni za sekondari na nyingine tatu za msingi, msaada ambao ulipokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Erick Komanya.

Hafla hiyo ilifanyika Sekondari ya Wavulana Tabora, ambako Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, alikabidhi mabati 216, mbao na misumari vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 15, kwa ajili ya Shule za Msingi Kanyenye, Kalunde na Ikomwa.

Aidha, NMB imetoa msaada wa mabati 175 ya geji 28, yenye thamani ya Sh. milioni 5, kwa ajili ya Shule ya Msingi Ndelenyuma, iliyopo katika Halmashauri ya Madaba, wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Akizungumza kabla ya kukabidhi bati hizo katika hafla ambayo ilifanyika katika Shule ya Msingi Ndelenyuma, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, alisema kwa miaka kadhaa sasa benki hiyo imekuwa mstari wa mbele kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Mpaka ninavyoongea leo, kwa mwaka huu 2019 pekee, tayari NMB tumetoa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 900, tumejikita zaidi kwenye miradi ya elimu, afya na majanga," alisema Shango wakati wa hafla ya makabidhiano hayo yaliyofanyika wilayani Songea.

# Wenye mahitaji maalum ya kijamii wachangishiwa fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WATU wenye mahitaji maalumu katika jamii wamechangishiwa fedha kwa ajili ya kupata huduma hizo ikiwamo mradi wa upatikanaji wa majisafi na salama.

Mahitaji mengine ni vyoo na ujenzi wa kituo cha kufundishia kwa njia ya mtandao katika Shule ya Sekondari ya Mtakuja iliyopo eneo la Kunduchi jijini Dar es Salaam.

Jukumu hilo lilitekelezwa na Klabu ya Rotari ya Bahari jijini Dar es Salaam hivi karibuni kwa ufadhili wa Benki ya NBC.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na wa Kati wa NBC, Evance Luhimbo alisema benki hiyo kwa miaka kadhaa imekuwa ikishughulisha katika kusaidia shughuli za jamii katika maeneo mbalimbali kama elimu, afya na masuala ya ujasiriamali.

"Sisi ni jukumu letu kama benki kurudisha katika jamii sehemu ya faida tuipatayo katika biashara yetu, ni benki kongwe yenye uzoefu katika kutoa huduma bora za kibenki kwa zaidi ya miaka 52, hivyo tutaendelea kusapoti miradi kama hii yenye kuleta tija katika jamii," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya kupokea maombi ya kuchangia hafla hiyo katika Klabu ya Rotari, benki yao haikusita kuitikia wito kwani ni imani jamii ikiwezeshwa kiuchumi na kielimu na jamii ikiwa na afya bora, inaweza kuchangia vizuri katika kuleta maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Aidha, Lhimbo alitaja baadhi ya shughuli za kujamii ambayo wamefanya ni kutoa vifaa vya ujenzi wa madarasa katika shule za mkoani Lindi, Zanzibar, msaada wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro pamoja na kutoa elimu ya masuala ya kifedha na ujasiriamali katika shule mbalimbali nchini.

Baadhi ya miradi ambayo imeshafanikishwa na Klabu ya Rotari ya Bahari ni matibabu ya moyo kwa watoto katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ukarabati wa maktaba katika Shule ya Msingi Buyuni na upanuzi wa kituo cha mafunzo ya ufundi stadi katika kituo cha masista cha Carmel, Kurasini. Mingine ni ukarabati wa maktaba katika Shule ya Sekondari ya Mtakuja pamoja na kutoa misaada ya aina tofauti katika vituo vingine vya walemavu na wasiojiweza.



Mafundi wakichanganya saruji na mchanga kwa ajili ya kufyatua matofali ya kujenga jengo la maabara ya Shule ya Sekondari Jaji Dani Mapigano Memorial iliyopo Kata ya Bugoji Musoma Vijijini, mkoani Mara, juzi, ambayo inatarajia kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | SHABANI NASSORO BUGE (TAWI LA ILALA) | SHABANI NASSORO BUGE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MGEULE JUU CHANIKA – WILAYA YA ILALA | 20/11/209 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | GRACE KENNETH REMMY (TAWI LA TEMEKE) | GRACE KENNETH REMMY | KIWANJA KILICHOENDELEZWA KILICHOKO MTAA WA KISUKURU KATA YA KISUKURU – WILAYA YA ILALA | 22/11/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | AMRI BAKARI MAKANYA (TAWI LA TEMEKE) | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MZINGA KATA YA KITUNDA - WILAYA YA ILALA | 22/11/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 004 | HUSSEN ABDALLAH CHANDE (TAWI LA TEMEKE) | HUSSEN ABDALLAH CHANDE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MSUFINI KATA YA CHAMAZI – WILAYA YA TEMEKE | 25/11/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 005 | RAHABU ERASTO MESSO (TAWI LA TEMEKE) | RAHABU ERASTO MESSO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA KWEMBE KATA YA KWEMBE – WILAYA YA UBUNGO | 27/11/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

Masharti ya mnada
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, AU
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 669,
DAR ES SALAAM
Tel+255 02221183403

Maseto Auctioneer,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU
+255 787 288 442 AU
+255762 260 787



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**WILAYA NYAMAGANA MWANZA**

**RM. COMMERCIAL CASE NO. 32/2019**

**MDAI: ..................................................ACCESS BANK LIMITED**

**DHIDI YA**

**WADAIWA:.............................1. LOLO INVESTMENTS**
**2. COLLENS MASAI BUTAMBALA**
**3. LOSINYARI LAIDSON MALLELI**
**4. CRESCENCIA JOSEPH SHAYO**

**KWA: LOLO INVESTMENTS NA WENZAKE**
**POPOTE WALIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mdai tajwa hapo juu amefugua madai dhidi ya LOLO INVESTIMENTS na wenzanke. Mahakama imepanga kutajwa kwa shauri hili tarehe 06/11/2019, saa 2:30 Asubuhi. Hivyo unatakiwa kuwepo Mahakamani tarehe hiyo na usipohudhuria Mahakama itapanga tarehe ya kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii tarehe 24 Octoba, 2019 leo tarehe 24/10/2019.

..........................
**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**MWANZA**

RESIDENT MAGISTRATE MWANZA

215502902



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**WILAYA NYAMAGANA MWANZA**

**RM. CIVIL CASE NO. 25/2019**

**MDAI: ....................................ACCESS BANK TANZANIA LIMITED**

**DHIDI YA**

**WADAIWA:....................................1. THOMAS CHUBWA KAPERA**
**2. DOROTHEA AMOSI BUTTA**

**KWA: THOMAS CHUBWA KAPERA NA**
**DOROTHEA AMOSI BUTTA**
**POPOTE WALIPO.**

**KUITWA SHAURINI**

Mdai tajwa hapo juu amefugua madai dhidi ya Thomas Chubwa kapera na Dorothea Amosi Butta. Mahakama imepanga kutajwa kwa shauri hili tarehe 08/11/2019, saa 2:30 Asubuhi. Hivyo mnatakiwa kuwepo Mahakamani tarehe hiyo na msipohudhuria Mahakama itapanga tarehe ya kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii tarehe 05 Novemba, 2019 leo tarehe 05/11/2019.

RESIDENT MAGISTRATE MWANZA

..........................
**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**MWANZA**

215502902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Malalamiko ya uchaguzi S/mitaa yapatiwe suluhu*

**KUNA** malalamiko mengi kutoka kwa vyama vya upinzani kuhusiana na mchakato wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uchaguzi wa serikali za mitaa, ambao unatarajiwa kufanyika nchini kote Novemba 24, mwaka huu.

Malalamiko hayo yanahusu wagombea katika maeneo kadhaa kunyimwa fomu za kugombea na mengine yanahusu kukataliwa na watendaji wa ngazi husika kuzipokea fomu hizo hadi juzi ambayo ilikuwa siku ya mwisho, huku jana ikiwa siku ya mchakato wa uteuzi.

Kimsingi, kulikuwapo na malalamiko ya wagombea kadhaa kuchaniwa fomu, baadhi kutekwa, kupigwa na mengine ambayo yanahusu vitendo vya kihalifu, ambavyo havipaswi kupewa nafasi katika nchi yetu ambayo wananchi wake wameishi katika misingi ya umoja wa kutaifa na amani kwa miaka yote tangu Uhuru kutoka kwa wakoloni.

Katika maeneo kadha, watendaji ambao ndio maofisa wasimamizi wa uchaguzi huo wametoa majibu kuhusiana na malalamiko hayo, lakini majibu mengi hayatoshelezi na yanaacha shaka.

Matumaini yetu ni kuwa kwa kila mmoja wetu kama taifa, Tanzania ni muhimu na ya kwanza na uchaguzi ni baadaye uwe wa serikali za mitaa au uchaguzi mkuu. Tunalisema hili na kuweka msisitizo huu kwa kuwa uchaguzi utapita na Tanzania itaendelea kuwapo milele.

Hatuoni sababu za kuwapo ugomvi, vitisho, malumbano na kila aina ya matukio yanayoashiria kuwa jamii yetu haithamini umuhimu wa amani na umoja wa kitaifa, badala yake kuthamini itikadi za vyama vya kisiasa, ambazo hazina tija katika afya ya taifa letu.

Kila mmoja anapaswa kuelewa kuwa uchaguzi sio vita bali ni kushindana kwa kujenga hoja pamoja na washindani kujenga utamaduni wa ustaarabu na kuvumiliana kwa kuwa wote tunajenga taifa moja.

Hayo ndiyo waliyoyasisitiza na kuyahimiza waasisi wa taifa letu kwa miaka yote waliyoishi duniani, ikiwamo baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mapema miaka ya tisini.

Kwa kuwa kuna malalamiko mengi, ni vizuri kushughulikiwa na serikali kwa kuwa ndiye msimamizi wa uchaguzi huo kupitia Waziri mwenye dhamana ya Tamisemi, Selemani Jafo.

Kuna njia nyingi za kuchukua kwa ajili ya kuyapatia ufumbuzi. Kubwa ni kukutana na viongozi wa vyama vyote vya siasa ambavyo vimesimamisha wagombea, ambavyo vinadai kuwa wagombea wao wamefanyiwa rafu ili kama kuna ukweli haki itendeke, hivyo muafaka kupatikana.

Pili maeneo ambayo yatabainika kuwa wagombea wa vyama hivyo hawakutendewa haki muda uongezwe ili warejeshe fomu zao ili wasimamishe wagombea katika vijiji, mitaa na vitongoji.

Mambo hayo yakifanyika, yataondoa dhana iliyojengeka kuwa wagombea wa upinzani wanafanyiwa rafu kwa lengo la kukibeba chama tawala, hivyo kutoa picha kuwa mambo hayo yatajirudia tena mwakani katika uchaguzi mkuu na kusababisha usiwe huru na haki.

Ikiwa vyama havitarudishwa na hatua zitakazochukuliwa na Waziri Jafo, baada ya kumpelekea malalamiko, hatua nyingine vinavyoweza kuchukua katika kudai haki ni kwenda mahakamani.

Tunaendelea kuhimiza uwajibikaji wa wadau wote wa uchaguzi huu ili uwe huru na haki, hivyo kuweka mazingira mazuri ya uchaguzi mkuu wa mwakani.

Tukijenga utamaduni wa kufanya uchaguzi wa ushindani katika mazingira ya haki na usawa, ni dhahiri kuwa amani, utulivu na umoja vitadumu katika taifa letu na hakika tutakuwa tunawaenzi kwa vitendo waasisi wetu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanasiasa kumbukeni dhana ya asiyekubali kushindwa...

Na Sabato Kasika

**WAKATI** nchi ikielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, Chama cha ACT- Wazalendo, kimetamba kupokea wanachama wapya 98 waliojiunga na chama hicho mwishoni mwa mwezi uliopita.

Distributed via ippmedia

Kwa mujibu wa kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, wanachama hao wapya wametokea katika vyama vya CCM na CUF waliojiunga kutoka maeneo mbalimbali ya jijini Dar es Salaam.

Sababu kubwa inayoelezwa na Kabwe ni kwamba wamekimbia kutokana na kutoridhishwa na mchakato wa kura za maoni ndani ya vyama vyao wa kupata wawakilishi katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Zitto anasema, wenyeviti 38 wa zamani wa mitaa na wajumbe wao wametoka chama cha CUF, wakati wenyeviti wa zamani 52 wa mitaa wamejiunga wakitokea CCM.

Kiongozi huyo anasema, sifa ya chama bora ni kile ambacho kina idadi kubwa ya wanachama wakiwamo wageni wengi na kwamba wingi huo wa wanachama unaashiria kukua na kukomaa kwa chama chake.

Pamoja na kwamba Zitto anataja sababu za wageni hao kujiunga na chama chake, lakini kuna haja ya kutafakari hamahama hiyo ambayo imekuja wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kwanza kabisa ieleweke kuwa katiba na sheria za nchi, chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, uwapo wa vyama vya upinzani ni takwa la kikatiba, na hakuna kosa mtu kuhama chama kimoja kwenda kingine.

Kujiunga na chama chochote kile pia ni hiari, hakuna sheria, ambayo inamlazimisha mtu kuwa mwanachama wa chama chochote isipokuwa kama anataka kuwania nafasi ya uongozi wa kisiasa, sharti awe na chama.

Hivyo suala la kuhama chama ni hiari ya mtu kutokana na atakavyoona na utashi wake mwenyewe, lakini kuna haja ya kuangalia sababu ambazo zimekuwa zinatajwa na wale wanaohama.

Lakini ni vyema kujadili kidogo jambo hili, kwani inaonekana kama baadhi ya wanasiasa wanadhani kuwa uongozi ni haki yao, vinginevyo wasipochaguliwa wanaona kama wameonewa na kuamua kuhama.

Mfano mmojawapo ni wa hao waliojiunga na ACT- Wazalendo wakidai kutotendewa haki kwenye kura za maoni, katika mchakato wa kupata wawakilishi wa chama kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wanasahau kwamba asiyekubali kushindwa siyo mshindani! Kwanini wasikubali na kuungana na wale waliopendezwa? Kwanini wakimbie chama baada ya kushindwa katika kura za maoni?

Kwanza nieleweke kwamba sipingani na suala la kuhama chama, ila ninapingana na sababu zao, ambazo kimsingi zinaonyesha hawatambui kuwa asiyekubali kushindwa siyo mshindani.

Zipo sababu za msingi, ambazo ninaamini kwamba hasa kwenye imani ya chama kama mtu anaona imani hiyo inakwenda kinyume na kile unachoamini, basi hana budi kuondoka kutafuta imani hiyo kwingine.

**Pamoja na kwamba Zitto anataja sababu za wageni hao kujiunga na chama chake, lakini kuna haja ya kutafakari hamahama hiyo ambayo imekuja wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.**

Vilevile sera za chama zinaweza kumfanya mtu akaamua kuhama chama kimoja kwenda kingine.

Kama atakuwa ni kiongozi, basi atakuwa alishajaribu kushawishi vinginevyo kupitia vikao husika bila mafanikio, na kulazimika kuachia ngazi na kuhama chama chake cha awali.

Wakati kwa viongozi ikiwa hivyo, kwa wanachama wa kawaida, wao kwa kawaida huwa wanaangalia kama anavutiwa na sera na imani ya chama au la na mwishoni wa siku wanafanya maamuzi.

Iwapo imani ya chama ni tofauti na jinsi mwanachama anavyoamini, basi atakuwa hana uwezo wa kushawishi mabadiliko juu ya imani hiyo, na kitakachofuata ni kuhama chama hicho tu.

Mwanachama anapofanya uamuzi wa kuhama chama kutokana na mazingira ya aina hiyo, haimaanishi kwamba amekisaliti, bali imani yake haiendani na sehemu aliyopo, hivyo hana budi kwenda kwingine.

Lakini mchezo wa kuvizia kwenye kura za maoni na kushindwa, kisha kukimbia chama kwa madai ya kuonewa katika mchakato wa kura za maoni, ni sawa na mtu asiyekubali kushindwa.

# Wanusurika kifo ajalini

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WATU 33 wakiwamo vichanga viwili, wamenusurika kufa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupinduka huko Chamanangwe Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Walionusurika ni Khamis Omar Hamad (25) mkazi wa Pamndani ambae ni dereva, Bama Sali Juma (40), Juma Mbarouk Salim (30, Suleima Hamad Salim (30), Faisal Said Omar (28), Mayasa Said Vhangule (30), Muzne Othman Salim (4), Vuai Haji Vuai (38), Arif Ahmed Ali (09), Mohammed Bakar Hamad (63), Khami Mbarouk Hamad (45) na Ali Mbarouk Salim (30).

Wengine ni Ali Abuu Haji (39), Sada Massoud Saleh (30), Aziza Kassim Mohammed, Mwanaisha Ali Kabele Shaibu Mussa Mbarouk (35), Rukia Ahmed Salim (40), Hamifa Ismail Bakar, Safia Ali Juma (30), Salim Haji Bakar (25) na Ali Mohammed Khamis (25).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Sheikhan Mohammed Sheikhan, alisema tukio lilitokea wakati gari hilo lilipokuwa linateremka kilima cha chamanangwe, hivyo kuvamia kisiki cha mvinje na kupinduka.

Alieleza tukio hilo lilitokea juzi jioni ambapo gari hilo lenye namba za usajili Z1146 AH aina ya Canter iliyokuwa ikitoka Chake Chake kuelekea Wete.

Kamanda Sheikhan alisema majeruhi walikimbizwa katika hospitali ya Vitongoji Wete na Mkoani kwa ajili ya matibabu zaidi.

'Tunashukuru hakufa mtu licha ya kuwa hii ni ajali mbaya sana, kwa upande wa majeruhi walikimbizwa katika hospitali za Wete, Vitongoji na Mkoani, na kwa wale ambao hawakuumia sana baada ya huduma ya kwanza waliopatiwa Hospitali ya Vitongoji waliruhusiwa na kurudi nyumbani," alisema Kamanda Sheikhan na kuongeza kuwa chanzo cha ajali hiyo ni kutokana na mwendo wa kasi kwa kuwa dereva wa gari alikuwa anafukuzana na gari lingine ambalo lilikuwa mbele yake.

"Dereva ni miongoni mwa walioumia vibaya kichwani, na bado yuko Hospitali ya Mkoani akipatiwa matibabu zaidi, " 'alieleza Kamanda Sheikhan.

Aliwataka madereva kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima.

Nae Katibu wa Hospitali ya Wete, Soud Haji Sadala, alieleza kuwa alipokea majeruhi saa 4:30 usiku ambapo wanaume walikuwa ni wanane, wanawake wawili na watoto wawili.

Hata hivyo alieleza kuwa kutokana na ushirikiano wa madaktari, majeruhi walipatiwa matibabu na wanaume wote pamoja watoto wamesharuhusiwa.

Nae Muzne Othman, mmoja wa majeruhi alielazwa katika ya Wete, alisema chanzo cha ajali ni mwendo wa kasi kutokana na dereva kufukuzana, na kwamba ameumia seheme za kifuani na anaendelea vizuri na matibabu.

# Aliyefungwa minyororo miezi 2 achukuliwa na mama yake

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHADRACK Johanes (26), mkazi wa Oldshinyanga Manispaa ya Shinyanga ambaye alikuwa amefungwa minyororo chumbani kwa miezi miwili, amechukuliwa na mama yake mzazi, kwenda naye jijiji Mwanza kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Inadaiwa kuwa Shadrack anasumbuliwa na ugonjwa wa akili.

Mama huyo, Nonja Kalala, akizungumza wakati wa makabidhiano na mratibu wa magonjwa ya afya ya akili kutoka Zahanati ya Oldshinyanga, Brigita Nyangare, ambaye alikuwa amekabidhiwa na serikali kumpatia matibabu kijana huyo, alisema ameamua kumfuata mtoto wake ili akamuuguze yeye mwenyewe kwa ukaribu.

Kalala alisema alisikitika sana kuona taarifa ya mwanawe kwenye gazeti la Nipashe juu ya mateso ambayo alikuwa akipewa na shangazi yake pamoja na kaka yake, ya kufungiwa ndani miezi miwili, huku akiwa uchi wa mnyama, akijisaidia pamoja na kula chakula humo humo, kitendo ambacho kilimuuma na kuamua kwenda kumchukua.

"Kijana wangu huyu nalijua tatizo lake la kurukwa na akili, ambapo mwaka jana nilikuwa naishi naye mimi jijini Mwanza, na baba yake... tumeshatengana zamani ambapo yeye anaishi Bukoba na mke mwingine, nilikuwa nampatia matibabu hadi akapona kabisa, lakini ghafla akanitoroka na kurudi huku Shinyanga," alisema Kalala.

"Baada ya kunitoroka nikafanya mawasiliano na shangazi yake pamoja na kaka yake wakasema wapo naye huku Shinyanga, na nilikuwa nikiulizia juu ya taarifa zake mara kwa mara naambiwa anaendelea vizuri, kumbe mwanangu anafanyiwa ukatili na bila gazeti la Nipashe kuandika taarifa zake nisingejua," aliongeza.

Aidha, alisema anawasamehe ndugu zake, ambapo alikuwa amepanga kuwafungulia mashtaka, na kubainisha atakachokifanya ni kuondoka na kijana wake kwenda kumpatia matibabu.

Naye Shadrack akizungumza kwa shida, kutokana na afya yake kuzorota kutokana na kufungiwa ndani siku nyingi, alisema anafurahi kujiwa na mama yake kwenda naye kuishi jijini Mwanza na kuomba apatiwe matibabu.

Naye Nyangare, alisema wamemruhusu mama wa kijana huyo kuondoka naye ili akampatie matibabu kwa ukaribu.

Nao ndugu zake na Shadrack ambao walikuwa wakiishi naye akiwamo shangazi yake, Devota Emmanuel, alisema hana tatizo na mtoto huyo wa kaka yake, ingawa walishindwa namna ya kumsaidia ndipo ikabidi wa mfungie ndani, huku akimruhusu wifi yake aondoke na kijana wake ili akampatie matibabu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Shinyanga, Panuela Samuel, alitoa wito kwa wazazi au walezi, pale wanapoona mtoto wao anakabiliwa na tatizo la kurukwa na akili wampeleke hospitali kupatiwa matibabu ikiwamo Mirembe, badala ya kumfungia ndani, kwa kuwa huo ni ukatili na kukiuka haki za binadamu.




Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Simon Karikari, akiongea na wateja wa kitengo cha Tigo Business jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa huduma na bidhaa zilizoboreshwa zaidi pamoja na tovuti inayompa mteja mamlaka ya kujihudumia na kudhibiti matumizi ikiwa na lengo la kuzisaidia kampuni mbalimbali kukuza huduma zao kidigitali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauza vipodozi watakiwa kuvisajili

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYABIASHARA wa vipodozi nchini wameshauriwa kusajili vipodozi wanavyouza hatua itakayowasaidia kutambua kwa urahisi vilivyopigwa marufuku kutokana na kuwa na viambata vya sumu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkaguzi Mwandamizi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mhandisi Donald Manyama, wakati akizungumza na waandishi wa habari walipokuwa wakifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya vipodozi yaliyopo Mwenge, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Manyama alisema kila muuzaji wa vipodozi inabidi asajiliwe kwenye kupitia tovuti ya shirika hilo au kama sio yeye basi anayemsambaziwa vipodozi inabidi awe amesajiliwa.

Kwa upande wa vipodozi ambavyo havijasajili, Mhandisi Manyama alisema watakuwa wakivipeleka kwenye maabara za shirika ili kuvipima kujua kama vinafaa kwa matumizi ya binadamu.

Alisema wauzaji wengi wa vipodozi hawajajisajili, hivyo kupitia ukaguzi huo wananawapa elimu kuhusu umuhimu wa kusajiliwa kupitia tovuti ya shirika wakion6yesha kila aina ya vipodozi wanavyouza.

Kwa wale ambao hawatafanya hivyo, Manyama alisema shirika limejipanga kuhakikisha operesheni hiyo ya kuondoa vipodozi hivyo kwenye soko nchini kote inafanikiwa sambamba na kutoa elimu kwa jamii kwa njia mbalimbali.

Alisema jukumu hilo wameanza kulitekeleza kuanzia Julai, mwaka huu baada ya baadhi ya majukumu yaliyokuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) kuhamishiriwa kwenye shirika hilo.

Alipoulizwa madhara ya vipodozi hivyo vyenye viambata sumu kwa matumizi ya binadamu, Manyama alisema vina madhara kwenye ngozi ya binadamu.

"Kwanza vinaichubua hiyo ngozi na kuifanya kuwa laini kiasi kwamba mtumiaji akifanyiwa operesheni ushonaji wake unakuwa ni mgumu," alisema na kuongeza:

"Vingine vinasababisha saratani, hivyo tunawashauri hata watumiaji kuacha kutumia vipodozi hivyo. Wengine wanavitumia bila kufahamu, wakiona mwenzao amebadilika ngozi, wanadhani havina madhara.

Vipodozi vilivyopigwa marufuku kutokana na kuwa na viambata sumu ambavyo vilikamatwa juzi katika maduka na saluni zilizopo ni Skin Balance, Jaribu, Mont Claire, Epiderm, Rapid Claire, Betasol, Oranvate, Pure White na Sivop.

Aina hiyo ya vipodozi ni tofauti na vilivyokamatwa hivi karibuni kwenye ukaguzi uliofanyika Kariakoo wilayani Ilala, jijini Dar es Salaa.

Kwenye ukaguzi huo vipodozi zilivyokamatwa na na kuondolewa sokoni ni Corolight, Movate, Coco Pulp, Diproson, Viva White, Carotone, Bronz na Eclair.

Vingine ni Citrolight, Tent Clear, Tender White, Clinic Clear, TCD, Baby Face, Light up, Dermotyl na Top Lemon. Mmoja wa wauzaji wa vipodozi hivyo, John Paul, alisema kuwepo kwa aina nyingi ya vipodozi vyenye viambata sumu ni kielelezo kuwa elimu inatakiwa kutolewa kwa watumiaji hasa wanawake ambao ndiyo waathirika wakubwa.



JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

OFISI Y ARAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

**NOVEMBA 5, mwaka huu Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, unatimiza miaka minne madarakani.**

Distributed via ippmedia

# TAMISEMI YAJIVUNIA MAFANIKIO TISA CHINI YA JPM

***Na Augusta Njoji, DODOMA***

Katika kutimiza miaka hiyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi) ni miongoni mwa wizara zinazojivunia mafanikio makubwa chini ya uongozi wake.

Mafanikio hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, Hospitali na vituo vya afya, mapinduzi sekta ya elimu kupitia mpango wa elimu bila malipo, ukusanyaji mapato, utoaji wa mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Mengine ni nidhamu kwa watumishi wa umma, uwepo wa tuzo maalum kwa wahitimu wa shule za msingi na sekondari waliofanya vizuri ili kuchochea ufaulu kwa wanafunzi na ujenzi wa viwanda vidogo.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tamisemi, Selemani Jafo, anasema ofisi yake ndio msimamizi wa mikoa, wilaya, halmashauri, vijiji, vitongoji na mitaa anajivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kipindi hicho ikilinganishwa na kipindi kilichopita.

"Ni wizara inayogusa watu kwa upana wake tulipotoka ilikuwa ni miongoni mwa wizara zilizokuwa zikilalamikiwa sana, kwa mfano mtakumbuka Rais alipokuwa akihutubia Bunge la 11 alisema wizara imekuwa na miradi isiyokamilika, miradi isiyo na viwango, uzembe, ufujaji fedha za umma na mambo mbalimbali,"anasema. Anasema ofisi hiyo ndio yenye mambo mengi kwa mustakabali wa watu na maendeleo ya nchini.

"Namshukuru Rais kwa kunipa fursa ya kuhudumu katika Wizara hii ipo chini ya Ofisi yake mwenyewe, awali alinipa jukumu la kuwa Naibu Waziri na sasa ni Waziri kamili ni mwaka wa nne nipo ndani ya Wizara hii,"anasema

Anasema Ofisi hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kwenye nyanja mbalimbali kwa kipindi cha miaka minne.

## MIUNDOMBINU

Anasema katika sekta ya miundombinu ya barabara kupitia wakala wake wa barabara mijini na vijijini(Tarura), Tamisemi inasimamia kilometa 140,000 ambapo awali zilikuwa kilometa 108,000.9.

"Katika maeneo haya Tamisemi imefanya kazi kubwa kwa kipindi cha miaka minne, kwanza ujenzi wa madaraja, kuimarisha barabara, na kuwapa fursa wananchi kufika maeneo mbalimbali kwa kurahisisha usafiri wa kusafirisha mazao au bidhaa mbalimbali zinazoimarisha uchumi wa nchi yetu.



*Stendi ya mabasi iliyojengwa katika Manispaa ya Singida kupitia mradi wa uendelezaji na uimarishaji wa Halmashauri za Miji (ULGSP) unaosimamiwa na OR-TAMISEMI*

"Mchakato wa ujenzi wa barabara katika miji, majiji na manispaa hapa nchini ni jambo la kujivunia sana, katika eneo hili tuna mradi wa TSCP ambao unagusa majiji, manipaa jumla nane ambayo ni Tanga, Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya na Manisapaa ya Ilemela, Kigoma ujiji na Mtwara Mikindani,"anasema

Anabainisha kuwa zaidi ya Sh.Bilioni 840 zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo hayo kwa kujenga barabara, mifereji, masoko, stendi za kisasa, ufungaji taa za barabara,mitambo ya taka ngumu, na madampo ya taka.




*Ujenzi wa soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe kupitia Mradi wa uendelezaji na uimarishaji wa Halmashauri za Miji (ULGSP) unaosimamiwa na OR-TAMISEMI*

"Mradi mkubwa unabadilisha miji kwa kiwango kikubwa sana, eneo hili najivunia sana kwa kuwa miji imebadilika sana kutokana na kazi kubwa ambayo Tamisemi imefanya.

Buza, kuweka taa za barabarani, kubadili mitaa iliyokuwa imejengwa kiholela 14.



*Stendi ya mabasi iliyojengwa katika Manispaa ya Singida kupitia mradi wa uendelezaji na uimarishaji wa Halmashauri za Miji (ULGSP) unaosimamiwa na OR-TAMISEMI*

"Pia kuna mradi DMDP ambao unagusa jiji la Dar es salaam katika mradi huu zinatumika Sh.Bilioni 660 fedha hizi zinajenga mtandao wa barabara za lami, mifereji, masoko na kituo cha Afya

"Mradi huu unabadilisha kabisa mtazamo wa jiji la Dar es salaam, ndio maana ukiona mto ng'ombe na mito mingine yote tunarekebisha vizuri kurudi katika hali ya kisasa, kijichi utaona barabara inayounganisha mbagala kuu na eneo la kibada tumejenga barabara nzuri na kujenga madaraja mazuri katika mto Mzinga na Twangoma, tumepata faraja kubwa sana,"anasema.



*Ujenzi wa barabara ya Kijichi – Toangoma katika Manispaa ya Temeke Jijini Dar es salaam. Barabara hii imejengwa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam (DMDP) unaosimamiwa na OR-TAMISEMI*

Kadhalika, anasema kuna mradi wa kuboresha Manispaa na Majiji takribani 18, mradi huo unajenga barabara za lami, taa za barabarani, mifereji, stendi za kisasa, masoko na mambo mengine.

"Lengo ni kufanya manispaa zetu kuwa za kisasa ndio maana leo ukipita manispaa ya Bariadi, Tabora, Lindi, Moshi, Babati, Singida, Kahama, Sumbawanga, Rukwa na mengine yamebadilika kutokana na ujenzi wa miundombinu hiyo.

"Hii ni juhudi kubwa inayofanya na Rais Magufuli, katika miradi mikubwa zaidi ya Sh.Trilioni mbili zimetumika hadi sasa kuhakikisha inaboresha miundombinu,"anasema.

## SEKTA YA AFYA



Jafo anasema Tamisemi imepewa jukumu la kusimamia Afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya wilaya.

"Kabla ya Rais John Magufuli kuingia madarakani nchi yetu ilikuwa na vituo vya Afya 115 vilivyokuwa na uwezo kwa kufanya huduma ya upasuaji lakini kwasasa serikali chini ya Tamisemi tumejenga vituo 352 vilivyo na uwezo wa kufanya upasuaji,"anasema.

Anabainisha kuwa tangu nchi ipate Uhuru kulikuwa na Hospitali za wilaya 77 lakini mwaka huu zinajengwa Hospitali za wilaya 69.







Shule kongwe ya Dodoma sekondari iliyofanyiwa ukarabati na Tamisemi hivi karibuni.

"Katika mpango wetu wa bajeti mwaka 2019/20 tunajenga vituo vya afya vingine 52, hivyo kwa kipindi cha miaka miwili tutakuwa na vituo vya afya 404 vilivyojengwa chini ya utawala wa zilizokuwa zimejengwa tangu Uhuru.

"Eneo hili kazi kubwa imefanyika chini ya Rais John Magufuli, miundombinu hii yote imejengwa



Muonekano wa Shule ya sekondari Pugu iliyokarabatiwa na Tamisemi.

Rais Magufuli, ukilinganisha na vituo 115 ambavyo vilikuwa vinafanya upasuaji tangu tupate uhuru,"anasema.

Aidha anasema kwa mwaka wa fedha 2019/20 zinajengwa Hospitali za wilaya 27 hivyo ndani ya miaka miwili zitakuwa Hospitali 96 ikilinganishwa na 77 kwa utaratibu wa 'Force Account' tukumbuke Hospitali za wilaya zamani ili ujenge ilikuwa inahitajika Sh.Bilioni 24 lakini kwa utaratibu huo tunatarajia kukamilisha ujenzi kwa Sh.Bilioni nne,"anasema.



Waziri huyo anasema kwa vituo vya afya zimetumika kati ya Sh.Milioni 400-500 kwa ujenzi miundombinu katika vituo hivyo, ambapo zamani zilikuwa zinatumika Sh.Bilioni mbili kujenga majengo ya vituo hivyo.

"Kwa hiyo ni mafanikio makubwa sana ambayo Tamisemi tumeyapata kupitia utaratibu ambao tumechagua kuutumia,"alisema.

Aidha anasema Rais ameongeza bajeti ya dawa kutoka Sh.Bilioni 30 hadi Sh.Bilioni 270 ambayo kwa kiwango kikubwa imeimarisha sekta ya afya kwa serikali za mitaa.

"Najivunia kama Waziri wa Tamisemi kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya Afya kwa kujenga vituo vya afya na Hospitali za Afya, Hii miundombinu yote ya afya imegharimu Sh.Bilioni 385.6,"anasema

**Ajira watumishi afya**

Jafo anasema kwa kipindi hicho tumeajiri watumishi kwenye mamlaka za serikali za mitaa ambapo kwa sekta ya afya watumishi 8,917 wameajiriwa.



Kituo cha Afya Kahangara kilichopo katika halmashauri ya Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza

## MRADI MWENDOKASI



Waziri Jafo anasema Mradi wa mabasi yaendayo haraka ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na OR-TAMISEMI ambapo unatekelezwa kwa awamu tatu na imeweza kupunguza foleni na adha ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es salaam.

Anasema lengo la mradi huo ni kuwa na mabasi 305 na kwasasa mabasi yanayotoa huduma ya usafiri ni 140.

"Mchakato wa kumpata mtoa huduma ambaye atawezesha upatikanaji wa mabasi mchakato wake upo katika hatua mbalimbali na atakapopatikana atakamilisha ununuzi pia wa mabasi yaliyobaki na kufikia idadi ya mabasi 305,"anasema.

Jafo anasema kukamilika kwake kutaondoa kero ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es salaam.







**SEKTA YA ELIMU**

Jafo anasema Tamisemi ina jukumu la kusimamia elimu kuanzia shule za awali hadi kidato cha sita.

"Katika sekta hii jambo tunalomshukuru Rais Magufuli ni mpango wa elimu bila malipo ambayo imesaidia kwa kiwango kikubwa watoto wa Tanzania, ambapo takribani Sh.Bilioni 23.86 zinatolewa kila mwezi kugharamia elimu bila malipo,"anasema.

Waziri huyo anasema pia Rais ameamua katika ujenzi wa miundombinu ambapo wameanza kwa kuboresha shule kongwe ambapo zilikuwa zimechakaa na kuhakikisha zinarejea kwenye ubora wake kutokana na awali zilikuwa zimechakaa.

"Wastani wa Sh.Milioni 800 hadi Sh.Bilioni 2 kwa kila shule kwa ajili ya kufanya ukarabati katika shule hizo mpaka sasa tumekamilisha ukarabati wa shule 62 kati ya shule 89,"anasema.

Anaeleza kuwa pia katika shule za msingi na sekondari kazi kubwa ya kuimarisha miundombinu imefanyika.

"Umaliziaji wa maboma Rais ametoa fedha ili kuhakikisha maboma unamaliziwa lakini shule mbalimbali zimejengewa madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu maabara pamoja na mabweni, ndio maana shule za kata tumeziongezea uwezo na kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano na sita,"anasema.

Kadhalika, anasema katika eneo hilo zimetumika Sh.Bilioni 305.1 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na utaratibu uliotumika ni mfumo wa 'force account' na kupata mafanikio makubwa.

**Ajira za walimu**

Jafo anasema idadi ya walimu kwa shule za msingi na sekondari imeongezeka ambapo zaidi ya walimu 18,000 wameajiriwa kuongeza idadi na kuchochea ufaulu.

"Katika matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka 2019 kati ya shule 100 bora, shule 52 zilikuwa za kata haya ni mafanikio makubwa haijawahi kutokea kwa ujumla upande wa elimu Tamisemi tumeendelea kufanya kazi kubwa ambayo haijawahi kutokea,"anasema.

**UTOAJI MIKOPO**

Jafo anasema kwa mara ya kwanza kumekuwa na sheria ya utoaji mikopo kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani sasa mikopo inatoka kwa mujibu wa sheria.

"Tunajivunia kwasababu katika mwaka wa fedha 2018/19 mpaka Agosti 2019 zaidi ya Sh.Bilioni 47 zimetolewa kwa makundi hayo, hii ni mara ya kwanza kutolewa fedha kiasi hichi kwa makundi hayo,"anasema.

Aidha, anasema kupitia fedha hizo watu wamejenga viwanda ili kujenga uchumi wa nchi.

**UJENZI WA VIWANDA VIDOGO**

Anasema mwaka 2017 aliagiza kila mkoa kujenga viwanda vidogo na vya kati 100 ambapo lengo lilikuwa ni kujenga viwanda 2,600 lakini hadi kufikia Desemba 2018, vilikuwa vimejengwa viwanda 4,877 sawa na asilimia 186.75 ya utekelezaji wa lengo.

"Sisi tumechagiza ujenzi lakini Wizara ya Viwanda na Biashara kazi yake ni kuviratibu kuangalia masoko ili waliojenga waweze kunufaika kwa uchumi wa nchi yao,"anasema.

**NIDHAMU YA WATUMISHI WA UMMA**

Jafo anasema kumekuwepo na nidhamu kwa watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kilichopita kwa kuwa nidhamu na utendaji wao umebadilika.

"Nawashukuru wasaidizi wangu Naibu Waziri Josephat Kandege na Mwita Waitara kwa kazi kubwa tunayoifanya ya kuleta mabadiliko kwenye Wizara, pia Katibu Mkuu Mhandisi Nyamhanga na wasaidizi wake wote, maana mafanikio yametokana na utendaji wao mzuri wa kuhakikisha mambo yanasonga mbele,"anasema.

**UKUSANYAJI MAPATO**

Jafo anasema anajivunia ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa na kuanzishwa kwa mfumo wa kutoa matokeo kila baada ya robo ya mwaka.

"Jambo hili limesaidia sana ukusanyaji wa mapato katika mamlaka zetu leo hii ndio maana tunaona mwaka 2018/19, makusanyo yalifika zaidi ya asilimia 91 haijawahi kutokea kwa kipindi kingine chote na tunaimani yataimarika zaidi kwa kuwa suala zima la matumizi ya mifumo ya kielektroniki na uadilifu umesaidia kufanya mapinduzi makubwa,"anasema.

**TUZO MAALUM**

Waziri Jafo anasema kuanzishwa kwa tuzo maalum kwa wahitimu wa shule msingi na sekondari ambapo mwaka huu imezinduliwa tuzo ya kiserikali jambo ambalo linaacha alama chini ya uongozi wake na litatoa motisha kwa walimu kwa kuwa nao wamekumbukwa kwenye tuzo hiyo.

**CHANGAMOTO**

Distributed via ippmedia

Anasema kuna watu wameshindwa kuelewa dhana ya matumizi ya 'force account'katika utekelezaji wa miradi ambapo awali watu walikuwa wanasuasua lakini kwasasa wanaenda vizuri.

"Pia baadhi ya watumishi wachache bado hawajabadilika katika suala zima la nidhamu kazini ndio maana tumeshuhudia maeneo mengine watu wakibadilishwa kutokana na ufujaji na wizi wa fedha kutokana na kuwa na mawazo yale yale, nataka wabadilike waone hichi ni kipindi cha tofauti sana,"anasema.

Jafo anasema changamoto nyingine ni watendaji kukiuka misingi ya ukusanyaji mapato katika matumizi ya elektoniki, wamekuwa wakivujisha mapato yanayotakiwa kukusanywa na serikali.

"Tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kwa watendaji wote ambao wamekuwa wakifanya mambo yasivyo,"anasema.

**KITU ASICHOKISAHAU**

"Nimekuwa Naibu Waziri na Waziri, nilikuwa Naibu Waziri kwa kipindi kifupi lakini Rais amenipa fursa ya kuwa Waziri kwa kipindi kirefu sasa, jambo ambalo sitalisahau, ni heshima niliyopewa na Rais kumsaidia katika Wizara kwa kuwatumikia watanzania, sitalisahau katika maisha yangu. "

"Wizara ina changamoto nyingi, ina mambo mengi, ina vitu vingi lakini Rais amenipa jukumu hili la kumsaidia tangu alipoingia madarakani kwangu mimi maishani mwangu sitasahau kwa imani hii kubwa aliyonipa Rais, naomba nimhakikishie kwamba sitamuangusha hata kidogo katika dhamana hii aliyonipa.Nitawatumikia watanzania kwa uadilifu na uaminifu uliotukuka,"anasema

**WANANCHI WATARAJIE NINI**

Anasema matarajio ni kwenda kujumuisha mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne iliyopita na mwaka wa tano kwenda kuona miji yote ikiwa imekamilika kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango kikubwa, sekta ya afya itakuwa imeimarika kwa kiwango kikubwa.

"Tutakwenda kuona sekta ya elimu itakuwa imeshika hatamu na shule za umma zitakuwa tishio lakini natarajia kuona makundi mbalimbali yaliyokuwa yanaweza sasa kuanza kusimama vizuri kujenga uchumi wao.Hii ndio ndoto ya miaka mitano ya utawala wa Rais Magufuli,"anasema.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
### Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
### Mtaa wa TAMISEMI,



**Uongozi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais –Tamisemi inaungana na Watanzania wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dk.John Pombe Joseph Magufuli kwa kutimiza miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.**

Ofisi ya Rais- Tamisemi inatoa pongezi kwa maendeleo makubwa ambayo yamepatikana kwa watanzania katika uongozi chini ya Mhe.Rais . Aidha inamtakia Mhe.Rais na uongozi wote wa Serikali afya njema ili waendelee kuwaongoza vyema watanzania kufikia uchumi wa kati.

**Mji wa Serikali- Mtumba,**
**S.L.P. 1923, 41185 DODOMA, Anuani ya simu "tamisemi" Dodoma**
**Simu Na:+255 26 2321607, Nukushi+255 26 2322116, Barua pepe:ps@tamisemi.go.tz**



# MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)

## MAMLAKA YA MAJI SAFI DUWASA INAVYOTEKELEZAA MIRADI MBALIMBALI YA MAJI JIINI DODOMA ILI KUENDANA NA UTENDAJI KAZI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO



KATIBU MKUU WA WIZARA YA MAJI, PROF. KITILA MKUMBO (WA TATU KUTOKA KUSHOTO) KATIKA PICHA YA PAMOJA NA VIONGOZI WA WILAYA YA CHEMBA WAKATI WA KUANZA KULIPA FIDIA KWA WANANCHI MWEZI OKTOBA 2019 ILI KUPISHA UJENZI WA MRADI MKUBWA WA BWAWA LA MAJISAFI LA FARKWA ILI KUHUDUMIA MAENEO YA JIJI LA DODOMA, CHEMBA, BAHI NA CHAMWINO.

**1.0 KUHUSU DUWASA**

- DUWASA ilianzishwa mwezi Julai, 1998 kwa mujibu wa kifungu na 3(1) cha sheria Na. 8 ya mwaka 1997 ambayo ilifutwa kwa sheria Na. 12 ya Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 na kufutwa na sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Jukumu la msingi la DUWASA ni kutoa huduma endelevu ya usambazaji Majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Mjini Dodoma.
- DUWASA ilianzishwa ikiwa daraja 'C' ikitegemea ruzuku ya Serikali (Wizara ya Maji) katika uendeshaji (gharama za umeme na mishahara). Hata hivyo, ilipanda kutoka daraja 'C' hadi 'A' mnamo mwaka 2003 na hivyo kujitegemea kwa 100% katika gharama za uendeshaji na sehemu ya uwekezaji.

**1.1 Dira (vision) ya DUWASA**

- Kuwa Mamlaka yenye ufanisi wa hali ya juu katika utoaji wa huduma ya majisafi na salama na usafi wa mazingira katika hali endelevu.

**1.2 Dhima (mission) ya DUWASA**

- Utoaji wa huduma ya majisafi, salama na ya uhakika na usafi wa mazingira kwa wateja wa Mamlaka waliopo mjini Dodoma kwa ufanisi wa hali ya juu, kuwa na watumishi wenye shauku, bidii ya kazi na wanaojituma, kutumia teknolojia sahihi inayokubaliana na mazingira na kuendelea kujibidiisha zaidi ili kuongeza ufanisi na tija.



BODI YA EWURA ILIPOTEMBELEA MAENEO MBALIMBALI YA DUWASA MWEZI SEPTEMBA 2019.

**2.0 HALI YA HUDUMA YA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA MJINI DODOMA**

**2.1 Huduma ya majisafi**

**2.1.1 Mahitaji ya maji**

- Utafiti na stadi za karibuni juu ya mahitaji ya maji kwa wakazi wa mji wa Dodoma ulifanywa mnamo mwaka 2002/2003 na kufanyiwa mapitio 2009.
- Kwa mujibu wa stadi hizo, mahitaji ya maji mjini kwa sasa ni zaidi ya meta za ujazo 48,000 kwa siku.
- Kiasi hiki kinajumuisha mahitaji ya UDOM yanayofiki takribani meta za ujazo 3,000 kwa siku.
- Hata hivyo, kufuatia ujio wa Serikali Makao Makuu ya Nchi - Dodoma, mahitaji ya maji yanaongezeka kwa kasi hali inayoashiria stadi hizi kupitwa na wakati na kuhitaji mapitio.

**2.1.2 Vyanzo na uwezo wa Uzalishaji maji**

- Chanzo pekee cha uzalishaji maji kwa matumizi ya wakazi wa mji wa Dodoma ni visima virefu vilivyochimbwa katika Bonde la Makutupora.
- Jumla ya visima vya uzalishaji maji 24 na visima 5 vya kuchunguza mwenendo wa maji ardhini vimechimbwa katika bonde hili.
- Uwezo wa miundombinu ya visimani kwa sasa pamoja na uwezo wa usafirishaji maji ni meta za ujazo 61,500 kwa siku.

**2.1.3 Uzalishaji halisi**

- Hivi sasa DUWASA inazalisha, kusafirisha na kusambaza wastani wa meta za ujazo 54,000 kwa siku.
- Kiasi hiki cha uzalishaji kimekuwa kikiongezeka kwa kasi siku hadi siku na inatarajia kufikia kiasi cha meta za ujazo 61,500 kwa siku katika kipindi kifupi kijacho.
- Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Jijini Dodoma.

**2.1.4 Usafirishaji na Usambazaji maji mjini**

- Mtandao wa kusafirisha na kusambaza majisafi urefu wa km 533.
- Matenki makubwa 10 yenye jumla ya ujazo wa mita za ujazo 92,670.



MHE. JUMAA AWESO (MB), NAIBU WAZIRI WA MAJI AKIANGALIA MOJA YA VISIMA VILIVYOCHIMBWA KWENYE UJENZI WA MRADI WA MAJI WAKATI WA UJENZI WA MJI WA SERIKALI MTUMBA.

- Mtandao huu pia unajumuisha vituo sita (6) vya kusukumia maji.
- Takribani 80% ya wakazi wa mjini Dodoma ambao ni zaidi ya 500,000 wanapata maji ya DUWASA.
- Maunganisho ya maji hadi Septemba, 2019 ni wateja 45,000.

**2.2 Huduma ya Majitaka**

2.2.1 Mfumo wa kukusanya na kusafirisha majitaka

- Mtandao (lateral sewers na Trunk mains) una urefu wa jumla ya Km 113.75 (Juni, 2019)
- Unahudumia takribani asilimia 20 tu ya wakaazi wa Mji
- Jumla ya maunganisho ya majitaka ni wateja 5,900 (Septemba, 2019).
- Mitandao imeenea kikamilifu (comprehensive reticulation sewers network) kwenye maeneo matatu tu ya mji (Area C, Area D na Central Business Area).
- Maeneo mengine ya mji yaliyofikiwa na mtandao wa kukusanyia majitaka japo kwa kiasi kidogo (Makole, Viwandani, Madukani, Kizota, Chamwino, Kikuyu Kaskazini, Uhuru na Tambukareli).

**2.2.2 Mabwawa ya kutibu Majitaka**

- Mfumo uliopo wa kutibu majitaka ni mabwawa (Waste Stabilization Ponds - WSPs)
- Kwa sasa mabwawa haya yamezidiwa kutokana na kuhudumia watu wanaozidi usanifu wake.

**3.0 UCHAKATAJI WA ANKARA, USAMBAZAJI NA MALIPO (MAKUSANYO)**

**3.1 Uchakataji wa Ankara na Usambazaji**

- Uchakataji wa Ankara kwa wateja wote wa DUWASA hufanyika kwa kutumia mfumo wa Smart Billing Manager-(SBM).
- Wasomaji mita hukusanya readings kutoka kwa wateja kwa kutumia mobile application ambapo usomaji huingizwa katika System moja kwa moja ambayo hutengeneza Ankara automatically.
- Utengenezaji wa Ankara hufanyika kila tarehe 21 ya kila mwezi.
- Usambazaji wa Ankara hufanyika kwa kutumia ujumbe mfupi SMS billing isipokuwa ankara za Taasisi.




KITUO CHA KUSUKUMIA MAJI KWENYE CHANZO CHA MAJI MZAKWE.

**3.2 Makusanyo ya Maduhuli**

- Makusanyo ya maduhuli hufanyika kwa kutumia njia za kielektroniki kupitia mfumo wa GePG pekee.
- Kupitia mfumo huu, mteja ana uwezo wa kulipia kwa kutumia mitandao yote ya simu, mabenki ya CRDB, NMB, TPB na NBC na wakala wa mabenki hayo.
- Wastani wa makusanyo ya maduhuli kwa mwezi ni Tshs 1.6Bn/=.

**3.0 UCHAKATAJI WA ANKARA, USAMBAZAJI NA MALIPO (MAKUSANYO)**

**Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli**




**4.0 CHANGAMOTO**

Baadhi ya changamoto zinazoikabili DUWASA katika kutekeleza majukumu yake:

i. Ufinyu wa mtandao wa kusambazia majisafi ambapo, zaidi ya kilometa 400 zinahitajika kujengwa ili kuyafikia maeneo mapya yasiyo na mitandao na yale yanayoendelea kuendelezwa. Pia urefu wa mtandao wa majitaka ni kilometa 86 tu ikilinganishwa na takribani kilometa 250 zinazohitajika.
ii. Taasisi za Serikali kutolipia ankara zake za maji kwa wakati. Hadi kufikia Juni, 2019, DUWASA ilikuwa inazidai Taasisi za Serikali zaidi ya Shs. 1.5bn/=.
iii. Upotevu wa maji unaofikia wastani wa 27%. Juhudi mbalimbali zinaendelea ili kuhakikisha kiasi hiki kinaendelea kushuka
iv. Kuchakaa na kubomokea (collapsing) kwa mtandao wa Majitataka maeneo ya Area C na D. Gharama ya kubadili mfumo huu ni takribani Shs 4.5bn/=.
v. Gharama kubwa za umeme wa kuzalisha, kusafirishia na kusambazia maji, wastani wa Shs.500M/- kwa mwezi.
vi. Wizi wa Maji unaofanywa na baadhi ya wateja wasıo waaminifu.

**5.0 MIPANGO YA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA MJINI DODOMA**

**5.1 Mipango ya ya muda mfupi**

- Ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya maji ambalo limekuwa likiongezeka siku hadi siku, DUWASA kwa kushirikiana na Serikali (Wizara ya Maji) imepanga na kuanza kutekeleza mradi wa kutafuta vyanzo vya maji chini ya ardhi katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji.
- Umuhimu wa kutekeleza mpango huu unasukumwa kwa



# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)



*Wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji kwenye mji wa Serikali Mtumba*

kiasi kikubwa na uamuzi wa Serikali ya awamu ya tano (5) kuamua kuhamia Makao Makuu ya Nchi – Dodoma hali inayopelekea ongezeko la uhitaji wa huduma nyingi za kijamii ikiwemo huduma nyeti ya maji.

- Mpango huu unatekelezwa wakati Serikali ikijiandaa kutekeleza mradi mkubwa wa chanzo kingine cha maji ambacho ni bwawa katika mto Bubu Wilayani Chemba. Utekelezaji wa mpango huu umefikia hatua ifuatayo:

(a) Utafutaji wa maji chini ya ardhi na uchimbaji visima katika eneo la Ihumwa/Mtumba (Mashariki mwa mji)
- Kazi ya utafiti wa maji chini ardhi pamoja na uchimbaji wa visima saba (7) vyenye uwezo za kuzalisha zaidi ya meta za ujazo 2,500 kwa siku imekamilika.

(b) Utafutaji wa maji chini ya ardhi na uchimbaji visima katika eneo la Ihumwa/Mtumba (Mashariki mwa mji)
- Kazi ujenzi wa miundombinu (mabomba ya kukusanyia maji toka visimani, mabomba ya kusafirishia maji hadi mji mpya wa Serikali, ununuzi wa pampu za visimani, ujenzi wa vituo vya kusukumia maji na matenki (sump meta za ujazo 200 na storage meta za ujazo 1000) umekamilika.
- Hatua hii ya Mradi huu unaogharimu jumla ya Shilingi 3.6bn/= na imekamilika mwezi Mei, 2019.
- Mradi unahudumia Mji mpya wa Serikali pamoja na maeneo ya Ihumwa.

(c) Utafutaji wa maji chini ya ardhi na uchimbaji visima katika eneo la Kikombo na Nala
- Katika eneo la Kikombo na Ihumwa, kazi ya utafuataji wa maji chini ya ardhi (Geophysical Survey) imekamilika.
- Kazi zinazoendelea ni za kuchimba jumla ya visima 10 kazi ambayo imeshaanza kwa kuchimba visima saba (7).
- DUWASA inaendelea na mpango wa kuchimba visima maeneo ya pembezoni mwa mji katika mwaka wa fedha 2019/2020.

(d) Miradi ya kusambaza maji maeneo yasiyo na huduma Katika Bajeti ya 2019/2020, DUWASA imetenga jumla ya shilingi 2.5Bil/- na imepanga kukopa Shs. 1.5bn/= kupitia IFF – OBA kuwezesha uboreshaji na usambazaji maji katika maeneo mbalimbali mjini.

(e) Ufungaji wa mita za malipo kabla
- Kutumia mita za malipo-kabla (Pre-paid water meters) kwa kuanza na wateja wa Taasisi 752 na hatimaye wateja wa majumbani kwa lengo la kupunguza au kuondoa kabisa madeni sugu.
- Mita hizi pia zimefungwa katika Wizara na Taasisi zote zilizojengwa katika mji wa Serikali Ihumwa.

**5.2 Mipango ya muda wa Kati/Mrefu**

Kazi zifuatazo zinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu ili kuwa na uhakika wa huduma ya majisafi na uondoshaji majitaka Mjini Dodoma na katika mji mpya wa Serikali.

(a) Mradi wa Chanzo cha Maji cha Farkwa –Wilaya ya Chemba
- Mradi una lengo la kupata chanzo cha nyongeza cha maji kwa wakazi wa mjini Dodoma.
- Mradi utawezesha ongezeko zaidi ya 120,000M3 Jijini Dodoma ambazo zinataweza kuhudumia zaidi ya watu 1,000,000.
- Kazi za tathmini ya athari za mazingira na kijamii (ESIA) na usanifu wa zimekamilika.
- Kazi za tathmini ya mali katika eneo litakapojengwa bwawa na miundombinu yake imekamilika.

(b) Mradi wa Chanzo cha Maji kutoka Ziwa Victoria
- Katika mpango wa muda mrefu, Wizara ya maji kwa kushirikiana na DUWASA imepanga kutumia Ziwa victoria kama Chanzo cha Maji cha uhakika kwa Jiji la Dodoma
- Tayari Wizara imeunda timu ya wataalamu wa ndani ambayo itandaa pre-feasibility study.
- Timu imeanza kazi mwezi Agosti, 2019 na itakamilisha mwezi Oktoba, 2019

(c) Mradi wa uboreshaji huduma za majisafi na Majitaka Mjini Dodoma na Chamwino Ikulu
- DUWASA imeajiri Mhandisi Mashauri Norplan Tanzania ltd ambaye anafanya ESIA na Usanifu wa kina.
- Lengo la mradi ni pamoja na kupata mahitaji halisi ya Mji wa Dodoma na Chamwino ya huduma za majisafi na majitaka yanayoendana na ujio wa Serikali Makao Makuu Dodoma kwa miaka 30 ijayo.
- Mhandisi Mshauri atafanya kazi ya kutafuta vyanzo vingine vya maji kwa maeneo ya pembezoni mwa mji.
- Inatarajiwa kuwa, baada ya kazi ya Mhandisi mshauri kukamilisha kazi yake na mradi wa ujenzi kutekelezwa huduma ya maji kwa wakazi wa Dodoma na Chamwino zitawafikia wananchi kwa asilimia zaidi ya 95.
- Gharama za mradi huu ni shilingi 885Mil/- kwa awamu ya kwanza ya Usanifu na shilingi Billioni 1.16 kwa awamu ya pili ya usimamizi wa kazi za ujenzi.

(d) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uondoshaji na kutibu majitaka Mjini
- Kupitia WSDP II , DUWASA ina mpango wa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji na kutibu majitaka
- Mradi unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani zaidi ya milioni 70 na unatarajiwa kuaza kutekelezwa mwaka 2019/2020
- DUWASA imeshapata eneo la ujenzi wa mabwawa mapya ya kutibu majitaka katika eneo la Nzuguni ambapo fidia ya Sh. Milioni 611 zimetumika kilipia fidia eneo la hekta 60.
- Aidha, mitandao ya kukusanyia majitaka itajengwa kwenye maeneo ya Area A, Chadulu, Chinangali, Kikuyu na Makole. Maeneo mengine yatakayohusika ni Ipagala, Urban Renewal east and West, Viwanda, Mlimani, Medeli, Ilazo, Kisasa, NCC na Nkuhungu. Pia, utafanyika ukarabati wa mtandao wa majitaka kwenye maeneo ya Area C na Area D.

**Imeandaliwa na:**
**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji**
**DUWASA**
**S.L.P 431**
**Barua pepe: md@duwasa.go.tz, Tovuti: www.duwasa.go.tz,**
**Simu: +255 26 2324245, Faksi: +255 26 2320060**
**Simu ya Bure: 0800110078**
**DODOMA**
**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA**
**(DUWASA)**



# SALAMU ZA PONGEZI

*Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) inaungana na Watanzania wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutimiza miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano.*


**DUWASA inatoa pia pongezi kwa maendeleo makubwa ambayo yamepatikana kwa Watanzania katika uongozi chini ya Mhe. Rais. Aidha DUWASA inamtakia Mhe. Rais na viongozi wote wa Serikali Afya Njema ili waendelee kuwaongoza vyema Watanzania kufikia Uchumi wa Kati.**

**Mamlaka ya DUWASA inawahakikishia Wananchi kuendelea kutoa huduma ya uhakika ya majisafi na uondoshaji wa majitaka Makao Makuu y Nchi Dodoma katika mazingira endelevu.**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**DUWASA**
**S.L.P 431**

**Barua pepe: md@duwasa.go.tz, Tovuti: www.duwasa.go.tz,**
**Simu: +255 26 2324245, Faksi: +255 26 2320060**
**Simu ya Bure: 0800110078**
**DODOMA**

# Miradi mikubwa yachochea ajira




IMEELEZWA kuwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati umekuwa chachu kubwa katika kuongeza wigo mpana wa upatikanaji ajira kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana Anthony Mavunde, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Anna Gidarya.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kwa muda mrefu serikali imekaa kimya kuhusu ajira kwa vijana, kumekuwa na wimbi kubwa la vijana mitaani wasio na ajira waliomaliza vyuo mbalimbali takriban miaka mitatu iliyopita.

"Je, ni lini serikali itafungua milango ya ajira kwa vijana wa Kitanzania walioteseka kwa muda mrefu? Je, serikali imefanya tathmini ya kiwango cha madhara yaliyotokana na vijana kukosa ajira?" Alihoji.

Pia alihoji ni vijana wangapi wameathirika na kujiingiza katika makundi mabaya kwa kukata tamaa ya kupata ajira.

Mavunde alisema kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19 jumla ya ajira serikalini ikijumuisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma zilikuwa 184,141.

"Aidha, ajira katika miradi ya maendeleo ya serikali zilikuwa 787,405, na ajira zilizozalishwa na Sekta Binafsi zilikuwa 646,466,"alisema.

Hata hivyo, alisema ukosefu wa ajira kwa vijana una madhara kiuchumi na kijamii, unapunguza mchango wa nguvukazi isiyo na ajira katika Pato la Taifa pamoja na jitihada za serikali kupunguza umaskini.

Aidha, alisema kunapunguza uwezo wa nguvukazi hiyo kuweza kujitegemea na kuendelea kuwa tegemezi kwa jamii.

"Ili kupunguza tatizo hilo serikali imeandaa mikakati mbalimbali za kuwezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri," alisema.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni utekelezaji wa programu ya kukuza ujuzi nchini ambayo katika kipindi cha mwaka 2017-2019, jumla ya vijana 47,585 wamewezeshwa kiujuzi na kujiajiri katika sekta mbalimbali.

Kuhusu suala la vijana kujiingiza katika makundi mabaya, Mavunde alisema ni suala la maadili na makuzi.

"Pia serikali kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana imekuwa ikiandaa miongozo ya maadili na makuzi kwa vijana na imekuwa ikiendesha mafunzo hayo kwa vijana nchini," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikabidhiwa 'tablets' na Spika wa Bunge, Job Ndugai, wakati wa ugawaji kwa wabunge wote katika ukumbi wa Msekwa, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Uvuvi wa mabomu wapungua

WIZARA wa Mifugo na Uvuvi, imesema kutokana na udhibiti wa uvuvi haramu unaotumia mabomu, umepungua na kwa mwaka huu hakuna matukio ya milipuko yaliyoripotiwa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema nayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Jang'ombe (CCM), Ali King, aliyetaka kujua ni kwa nini uvuvi wa kuzamia kwa kutumia chupa umezuiliwa.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema katika miaka kuanzia 2017 kurudi nyuma kulikuwa na matukio mengi ya milipuko lakini yamepungua na hadi sasa hakuna milipuko.

Alisema kutokana na madhara ya matumizi ya milipuko katika uvuvi, matumizi ya chupa (mitungi ya gesi) katika shughuli za uvuvi yamekatazwa kisheria kwa mujibu wa Kanuni ya Uvuvi ya 66(2) ili kunusuru rasilimali za uvuvi na mazingira ya bahari kwa ujumla.

"Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kutokana na juhudi kubwa ambazo zimefanywa na Serikali kupitia Wizara za kudhibiti matumizi ya milipuko na mitungi ya gesi (gas cylinder) katika uvuvi, uvuvi huu haramu umepungua kwa asilimia 99 katika maeneo ya Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi," alisema.

Aidha, alifafanua shughuli za uvuvi nchini zinasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na miongozo mbalimbali ambayo hutolewa kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha kuna matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Alieleza pia kwa mujibu wa Kanuni ya Uvuvi ya Mwaka 2009 Kifungu cha 66(1-Q) vifaa vya kupumulia chini ya maji au scuba au mitungi ya gesi au chupa haviruhusiwi kutumika kwa ajili ya kuvua samaki au viumbe wengine wa baharini.

"Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 66(2) vifaa vya kupumulia chini ya maji au scuba au mitungi ya gesi au chupa vinaweza kutumika tu kwa ajili ya uvuvi wa burudani (sport fishing), uvuvi wa samaki wa mapambo, mafunzo na utafiti na kwa kibali maalum," alisema.

# Uthamini maeneo Tarime Acacia kulipa fidia waiva

SERIKALI imesema Mthamini Mkuu wa Serikali ameshakamilisha uthaminishaji wa maeneo 1,838 yanayopaswa kulipwa fidia na mgodi wa Acacia na tayari umeshawasilishwa kwenye menejimenti ya mgodi kwa hatua za ulipaji.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Agness Marwa.

Katika swali lake, alieleza kuwa wananchi wengi walibomolewa nyumba zao na Mgodi wa Acacia uliopo Nyamongo wilayani Tarime na wengine hawajalipwa fidia ya maeneo yao mpaka sasa.

"Aidha, mgodi pia umeanza kuchimba chini maeneo ya watu (Underground mining). Je, ni lini mgodi wa Acacia uliopo Nyamongo utalipa fidia kwa wananchi hawa?" Alihoji.

Waziri Biteko alisema uthaminishaji katika maeneo yanayozunguka mgodi wa North Mara na ulipaji wa fidia umegawanyika katika awamu nyingi kwa kuzingatia vijiji husika kuridhia.

"Kijiji cha Nyabirama chenye wakazi 1,974 waliothaminiwa katika awamu ya 20, 35 na 42 wote walilipwa fedha zao isipokuwa wakazi 64 ambao fidia yao iliyoidhinishwa ya Sh. bilioni 1.9 waliikataa na hundi zao zilibaki Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Tarime," alisema.

Aidha, alisema eneo la Kijiji cha Nyabichune lilithaminiwa katika awamu ya 47 na kuidhinishwa Sh. milioni 224 kwa ajili ya watu 69.


Hata hivyo, alisema wizara iliagiza uthamini wa maeneo ya kijiji cha Nyabichune urudiwe kwa sababu wananchi walipunjwa.

Alifafanua kuwa serikali imeendelea kusimamia sekta ya madini kwa kuhakikisha uwekezaji unafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Alisema serikali inahakikisha wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo miradi ya uendelezaji migodi inataka kufanyika na kulazimika kupisha maeneo yao, wanalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na wanapewa makazi mbadala ambayo yana hali bora kuliko makazi waliyokuwa nayo awali.

Akizungumzia kuhusu suala la mgodi kubadilisha aina ya uchimbaji toka uchimbaji wa wazi kwenda uchimbaji wa chini, Biteko alisema uamuzi huo ulifikiwa baada ya mgodi kufanya utafiti ulioonyesha kuwa gharama ya uchimbaji wa chini ilikuwa ni ndogo ukilinganisha na gharama za kuendelea na mgodi wa wazi.


"Niwatoe shaka wana Tarime na kuwa wizara inafuatilia kwa karibu uchimbaji unaofanyika na mpaka sasa uchimbaji wa underground unafanyika eneo la Gokona kuelekea Nyabigena ndani ya maeneo waliyokuwa wakichimba tangu awali," alisema.



Ukurasa 17

**UN yaongeza muda kwa Ujumbe wa Amani Darfur**

Afrika inaposaka mwelekeo, mifungamano uga kimataifa



Ukurasa 18



Ukurasa 20

**Figisu hizi somo la Jafo halikueleweka?**


# siasa

JUMATANO NOVEMBA 6, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 19

**Wananchi wanavyosubiri nguvu ya hoja kutoka kwa wagombea**

# Miaka minne ya JPM na mafanikio yake

Distributed via ippmedia

**Na Mashaka Mgeta**

UTAWALA wa awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli, umetimiza miaka minne tangu kuingia kwake madarakani na kuapishwa rasmi Novemba 5, mwaka 2015.

Kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake, Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete, Rais Magufuli pia ametokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ni chama kilichoundwa Februari 5, mwaka 1977, kikitokana na Afro Shiraz Party (ASP) na Tanganyika African National Union (TANU).

Ni kwa mpangilio huo wa kidemokrasia katika kuiongoza Tanzania, viongozi hao (ukimuondoa Mwalimu Nyerere aliyefariki dunia Oktoba 14, 1999), wamehudumu kwa vipindi viwili vya jumla ya miaka 10 kwa awamu ya uongozi wao.

Kupitia vipindi hivyo, serikali zilizopita zilifanikiwa kusimamia misingi ya umoja na utaifa, ingawa kwa viwango na namna tofauti, lakini mwishowe, waliondoka madara-

INAENDELEA UK.16



Rais John Magufuli. **PICHA: MTANDAO**

**Afrika inaposaka mwelekeo, mifungamano uga wa kimataifa**

Ukurasa 18

# Miaka minne ya JPM na mafanikio yake



Mradi wa Umeme wa Rufiji (MW 2115), miradi iliyoanza kipindi cha Rais Magufuli.



Reli ya kisasa (SGR) moja ya miradi mikubwa inayoendelea kugharimiwa na serikali ya Rais Magufuli katika miaka yake minne.

**INATOKA UK.13**

kani wakiwa na 'alama' za kukumbukwa.

Ndivyo inavyojitokeza, japo kwa namna tofauti katika utendaji kazi wa serikali ya Rais Magufuli, kufikia wakati huu ambapo Taifa linaadhimisha miaka minne ya kuwapo kwake madarakani.

### UWAJIBIKAJI OFISI ZA UMMA

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Fikiri Hussein anasema miongoni mwa maeneo yanayoibua tofauti ya mazoea katika utendaji kazi kwa watumishi wa umma katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais Magufuli, ni uwajibikaji murua kwenye ofisi za umma.

Hussein anasema ingawa kila utawala ulitumia mbinu, sheria, kanuni na taratibu kuhakikisha misingi ya utawala wenye kukidhi mahitaji ya umma, lakini sasa kunaonekana ishara za wazi katika ukuaji wa nidhamu kwa watumishi wa umma.

"Miaka ya kabla ya awamu ya tano, kuna mambo yalikuwa ya kawaida kuyashuhudia kwa watumishi wa umma...jambo kama hulka ya mtumishi kumuacha mwananchi wa kawaida akihitaji huduma, ama kuomba hongo waziwazi ili kutoa haki ilikuwa kawaida sana," anasema Hussein.

Hata hivyo, Hussein anasema ingawa kuna sababu nyingi zinazochochea hali hiyo kuwa tofauti sana na utawala uliopita, lakini ukali wa Rais Magufuli na kauli zisizotiliwa shaka katika kuhimiza uwajibikaji kwa umma, ni miongoni mwa sababu za kutufikisha katika hatua hiyo," anasema.

Justina Macha, mtaalamu wa sayansi ya siasa anaunga mkono hoja hiyo kwa kusema, vipo viashiria kadhaa vinavyothibitisha namna uwajibikaji katika ofisi za umma ulivyoboreka katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais Magufuli.

> Nchini Tanzania inakadiriwa kuwa idadi ya viwanda vilivyopo inafikia 53, 876. Kati ya hivyo vikubwa ni 251, vya kati ni 173, vidogo vinafikia 6,957 na 46, 495 ni vidogo kabisa.

Justina anatoa mfano wa ukuaji wa mapato (kwa mujibu wa takwimu zinazotangazwa na serikali) na namna zinavyoelekezwa katika huduma za jamii kuwa ni sehemu ya uthibitisho wa hoja hiyo.

Anasema sehemu ya utekelezaji huo ni kutengwa kwa asilimia 10 ya mapato ya halmashauri kwenda kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, sura 290 kifungu cha 37 (a).

Ingawa hakutoa takwimu, lakini Justina anasema utekelezaji wa azma hiyo unakidhi mahitaji ya kutoa mikopo isiyo na riba, ili kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kujiimarisha kwa shughuli za ujasiriamali.

### ONGEZEKO LA MAPATO

Kiongozi wa vijana katika moja ya vyama vya siasa nchini, Julius Fidelis, anasema umakini wa Rais Magufuli katika kudhibiti matumizi mabaya ya mali za umma, hasa kupitia vitendo vinavyohusiana na ufisadi umefanikisha ongezeko la mapato yanayoipa nguvu serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Fidelis anasema takwimu zinaonyesha kuwa umakini huo umesababisha wastani wa mapato yanayokusanywa na serikali kuwa kati ya Sh, bilioni 850 hadi trilioni 1.3 kwa mwezi, huku takwimu zilizotangazwa kwa ajili ya Septemba mwaka huu zikionyesha kiasi hicho kupanda hadi kufikia takribani Sh. trilioni 1.8

Hali kama hiyo inaelezwa kuwapo kwenye ngazi ya halmashauri



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia), akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (kushoto) wakikagua mojawapo ya majengo ya Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Simiyu ambayo inajengwa katika kipindi hiki cha miaka minne ya Rais Magufuli. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

za majiji, wilaya na miji, ambapo 195 miongoni mwa halmashauri zilizopo nchini zilifikia kiwango cha asilimia 90 ya ukusanyaji mapato kwa mwaka 2018/2019.

Ukusanyaji mapato huo unaelezwa pia kupitia takwimu za vyanzo tofauti zinazoonyesha kuwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa serikali 2017/2018 mapato yaliyokusanywa yalikuwa ni asilimia 81, hivyo kufanya ongezeko halisi kuwa ni asilimia tisa.

### VIWANDA

Moja ya ajenda za serikali ya awamu ya tano ni kuugeuza uchumi wa Tanzania kutoka unaotegemea kilimo na kuwa wa viwanda. Azma hiyo inaonekana kutekelezwa ipasavyo wakati utawala wa Rais Magufuli ukifikisha miaka minne.

Takwimu zinaonyesha kuwa ukuaji wa sekta ya viwanda kwa mwaka mwaka 2015 ilikuwa ni asilimia 6.5, ambavyo pia vilichangia pato la taifa (GDP) kwa asilimia 5.2. lakini mwaka 2018, ukuaji huo ulifikia asilimia 8.3 na mchango wake kwa pato la taifa ukawa ni asilimia 8.

Mabadiliko hayo yenye mafanikio katika sekta ya viwanda, yalichochewa na hatua kadhaa zikiwamo kufufua viwanda vya zamani na kuweka mazingira yanayochochea uanzishwaji wa viwanda vipya, hasa kupitia agizo la Rais Magufuli kwa kila mkoa kuwa na angalau viwanda 100.

Halmashauri ya Mji Kibaha mkoani Pwani inaonekana kuwa 'kinara' katika 'kukaribisha' viwanda kutokana na vile vikubwa na vya kati kufikia 42 huku vidogo vikikadiriwa kuwa zaidi ya 200.

Nchini Tanzania inakadiriwa kuwa idadi ya viwanda vilivyopo inafikia 53, 876. Kati ya hivyo vikubwa ni 251, vya kati ni 173, vidogo vinafikia 6,957 na 46, 495 ni vidogo kabisa.

### AFYA

Huduma za afya ni miongoni mwa maeneo yanayoyajwa kuboreka kwa kasi katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais Magufuli.

Uboreshaji huduma za afya unaelezwa kufikia katika utoaji fedha zikiwamo Shilingi milioni 500 zilizotengwa kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya afya. Takwimu zinaonyesha kuwa vituo vya afya 352 vipo katika hatua mbalimbali za kukamilika ili kuifanya idadi yake kufikia 7,284.

Kwa mujibu wa Mpango wa Kuboresha Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya ya Msingi katika mamlaka ya serikali za mtaa, uliochapishwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) mwaka huu, vituo 304 vitatoa huduma za dharura na upasuaji. Vituo 119 vimekamilika na 58 kati ya hivyo vimewekwa katika orodha ya kuwa tayari kutumika.

Ni kupitia mpango huo, halmashauri kadhaa zilipata mafungu ikiwamo ya Mji wa Kibaha uliyopata Sh.bilioni 2, Sh. milioni 500 kati ya hizo zikaelekezwa katika upanuzi wa kituo cha afya mkoani na Sh. bilioni 1.5 zikawekwa kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo ni miongoni mwa hospitali mpya 67 zilizogharimu Sh. bilioni 100.5 na zitakazofikisha idadi ya kuwa 144 nchi nzima.

### ELIMU

Uboreshaji wa elimu hasa ya msingi na sekondari, pamoja na changamoto zinazojitokeza ni miongoni mwa mafanikio yanayoorodheshwa katika utendaji kazi wa miaka minne ya Rais Magufuli.

Miongoni mwa changamoto zinazotajwa katika utekelezaji wa 'elimu bila malipo' ni wingi wa wanafunzi wakiwamo wa shule za msingi katika halmashauri ya Mji Kibaha, ambapo kwa mwaka huu pekee, idadi yao ilifikia 5,172, wavulana wakiwa ni 2,625 na wasichana 2,547.

> Miaka ya kabla ya awamu ya tano, kuna mambo yalikuwa ya kawaida kuyashuhudia kwa watumishi wa umma...

Takwimu za kipindi cha mwaka 2015 ikiwa ni kabla ya kuingia madarakani kwa Rais Magufuli, idadi ya wanafunzi mjini humo ilikuwa ni 2,944 ambapo 1,390 walikuwa wavulana na wasichana 1,554.

Ni kwa hali hiyo, pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi kwa nyakati tofauti, bado serikali ya awamu ya tano imeendelea kutekeleza wajibu wake wenye kuibua matokeo chanya miongoni mwa yaliyoorodheshwa katika utendaji kazi wake.

***Mwandishi wa Makala haya anapatikana kupitia simu namba +255754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.***

# UN yaongeza muda kwa Ujumbe wa Amani Darfur



Vikosi vya UNAMID vikiwa kwenye shughuli zake za kawaida huko Darfur. **PICHA: MTANDAO**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), limepiga kura ya kuviongezea muda wa mwaka mmoja zaidi, vikosi vya pamoja vya usalama vya Umoja huo na ule wa Afrika (AU) katika jimbo la Magharibi mwa Sudan la Darfur.

Juhudi kubwa zinaendelea kufanywa na Umoja wa Mataifa (UN) ili kuhakikisha amani endelevu na hali ya utulivu inapatikana katika jimbo hilo.

Azimio lililodhaminiwa na Uingereza pamoja na Ujerumani limemtaka Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, kuwasilisha ripoti na mapendekezo kwa baraza hilo Januari 31 mwakani, kutathmini hali ilivyo Darfur.

Naibu Balozi wa Uingereza, UN, Jonathan Allen, anasema ujumbe huo wa UN na AU ujulikanao kwa kifupi kama UNAMID, unalo jukumu muhimu la kuweka mazingira mazuri ya amani na maridhiano hasa wakati huu wa mchakato wa amani.

Mwanadiplomasia huyo ameongeza kwamba kwa kuviongezea muda vikosi vya UNAMID, UN imetambua umuhimu wake katika kudumisha hali ya utulivu kwenye jimbo hilo.

Mwishoni mwa Juni mwaka huu, UNSC lilikubaliana pia kutoondoa ujumbe wa UNAMID hadi Oktoba 31.

Baada ya hapo UN na AU, walipendekeza kuuongezea muda ujumbe huo hadi Oktoba 31 mwaka 2020, uamuzi ambao umeidhinishwa.

Julai mwaka jana, baraza hilo la usalama lilipiga kura pia na kuamua kupunguza kwa idadi, maofisa wa ujumbe wa UNAMID, kufuatia hali ya utulivu kuanza kurudi na mizozo kupungua.

Lengo lilikuwa ni kuviondoa kabisa vikosi hivyo ifikapo Juni 30 mwaka 2020.

Mzozo wa Darfur ulianza mwaka 2003 baada ya raia weusi nchini humo kuanzisha uasi dhidi ya serikali baada ya kudai kuwa serikali ya Sudan ilikuwa inaongozwa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi na ukabila.

Vilevile Serikali ya Khartoum ilidaiwa kuwapa silaha wanamgambo wa Kiarabu kuwashambulia raia weusi, madai ambayo iliyakanusha.

Mzozo wa Darfur uliendelea kwa muda wa miongo mitatu chini ya utawala wa aliyekuwa Rais Omar al-Bashir wakati ambao Sudan ilishuhudia umwagikaji wa damu si tu katika jimbo la Darfur bali hata katika maeneo ya Blue Nile na Kordofan Kusini.

Utawala wa Al-Bashir uliangushwa mwezi Aprili mwaka huu baada ya maandamano makubwa kushuhudiwa nchini humo kushinikiza mabadiliko katika uongozi.

Baada ya hapo, makubaliano ya kugawana madaraka yalitiwa saini mwezi Agosti kati ya jeshi na waandamanaji.

Waandamanaji waliitaka serikali kufikia makubaliano ya amani na makundi yenye silaha katika muda wa miezi sita. **DW**

# Afrika inaposaka mwelekeo, mifungamano uga wa kimataifa

## • Ni kukidhi upungufu wa uthabiti duni wa kisiasa nyumbani



Baadhi ya viongozi wa Afrika wakiwa na Rais wa Russia, Vladimir Putin (aliyenyosha mkono) kwenye mkutano wao wa hivi karibuni uliofanyika Russia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

KUFANYIKA kwa mkutano mkubwa kati ya wakuu wa nchi za Afrika na Russia hivi karibuni kumeongeza changamoto ya kupata mwelekeo wa ushirikiano kimataifa na mwelekeo kitaifa katika nchi nyingi za Afrika.

Yako maeneo uasi unaendelea kuwaka moto, migawanyiko ni mikubwa na uthabiti wa uchumi ni hafifu. Mikutano ya ushirikiano kimataifa inasaidia kutoa mwanga wa nini kinaweza kufaulu katika Afrika, na pia kujenga heshima kwa tawala zilizopo kuwa zinatambuliwa na kuhitajiwa na viongozi wa mataifa makubwa. Ni kielelezo cha umakini.

Mkutano kati ya Russia na Afrika ulifanyika Oktoba 23 hadi 24 kando ya ufukwe wa Sochi, jiji la kitalii eneo la Black Sea; karibu na Georgia ambayo zamani ilikuwa sehemu ya Urusi ya kijamaa.

Mkutano huo ambao ni wa kwanza kati ya nchi za Afrika na Russia ulifanyika chini ya kaulimbiu ya 'amani, usalama na maendeleo,' ambao kimsingi ni sehemu ya juhudi za kimataifa kutafuta suluhu ya vita maridhawa maeneo tofauti, na kutumia amani kuongeza kasi ya kupata maendeleo.

Russia ndiyo inaanza kuingia katika kutafuta uhusiano wa karibu na nchi za Afrika.

Pamoja na kuwa katika ufunguzi wake Rais Vladimiri Putin alizungumzia ukandamizwaji wa Afrika na mataifa ya kibeberu, alikuwa anajua anacheza zeze na kuimba wimbo unaofahamika sana barani Afrika.

> Juhudi za nchi za Afrika kujenga mahusiano ya kimataifa yenye uwezo wa kupunguza shinikizo la demokrasia na maendeleo (kwa njia ya soko, zaidi) ndiyo rahisi kusema kuwa yanafanikiwa.

Ila ukiangalia kwa karibu unakuta kipindi hicho kilishapita na sasa kila mahali vijana katika nchi za Afrika wanataka demokrasia, kutokana na kuchoshwa na mazingira duni ya maisha bila ajira, huku tabaka tawala linaendesha VX na wasaidizi au jamaa zao ndiyo wanaendesha 'viboksi.'

Inafika mahali bei ya mkate inapanda au nauli, na hapo nchi inalipuka. Yako maeneo ambako Russia na Afrika zingekuwa na mengi ya kuongea kwa mfano suala la vikwazo vya Marekani kwa Zimbabwe, ambako nchi hiyo ilitisha maandamano na siku huria kwa wafanyakazi kupinga vikwazo hivyo.

Lakini inaelekea suala hilo halikupewa kipaumbele katika mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika na Rais Putin, lakini vyombo vya habari viliendelea kukumbushia mzaha kuhusu vikwazo kati ya hayati Rais Robert Mugabe na Rais Putin mwaka 2015, na Rais Emmerson Mnangagwa alileta suala hilo mezani katika mkutano wa Sochi majuzi.

Katika mikutano ya Afrika na mataifa kama Russia, China na hata Japan, kigezo cha lazima ni ushirikiano kwa msingi wa sera na mwelekeo wa utawala ambao Afrika au nchi binafsi ina haki ya kuchagua.

Mikutano na nchi za Magharibi ni tofauti kwani suala la demokrasia halibishiwi katika mikutano kama hiyo, kuwa ndiyo msingi wa ushirikiano wa kimataifa, kwa mfano wiki hii kuna mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje wa nchi za Ulaya Kaskazini (Nordic) na Afrika.

Pia kuna mikutano ya |Francophonie au 'Francafrique' ambako pia demokrasia ni kigezo halisi.

Juhudi za nchi za Afrika kujenga mahusiano ya kimataifa yenye uwezo wa kupunguza shinikizo la demokrasia na maendeleo (kwa njia ya soko, zaidi) ndiyo rahisi kusema kuwa yanafanikiwa.

Nje ya nchi za Magharibi, mikutano mingine kati ya Afrika na mataifa makubwa inakubali msingi huu wa kila nchi kuchagua uelekeo inayotaka, lakini mataifa hayo pamoja na marafiki zao walio madarakani nchi nyingi za Afrika hawajapata upenyo wowote katika hisia za wananchi wengi barani.

Juhudi za Rais Mnangagwa kulaani ukandamizaji zikawa debe tupu; wengi hawakutokea.

Kuna upande mwingine wa majadiliano kati ya Afrika na Russia ambao ulielekea mkondo wa ki-Magharibi, ule wa kaulimbiu ya 'Wanawake katika mahusiano ya Russia na Afrika: Uwiano wa jinsia katika siasa, uchumi na jamii.'

Mkutano wa Sochi pia ulijadili teknolojia za kupata maji safi kwa urahisi, na hata kufanyia ukarabati reli za zamani na kuongezea nyingine, licha ya kuwa miradi hiyo labda si mikubwa kama hii inayoendelea, au Russia kushindana na China katika suala la miundombinu Afrika.

Russia kimsingi inahitaji eneo la biashara, si kujitutumua.

Kwa upande mwingine, mkutano wa kiuchumi wa China na Africa (FOCAC) uliofanyika Beijing mwezi Septemba katika kumbi za Bunge la China (Great Hall of the People) ulikuwa na mandhari ya watu wanaofahamiana.

Uenyekiti wa mkutano wa Sochi ulikuwa moja kwa moja wa Russia lakini ule wa Beijing, kama jukwaa la kuangalia mahusiano ya kiuchumi kati ya China na Afrika, ulikuwa na wenyeviti wawili, Rais Xi Jinping na Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini kutokana na uwepo wa mikutano hiyo kuwa jambo la kawaida.

Russia inakuja nyuma kama zilivyo nchi za Ulaya Kaskazini, wakati China inafanana na Ufaransa, ipo siku hizi zote.

Kulikuwa pia na tofauti za wazi za kina cha majadiliano na maeneo yaliyokubaliwa kati ya nchi zilizoshiriki kuendelea kuzifanyia kazi au kukamilisha kazi zinazoendelea, kwani China ina maeneo mengi inafanya kazi na nchi za Afrika, tofauti na Russia.

Hapa nchini kwa mfano kuna kampuni ya Russia inatafuta madini ya uranium na mengineyo yanayotumika katika eneo la nguvu za atomiki, na siyo rahisi kukuta taasisi za kiuchumi au kitamaduni zinazofanya kazi hapa, kwani zilikwama wakati Urusi ya kijamaa ilipoanguka.

China ambayo haijawahi kuona mtikisiko mkubwa kama wa Urusi imejenga uhusiano zaidi ilipobadili sera kuingia utandawazi

Baadhi ya nchi za Afrika ikiwemo Tanzania zilijitahidi kuunda umoja wa kupinga vikwazo vya uchumi vya Marekani dhidi ya Zimbabwe, ila tofauti ni kuwa hatua hiyo haikutangazwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki.

Ni kampeni ya ki-NGO ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambako Philip Mangula, veterani wa vita vya ukombozi na kuundwa kwa makambi ya kufunza wapiganaji nchi tofauti Kusini mwa Afrika na makamu mwenyekiti Bara alitangaza.

La kushangaza kuhusu kampeni hiyo ni kuwa kumeundwa siku maalum katika mwaka ya kupinga vikwazo dhidi ya Zimbabwe, kana kwamba hakuna uwezekano maendeleo kiasi tu ya demokrasia yapatikane nchini Zimbabwe na vikwazo hivyo viondolewe, ambayo ina maana kuwa Zimbabwe ni nchi ya kimapinduzi kama Cuba, isiweze kuleta mageuzi viondolewe.

Kana kwamba inatoa majibu kwa harakati za makamu mwenyekiti Mangula na rafiki yake Mnangagwa katika mfungamano wa 'Frontline States' Marekani iliongeza vikwazo dhidi ya Waziri wa Usalama wa Taifa wa Zimbabwe, Owen Ncube.

Kikwazo chenyewe ni kuwa hawezi kuingia nchini Marekani, kuingiza au kutoa fedha au mali zozote nchini humo, akituhumiwa kuhusika na uvunjaji wa haki za binadamu.

Umoja wa Ulaya (EU) na Marekani wanasema vikwazo dhidi ya Zimbabwe vinagusa watu kadhaa; havina athari yoyote kwa uchumi wa jumla wa nchi hiyo.()

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2019;

# Wananchi wanavyosubiri nguvu ya hoja kutoka kwa wagombea

**Na Reubeni Lumbagala**

KWA mujibu wa Mwongozo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa viongozi wa ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa unaofanyika Novemba 24, 2019, zoezi la kuchukua na kurejesha fomu za kugombea nafasi mbalimbali katika serikali za mitaa lilianza Oktoba 29 na kukamilika juzi Novemba 4, 2019.

Katika kipindi hicho cha siku saba, wagombea wa vyama vyote vya siasa vilivyothibitisha kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa, walikuwa na haki ya kwenda kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kugombea.

Baada ya kuchukua fomu hizo, wagombea walikuwa na muda wa kutosha wa kujaza fomu hizo kwa usahihi na kuzirejesha, ili kupata ridhaa ya kugombea katika nafasi wanazotaka kugombea.

Makala ina imani kwamba wagombea walizingatia muda na siku za kuchukua na kurejesha fomu zilizokuwa zimetolewa, na kwamba Novemba 5 ambayo ilikuwa ni siku ya jana Jumanne, uteuzi wa wagombea ulifanyika kwa kuwa ilikuwa siku ya uteuzi wa wagombea.

Wagombea ambao wamepitishwa, watakuwa na kazi ya kwenda kujinadi na kuuza sera zao kwa wananchi ambao ndiyo wapigakura.

Kuanzia Novemba 17, 2019 ni muda wa kuanza kwa kampeni, kipindi ambacho shughuli zake hizo za kujinadi kwa wagombea zitafungwa rasmi na Novemba 24, itakuwa ni Siku ya Uchaguzi.

Wananchi waliojiandikisha katika daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, watashiriki kuchagua viongozi bora kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo ya maeneo wanayoishi. Wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wanapaswa kufahamu kuwa wapigakura wapo tayari kusikiliza sera zao na si vijembe kutoka kwao.

Wananchi wana uelewa wa kutosha kuhusiana na aina ya viongozi wanaowataka kwa ajili ya kushirikiana nao katika harakati za kujiletea maendeleo.

Kutokana na uwepo wa demokrasia ya vyama vingi hapa nchini, wagombea mbalimbali wa vyama vya siasa watakuwa katika majukwaa ya kujinadi ili wapigakura waweze kuwapa ridhaa ya kuongoza kwa miaka mitano ijayo, yaani mwaka 2019-2024.

Ni muhimu wagombea wakazingatia kuwa wananchi wanataka kusikia nguvu ya hoja wakati wa kujinadi kwao na si maneno ya vijembe na ya kuvunjiana heshima ambayo hayana tija katika maisha ya wapigakura wao.

Wananchi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika maeneo yao wanayoishi kama vile ukosefu wa zahanati, shule, ukosefu wa maji, umeme, masoko nk.

Wanategemea basi kupitia viongozi watakaopatikana, wasaidiwe kupunguza kama si kumaliza kabisa changamoto na kero hizo.

Wagombea wanalo jukumu la kujibu changamoto zinazowakabili wananchi wao kwa kueleza mikakati ya muda mfupi na ya muda mrefu ya namna watakavyotatua changamoto za wananchi wao.

Kwahiyo, mgombea ambaye atashindwa kujikita kueleza namna atakavyotatua changamoto za wananchi wake na kuishia kupiga vijembe dhidi ya wagombea wenzake, atakuwa katika hatari ya kushindwa katika uchaguzi huu.

Wagombea wasijikite kutafuta udhaifu binafsi dhidi ya wagombea wenzao, badala yake wajikite kuzungumzia mikakati yao binafsi ya namna watakavyowatumikia wananchi kuendeleza kasi ya maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa mustakabali mwema wa maisha yao.

Aidha, wananchi wanahitaji viongozi-watumishi; ambao kwao uongozi ni utumishi na si kichaka cha kufanya biashara, kuendeleza vitendo vya rushwa na kunyanyasa wengine kwa kuwanyima haki zao.

Wananchi wanahitaji viongozi ambao kwao ajenda kubwa itakuwa ni kuleta ustawi bora wa maisha ya wananchi wao kwa kutanguliza mbele maslahi yao wananchi. Viongozi ambao watakuwa sauti ya wasio na sauti, viongozi ambao watawatanguliza wananchi wao kwanza kabla ya maslahi yao binafsi na ya vyama vyao.

Viongozi wa serikali za mitaa walioko katika vijiji, vitongoji na mitaa ndio watu wa kwanza ambao wananchi wanawafikia kwa urahisi katika kufikisha hoja zao kwao.

Hivyo, upo umuhimu kwa wananchi kuhakikisha kuwa wanachagua viongozi bora ambao watakuwa chachu ya mabadiliko chanya na mageuzi ya kimaendeleo.

Wananchi wakatae kununuliwa kwa kupewa rushwa ili kuchagua viongozi.

Viongozi wanaopatikana kwa rushwa kamwe hawatakuwa na kipaumbele cha kuwatumika wananchi wao, badala yake watajikita kuangalia namna watakavyorudisha fedha zao.

Fedha walizozitumia kuhonga wapiga kura kipindi cha kujinadi kwao. Wananchi wapo tayari kusikiliza wagombea ambao watakuwa na nguvu ya hoja katika kusimamia ajenda ambazo ni kipaumbele cha wananchi.

Wagombea wa aina hiyo, ndio watakaopata ridhaa ya kuwaongoza wananchi. Nguvu ya hoja itamalaki katika majukwaa ya siasa kwani ni kitu pekee wananchi wanachotaka kusikia.

Nawakatia kila la kheri wagombea wa vyama vyote, wafanye kampeni za kistaarabu, kampeni zenye ukomavu wa kisiasa ili hatimaye wapatikane viongozi bora, waaminifu na wenye weledi katika kuwatumikia wananchi wao. Tafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyo wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764666349.***


Distributed via ippmedia

Mgombea jukwaani akinadi sera zake.**PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Wananchi wana uelewa wa kutosha kuhusiana na aina ya viongozi wanaowataka kwa ajili ya kushirikiana nao katika harakati za kujiletea maendeleo.



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson (kushoto) akiwa katika moja ya mikutano ya kuhamasisha ustawi wa wanawake.

# Figisu hizi somo la Jafo halikueleweka?

## • Ni vyema zisiingilie mchakato unaofuata



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

MCHAKATO wa kuchukua na kurejesha fomu kuwania uenyeviti wa serikali za mitaa, vitongoji, vijiji na mitaa ulimalizika juzi, huku kukiwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya vyama vya upinzani kwamba vimefanyiwa figisu.

Uchukuaji wa fomu hizo ulianza Oktoba 29 mwaka huu na kuendelea kwa muda wa siku saba zilizomalizika juzi Novemba 4, lakini ukiwa umeacha 'makovu' kwa baadhi ya vyama vya siasa.

Miongoni mwa figisu ambazo vyama hivyo vinadai kufanyiwa ni kufungwa kwa ofisi za serikali na kusababisha baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani kushindwa kurejesha fomu za kuwania uongozi walizochukua na kuzijaza.

Figisu hizo zinadaiwa kuwapo wakati tayari Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ambaye ndiye mwenye dhamana ya uchaguzi huo akiwa ametoa angalizo kabla ya uchukuaji wa fomu hizo akitaka kila upande kutimiza wajibu kikamilifu ili kufanikisha uchaguzi huo.

> Sitaki kuona mtu anabughudhiwa kwa jambo lolote, hivyo kila mmoja ni ruksa kurejesha fomu au kuchukua fomu bila kuwapo kwa vikwazo.

Kabla ya utoaji wa fomu, Jafo, alitoa maelekezo kwa wasimamizi wa uchaguzi wahakikishe hauingiliani na changamoto za aina yeyote kama walivyopewa maelekezo.

Kwa mujibu wa Jafo, wasimamizi walitakiwa kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake stahili ya kidemokrasia kama, ambavyo serikali inakusudia, ili kila mtu ashiriki katika uchaguzi bila kukwazwa na jambo lolote.

Kwamba serikali inataka kuona kila Mtanzania anapata haki yake ya msingi ya kutimiza matakwa ya kidemokrasia, hivyo ni muhimu kusimamia kanuni katika mchakato mzima wa kuchukua na kurejesha fomu.

Vyama vya siasa navyo vinapewa angalizo kwamba vitumie vizuri demokrasia kwa kupeleka watu wanaowakusudia na kuwadhamini kwa mujibu wa kanuni, huku watendaji wa vijiji na mitaa wakiwa hawaruhusiwi kutekeleza jukumu lolote, ambalo linapaswa kuamuliwa kwanza na halmashauri za vijiji au mitaa.

### UCHUKUAJI WA FOMU

Baada ya maelekezo hayo ya Jafo, fomu za kuwania uongozi zilianza kutolewa Oktoba 29 mwaka huu kwa muda wa siku saba ambazo zilikamilika juzi Jumatatu Novemba 4, huku kukiwa na malalamiko kadhaa.

Malalamiko hayo kutoka kwa vyama vya upinzani ni wagombea kurejesha fomu na kukuta ofisi za serikali zimefungwa na kulazimika kukesha nje ya ofisi hizo ili kuhakikisha wanakabidhi fomu hizo.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ndicho kilichodai kufanyiwa vituko kwamba baadhi ya wagombea wake wamekwamishwa kwa makusudi katika mchakato mzima wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, kuna maeneo ofisi za serikali hazijafunguliwa tangu Novemba Mosi, mwaka huu, hivyo kusababisha wagombea kushindwa kurejesha fomu katika ofisi husika.

Miongoni ofisi hizo ni za Kata ya Sola, Shanwa na Nyalikungu wilayani Maswa, mkoa Simiyu na kusababisha wagombea wa chama kulazimika kukesha na kupelekewa chakula na maji kwenye eneo la tukio.

Ratiba ya mchakato wa uchaguzi huo inaonyesha kuwa uteuzi wa wagombea, ambao hufanywa na Msimamizi wa Uchaguzi katika kata husika, ulitarajiwa kufanyika jana.

Uteuzi huo ni kwa nafasi za uenyekiti wa kijiji, mtaa, ujumbe wa halmashauri ya kijiji na mtaa na kufuatiwa na kampeni, ambazo zitaanza Novemba 17 na kumalizika Novemba 23 na kufuatiwa na uchaguzi.

### MAJIBU YA JAFO

Akijibu malalamiko hayo anakiri kutambua uwapo wa matatizo mbalimbali yaliyojitokeza, likiwamo la baadhi ya maeneo ambayo ofisi za serikali zilifungwa na hivyo akatoa maelekezo zifunguliwe na watu wachukue fomu na kuzirejesha.

Anasema, malalamiko yote yaliyotokea katika maeneo mbalimbali baada ya kuyapokea alikuwa anayatolea maelekezo ili kusiwapo na mkwamo katika mchakato mzima wa kuchukua fomu.

"Wale niliowapa dhamana, niwaagize wasimamizi wote wa uchaguzi kuhakikisha vituo vyote vinafunguliwa kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria zetu," anasema na kuongeza:

"Sitaki kuona mtu anabughudhiwa kwa jambo lolote, hivyo kila mmoja ni ruksa kurejesha fomu au kuchukua fomu bila kuwapo kwa vikwazo."

Jafo anawataka Watanzania waendelee kushiriki katika mchakato wa uchaguzi huo kwa amani na wakuu wa mikoa na wilaya kuendelea kusimamia suala zima la amani.

Mbali na hayo, Waziri Jafo anawataka wadau kuacha kuhujumiana kwa njia moja au nyingine, kwa sababu hujuma hizo inawezekana zinatoka katika maeneo mbalimbali.

Iwapo maelekezo hayo ya serikali yatazingatiwa, uchaguzi huo unaotarajiwa kuhusisha wapigakura milioni 19.7 utafanyika kwa amani na utulivu huku kila Mtanzania akipata haki ya kuchagua kiongozi anayemtaka.

### IDADI YA WAPIGAKURA

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014, Watanzania waliojiandikisha kupiga kura walikuwa ni 11,882,086, lakini mwaka huu takriban milioni nane wameongezeka.

Hata hivyo, mwaka huu Watanzania milioni 19.7 wanatarajia kushiriki katika uchaguzi utakaofanyika mwishoni mwa mwezi huu ingawa uchukuaji na urejeshaji wa fomu ulitawaliwa na malalamiko kwenye baadhi ya maeneo.

Uchukuaji wa urejeshaji wa fomu umemalizika, sasa kinachoendelea ni uteuzi wa wagombea na kisha zitafuata kampeni zitakazoanza Novemba 17 mwaka huu, ni vyema wahusika wakazingatia maelekezo ya Jafo.

Lengo la kuzingatia maelekezo ni kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima kama ilivyojitokeza katika mchakato huo uliomalizika, ikidaiwa ofisi za serikali kufungwa na kusababisha baadhi ya wagombea kushindwa kurejesha fomu.





## DC atema cheche vitendo vya rushwa

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi, amewaonya wagombea wa nafasi za uenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijiji kuepukana na vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mahundi alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na Nipashe ikiwa ni siku chache tangu wagombea wa nafasi hizo warejeshe fomu za kugombea, mchakato ambao alisema ulifanyika katika hali ya utulivu.

Alisema zikiwa zimekabaki siku kadhaa kuelekea uchaguzi huo, baadhi ya wagombea wasiokuwa waadilifu hutumia muda huo kuwarubuni wananchi kuwachagua ilhali hawana uwezo wa kuwaongoza.

Mkuu wa Wilaya alisema vyombo vyote vya haki na sheria vimejipanga vyema kukabiliana na wagombea ambao watabainika kufanya vitendo vya rushwa na kuchukuliwa hatua.

"Kama unajiamini kwa nini utoe rushwa ili wakuchague? Alihoji Mahundi na kuongeza kuwa:

"Ninachojua kiongozi mzuri ni yule anayejiamini kwa kazi zake na uadilifu wake. Sitakubali mtu atumie nguvu wananchi kumchagua. Pia sitakubali kuona wilaya yangu inaingia dosari kwa sababu ya masuala ya rushwa," alisema Mahundi.

Aliwasihi wananchi kujitokeza kwa wingi kuelekea katika uchaguzi ujao ili kumchagua kiongozi ambaye atawafaa na atawaletea maendeleo katika maeneo yao.

Mahundi aliwataka wananchi kutokubali kupokea rushwa kutoka kwa wagombea ambao wanahitaji kuchaguliwa badala yake wachague viongozi waadilifu na walio tayari kutumika kwa maslahi ya wananchi.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alipozungumza na waandishi wa habari hivi karibuni alisema kamwe hawatamwonea haya kiongozi yeyote kujihusisha na rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema taasisi hiyo inafanya kazi kwenye maeneo yote ya mkoa wa Mbeya tangu mchakato ulipoanza kwa kushirikiana na wasamaria wema ambao hutoa taarifa za viashiria vya rushwa.

**"Ninachojua kiongozi mzuri ni yule anayejiamini kwa kazi zake na uadilifu wake. Sitakubali mtu atumie nguvu wananchi kumchagua. Pia sitakubali kuona wilaya yangu inaingia dosari kwa sababu ya masuala ya rushwa," alisema Mahundi.**

# Maandalizi kilimo korosho Mbarali moto

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

KILO 300 za mbegu ya korosho zimekabidhiwa kwa wananchi wa kata ya Miyombeni katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kwa lengo la kuzalisha miche 55,000 itagawiwa kwa wakulima wilayani hapa.

Akikabidhi mbegu hizo juzi, Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, alisema lengo ni kuhakikisha korosho linakuwa moja ya mazao ya biashara badala ya kutegemea kilimo cha mpunga pekee ambacho wakati mwingine humwingizia hasara mkulima.

Mfune alisema serikali imetoa kilo 300 za mbegu kwa wakulima ili kuwahamasisha kulima zao hilo lakini mikakati ni kwamba kila mkulima wilayani hapa anatakiwa apande korosho.

"Korosho ni miongoni mwa mazao matano ya kimkakati ambayo serikali inasisitiza kulima katika maeneo mbalimbali kwa sababu lina faida kubwa kulinganisha na mazao mengine.

"Kwa kulitambua hilo, wilaya yetu ya Mbarali tumetoa kilo 300 za mbegu kwa ajili ya kupanda na miche 55,000. Tunategemea kuizalisha na kuigawa kwa wakulima," alisema Mfune.

Aliongeza kuwa si mashambani pekee miche ya korosho inapaswa kupandwa bali hata kwenye makazi ya watu na kwa kufanya hivyo kutaleta faida si tu kupata tunda la korosho bali hata hewa safi na kivuli.

Diwani wa Miyombeni, Mustaulo Sanzala, aliwashauri wakulima kuchangamkia fursa kwenye zao la korosho na kuacha kusikiliza maneno ya baadhi ya wanasiasa wanaodai ni zao ambalo limekuja kuua kilimo cha mpunga.

Alisema zao hilo linahitaji uvumilivu kwa kuwa huchukua miaka mitano ndipo huanza kuzaa matunda na kwamba katika kata yake, kijiji cha Mapogoro kimegawa mashamba kwa wananchi ili kulima zao hilo.

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Wilaya ya Mbarali, Daniel Kamwela, alisema hadi sasa wakulima 229 wamesajiliwa kwa ajili ya uzalishaji wa korosho na hekta 328 zimepandwa zao hilo.

Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali imenunua kilo 500 za mbegu za korosho ambazo zinategemewa kuzalisha miche 70,000.



Diwani wa Kata ya Mwakibete, jijini Mbeya, Lucas Mwampiki (aliyesimama) akiwaongoza wazazi wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Uhuru, kwenye majadiliano ya namna ya kukabiliana na mrundikano wa wanafunzi katika shule hiyo, juzi, ambapo walikubaliana kujenga shule nyingine. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajasiriamali wenye ulemavu waomba msaada

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

KIKUNDI cha Watu Wenye Ulemavu (Uwalemba) katika Kata ya Rujewa wilayani Mbarali mkoani Mbeya, kimeiomba serikali kuwasaidia eneo kwa ajili ya kufanya shughuli za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni na mafuta ya kupakaa.

Ombi hilo lilitolewa jana na katibu wa kikundi hicho, Ramadhani Shamte, wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, alipotembelea na kuangalia shughuli za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazofanywa na kikundi. Shamte alisema wamejitahidi kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao kwa kutumia teknolojia za kisasa lakini changamoto kubwa inayowakabili ni eneo kuwa finyu, hivyo kuomba kusaidiwa eneo kubwa ambalo litasaidia kupanua wigo wa uzalishaji.

Alisema mbali na kuhitaji eneo kubwa la kufanyia shughuli zao, pia wana tatizo la masoko kwa kuwa licha ya kuzalisha kwa wingi bidhaa za mafuta ya kupakaa, sabuni za miche na maji hawana soko la uhakika kuuza bidhaa hizo.


Shamte aliiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika ili kuuza bidhaa zao ambazo alisema zinakidhi ubora katika soko la ushindani ndani na nje ya nchi.

"Sisi walemavu tuliamua kujikusanya na kuanzisha kikundi ambacho kinafanya shughuli mbalimbali za maendeleo. Tulibahatika kupata mkopo wa Sh. milioni 46 kutoka halmashauri uliotuwezesha kupata mtaji wa kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni. Tatizo linalotukabili ni eneo finyu la kufanyia shughuli zetu na soko, hivyo tunaomba serikali na wadau wengine watusaidie," alisema Shamte.

Alisema kiwanda chao ambacho kimepewa jina la Mbarali Soap hadi sasa kimetoa ajira kwa watu 12 ambao kati yao sita ni wenye ulemavu na sita hawana ulemavu.

Mfune alifurahishwa na uthubutu wa kundi hilo la walemavu bila kujali hali zao kujiingiza kwenye shughuli za uzalishaji na kushauri watu wengine kuiga mfano huo badala ya kushinda vijiweni wakiilalamikia serikali kwamba haijafanya jambo lolote.

Aliwashauri wananchi na vikundi vingine kuchangamkia fursa za mikopo zinazotolewa na halmashauri huku akisisitiza asilimia 10 ya mapato ya ndani imetengwa kwa ajili ya kuvisaidia vikundi vya kinamama, vijana na wenye ulemavu.





# Tangazo serikali laathiri uhifadhi

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KUKOSEKANA kwa tangazo la serikali katika umiliki wa Hifadhi ya Misitu ya Kondoa Irangi yenye michoro ya asili katika milima ya Kolo-Kondoa ambayo ni kivutio kikubwa, kumekuwa tatizo katika kuilinda hifadhi hiyo.

Meneja wa Wakala wa Huduma za Misiti Tanzania (TFS) Wilaya ya Kondoa, Hashimu Kitova, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa wa Dodoma iliongozwa na Mkuu wa Mkoa, Dk. Binilith Mahenge, ilipotembelea hifadhi hiyo, ikiwa ni moja ya ziara zake ya kukagua hifadhi zilizopo.

Alisema katika Wilaya ya Kondoa kuna hifadhi tatu za misitu ambazo ni Chemshem yenye hekta 2,000, Salanga yenye hekta 8,662 na Irangi yenye zaidi ya hekta 13,000, lakini kwenye tangazo la serikali linaonyesha ni mbili tu - Chemchem na Salanga.

Hatua ya kukosekana kwa tangazo katika hifadhi hiyo, alisema ni tatizo katika kuhifadhi rasilimali zilizopo.

Katova alibainisha njia wanazotumia katika kuhifadhi misitu hiyo na kutokuwa na uharibifu ikiwamo kuwashirikisha jamii juu ya umuhimu wa misitu hiyo na faida zake japo si wote wanaelewa.

"Tumekuwa tukishirikisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kutunza hifadhi lakini wachache wamekuwa wanaelewa juu ya somo hilo," alisema Katova.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Mahenge, aliipongeza wilaya hiyo kwa kulinda hifadhi za misitu ikiwamo kukomesha vitendo vya uchomaji wa misitu.

"Nawaomba mwendelee kulinda hifadhi zetu ili ziendelee kuvutia kwa sababu hizi ni urithi wetu," alisema Dk. Mahenge.

Alisema baada ya kujiridhisha na kuona misitu hiyo inavyolindwa, ameahidi kupeleka mapendekezo hayo katika kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ili kupitisha msitu huo upate tangazo la serikali na kuwa hifadhi.

**"Tumekuwa tukishirikisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kutunza hifadhi lakini wachache wamekuwa wanaelewa juu ya somo hilo," alisema Katova.**

# Vituo tembezi vya mafuta vyaja rasmi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imesema inatarajia kuanzisha utaratibu wa kuwapo vituo vya mafuta vinavyotembea ili kurahisisha upatikanaji wa nishati hiyo maeneo ya vijijini.

Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa Ewura, Titus Kaguo, alisema hayo mwishoni mwa wiki katika semina ya waandishi wa habari iliyofanyika jijini hapa.

Kaguo alisema hayo alipokuwa akitoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali juu ya masuala ya mamlaka hiyo.

"Kwa sasa tunakuja na vituo vya mafuta vinavyotembea ambavyo vitatoa huduma vijijini. Kwa mfano mtu anakuwa na gari ndogo kama 'kirikuu' unaweka tangi ambalo litakuwa limepimwa halina athari au pikipiki za guta mtu anabeba lita 50 anapita njia labda ya Mtera na kuuzia pikipiki. Hii itasaidia kuziba pengo la ukosefu wa vituo vya mafuta maeneo ya vijijini," alisema.

Alieleza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinafanyia utafiti suala hilo na liko katika hatua za juu na hivi karibuni watatoa taarifa ya kuanza kwa biashara hiyo.

"Tunaimani itapunguza athari za watu kujenga vituo vikubwa kwenye vijiji. Usafirishaji mafuta kwenye madumu pia ni hatari, hatuwezi kuruhusu vitu vya aina hii kutokana na uhaba wa vituo," alisema.

Aidha, Kaguo alisema kuna mfumo wa ujenzi wa vituo vijijini lengo ni kuwasaidia watu ambao hawana uwezo wa kujenga vituo vikubwa. Vituo vidogo vya mafuta vitakuwa mkombozi na gharama zake nui takriban Sh. milioni 50 kwa kituo kimoja.

"Kujenga kituo ni gharama, kituo kikubwa kama pale Dar es Salaam unaweza kukuta gharama yake ni kati ya Sh. milioni 800 hadi Sh. bilioni moja, ndiyo maana tumekuja na mfumo unaoendana na maeneo ya vijijini.

Kwa mfano kituo cha pampu moja ambacho kina uwezo wa kuwa na lita za mafuta 100,000, huwezi kuweka lita milioni mbili wakati wewe unauzia pikipiki ambazo zinatumia lita 12," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany, alitoa tahadhari mbalimbali kuhusu matumizi ya mafuta ikiwamo magari ya kubebea mafuta kuegeshwa au kulazwa pasipo husika na badala yake yawekwe sehemu maalumu zilizotengwa.

Mchany alitaja tahadhari nyingine ni kuwa shughuli zote zinazohusu mafuta ya petroli lazima zifanyike kwa umakini na uangalifu mkubwa ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

Alisema ni muhimu kuzingatia na kufuata sheria, kanuni, viwango vya ubora na masharti ya leseni wakati wote huku akiwataka kuzingatia utunzaji, usafirishaji na utumiaji na uuzaji wa bidhaa za petroli.


Distributed via ippmedia

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isack Kamwelwe (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Wasichana ya Kondoa, mkoani Dodoma juzi, alipotembelea kuangalia mtandao jamii wa Kondoa wa intaneti ya kutumia mawimbi ya TV, uliobuniwa na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) na kuunganishwa shuleni hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri ataka huduma nafuu intaneti

**Na Ibrahim Joseph, KONDOA**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isack Kamwelwe, amewataka watoa huduma za mawasiliano nchini kushirikiana ili kutatua changamoto ya gharama za huduma za mtandao (intanet) ili kuwa nafuu kwa wananchi wa mjini na vijijini.

Kamwelwe alisema hayo juzi wakati wa kilele cha kongamano la nne la masuala ya mtandao jamii kwa nchi za Afrika lililofanyika Kondoa mkoani Dodoma.

Pia aliwataka watoa huduma za mawasiliano kufikisha huduma ya mtandao wa intaneti yenye kasi vijijini ili kuwafikia wananchi wa maeneo hayo ambao ni kundi kubwa nchini.

Alisema kutokana na gharama za huduma za intaneti hapa nchini kuwa kubwa, iko haja ya watoa huduma za mawasiliano kuitatua ili wananchi waweze kunufaika.

"Gharama za mtandao wa intaneti bado ziko juu kwa hiyo iko haja kwa wadau mbalimbali wa mawasiliano kushirikiana ili kuleta majawabu yatakayofanya huduma hii ya mawasiliano kuwa nafuu maeneo ya vijijini na mijini," alisema.

Alisema huduma za intaneti kwa sasa zimekuwa zikitumika kupata habari, kuongeza elimu na kupata taarifa za matukio katika jamii, hivyo gharama zake zinatakiwa kuwa chini ili wananchi wengi wamudu.

Waziri Kamwelwe alisema serikali inatambua changamoto zinazokwamisha baadhi ya huduma kutowafikia wananchi, hivyo zitashughulikiwa ili wananchi wanufaike na uwapo wa mawasiliano nchini.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hadi Juni, mwaka huu, kulikuwa na laini za simu milioni 43.75 na watumiaji wa mtandao wa intaneti walikuwa milioni 23.14 mpaka mwaka jana.

Kamwelwe alibainisha kuwa takwimu hizo zinaonyesha kuna tofauti ya watumiaji wa simu na wale wa huduma ya intaneti kutokana na kuchangiwa na baadhi ya maeneo kukosa huduma hiyo.

"Hii ina maana kwamba kukosa intaneti watu hawa hawawezi kushiriki katika uchumi wa kidijitali, hivyo kutonufaika huduma za mtandao kama vile elimu kwa mtandao na afya," alisema.

Msimamizi na mvumbuzi wa mtandao jamii Kondoa, unaotumia mawimbi ya televisheni, Jabhera Matogoro kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) alisema lengo la kuwapo mtandao huo ni kufikisha huduma ya intaneti kwa watu wa maeneo hayo.

Matogoro alisema katika utafiti wao walijenga mnara unaotumia mawimbi ya televisheni ili kufikisha huduma ya mtandao wa intaneti katika jamii na kwa kuanza, waliunganisha katika Shule ya Wasichana Kondoa, Chuo cha Ualimu Bustani na maeneo ya vijiji vilivyo jirani.

Alisema pamoja na kusherehekea mafanikio hayo, waliunganisha na kongamano ambalo limeshirikisha watu kutoa nchi za nje zipatazo 18.



# Makamu wa Rais awapa somo wahandisi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wahandisi wa miradi ya ujenzi wa barabara wanapaswa kuzingatia maadili ya kazi zao hasa kwenye maeneo yenye mteremko unaoishia kwenye madaraja ili kuzuia athari kwa wananchi wanaoishi jirani na sehemu hizo.

Amesema kuna uzoefu mkubwa unaojitokeza kwenye maeneo yenye madaraja makubwa wakati wa mvua za masika kukumbwa na maji mengi yanayoishia katika makazi ya wananchi wanaoishi karibu na madaraja.

Balozi Seif Ali Iddi alisema hayo jana Mkokotoni alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Bububu hadi Mkokotoni na kuridhika na kazi iliyofika ya uimarishaji wa miundombinu.

Alisema wahandisi wa miundombinu wana jukumu la kukahikisha maisha ya wananchi yanakuwa salama katika makazi yao ili kuipa nafasi serikali na taasisi zake kushughulikia masuala mengine badala ya nguvu kubwa kuitumia katika kuihudumia jamii wakati wa majanga.

Msimamizi wa ujenzi wa barabara hiyo, Mhandisi Ismail Ibrahim Kulengwa, alisema ujenzi huo unaohusisha kilomita 52, unatarajiwa kukamilika Februari, mwakani na sasa umefikia asilimia 63.

Mhandisi Kulengwa alisema barabara ya Bububu hadi Mkokotoni pekee hivi sasa ujenzi wake umeshafikia asilimia 80% unaotarajiwa kukamilika Januari, mwakani ukihusisha madaraja 14, kati ya hayo manane makubwa na sita yaliyobakia ni ya kati.

Alisema kilomita 26 kati ya 31 za barabara hiyo ya Mkokotoni hadi Bububu tayari imeshawekewa lami huku kazi ikiendelea hivi sasa itakayokwenda sambamba na uwekaji wa vyuma katika maeneo ya daraja na yale yenye mteremko mkali.

Baadaye, Balozi Iddi aliangalia maendeleo ya ujenzi wa nyumba watakazopewa wananchi waliokumbwa na mafuriko zinazojengwa na kusimamiwa na Kamisheni ya Maafa Zanzibar.

Msimamizi wa ujenzi wa nyumba hizo, Mhandisi Ernest Mambangula, alimweleza Balozi Iddi kwamba ujenzi huo uko katika hatua nzuri licha ya kipindi hiki kusubiri mabati kwa ajili ya uwezekaji.

Mhandisi Ernest alisema kila jengo litakuwa na uwezo wa kuhudumia familia mbili zitakazobahatika kupata vyumba vitatu, jiko, sebule na huduma muhimu za kibinadamu vikiwamo vyoo.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Kamisheni ya Maafa Zanzibar, Muhidini Ali Muhidini, alimweleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba mradi huo unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa serikali ifikapo Januari, mwakani.



Distributed via ippmedia

Kaimu Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Ramadhan Mtindasi (kushoto), akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange (kulia), kuhusu moja ya swichi zinazotumika kuwasha pampu ya Kibamba, inayosukuma maji kwenye tangi la Kisarawe mkoani Pwani, wikiendi. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Cyprian Luhemeja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Korea Kusini yaahidi makubwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amefanya mazungumzo na ujumbe wa ubalozi wa Jamuhuri ya Watu wa Korea kwa ajili ya kuzidisha ushirikiano katika sekta ya elimu.

Katika mazungumzo yao Waziri Juma aliomba nchi hiyo kusaidia kujenga kituo cha mafunzo ya amali Zanzibar katika Manispaa ya Mjini Magharibi kwa kuwa kilichopo sasa ni kidogo kulinganisha na mahitaji ya wananchi wanaotaka elimu hiyo.

Alisema Tanzania ya sasa ni ya viwanda, hivyo ili kuwasaidia vijana katika kupambana na ajira ni lazima kuwapatia elimu ya amali ili wapate ajira na kujiajiri kutokana na ujuzi watakaoupata.

Juma alisema vyuo vya elimu vya amali vilivyopo vina idadi kubwa ya wanafunzi na hii inasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya wananchi wanaotaka kupati elimu hiyo ambayo asilimia kubwa huwezesha kujiajiri baada ya kumaliza masomo.

Pia alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuinua elimu kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Korea katika kusaidia masuala mbalimbali yakiwamo ujenzi wa majengo ya shule.

Naye Balozi wa Jamuhuri ya Watu wa Korea nchini Tanzania, Tae-ick Cho, alisema wataendeleza ushirikiano uliopo baina yao na Zanzibar katika kusaidia miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Alisema Jamhuri ya Watu wa Korea itaendeleza miradi yao katika sekta ya elimu ambayo ni muhimu kwa karne ya sasa kutokana na maendeleo ya nchi kuhitaji sana elimu ambayo yanakwenda sambamba na matumizi ya sayansi na teknolojia.

Balozi huyo alimhakikishia Waziri kuwa ataendelea kuisaidia sekta hiyo ili Zanzibar ipige hatua.

Mazungumzo hayo yalihudhuriwa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said; Katibu Mkuu wa Wizara, Idrisa Muslim Hija na Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji, Abdullah Mzee Abdullah.

# SMZ yawaonya wavunja amani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema haitasita kumdhibiti mara moja mtu au kikundi chochote kinachoashiria kusababisha uvunjifu wa amani hasa kipindi hichi ambacho taifa linaelekea kwenye uchaguzi mkuu mwakani.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alitoa hadhari hiyo jana alipofanya ziara maalum ya kukagua miradi ya maendeleo pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi inayosimamiwa na taasisi za serikali ndani ya Wilaya ya Kaskazini A.

Balozi Iddi katika ziara hiyo, alizindua rasmi gari la kubebea wajongwa lililotolewa na uongozi wa Jimbo la Kijini katika Kituo cha Afya cha Kijini na kushiriki kazi za ujenzi wa Tawi la Kibuyuni Jimbo la Mkwajuni.

Pia aliweka jiwe la msingi la mradi wa CCM Tawi la Chaani na kuonya kuwa serikali haitaridhia kuchezewa kwa amani ya nchi iliyopo sasa.

Alisema hakuna mwananchi hata mmoja aliyeshiba uzalendo na kulinda heshima yake anayependelea kuona mazingira aliyoyazoea muda wote wa maisha yake yanazungukwa na cheche za shari.

Alitahadharisha kwamba wako baadhi ya watu wameshaanza harakati za kuzunguka mitaani Unguja na Pemba na kuanza fitna na majungu yanayoashiria kutaka kuwagawa wananchi katika mwelekeo wa taifa kukaribia kuingia ndani ya uchaguzi mkuu mwakani.

Balozi Seif alisema wachafua amani lazima waogopwe kwa kuwa ni sawa na wagonjwa wa maradhi hatari ya kuambukiza kama kifua kikuu wanaostahiki kudhibitiwa ili wasieneze uchafuzi huo.

**Balozi Iddi katika ziara hiyo, alizindua rasmi gari la kubebea wajongwa lililotolewa na uongozi wa Jimbo la Kijini katika Kituo cha Afya cha Kijini na kushiriki kazi za ujenzi wa Tawi la Kibuyuni Jimbo la Mkwajuni.**

# Bil. 3/- kujenga bwawa Kaliua

**Na Tiganya Vincent**

SERIKALI inatarajia kutoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Maji katika eneo la Ichemba wilayani Kaliua mkoani Tabora.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kukamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo kwa gharama ya Sh. milioni 40.8 kwa kutumia mapato yake ya ndani.

Kauli hiyo imetolewa jana na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, wakati wa ziara yake katika Wilaya ya Kaliua ya kukagua miradi ya maji na kutatua kero za maji.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia jumla ya wakazi 229,290 wa Kata za Ichemba, Kanoge, Mwongozo, Nhwande, Makingi, Sasu, Kanido, Milambo na Igombenkulu na wakimbizi kutoka Burundi.

Waziri huyo alisema ujenzi wa bwawa hilo unatarajiwa kuanza, baada ya mvua za masika kumalizika.

Aidha, Prof. Mbarawa alisema kwa kutambua tatizo la maji katika eneo hilo, serikali imetoa Sh. milioni 571 kwa ajili ya mradi wa dharura wa kutatua tatizo la maji Kaliua Mjini wakati wakisubiri utekelezaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria.

Alisema mradi wa uletaji maji kutoka Ziwa Victoria katika mji wa Kaliua ni sehemu ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 ya Tanzania ambao unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. trilioni moja.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, alisema eneo hilo linakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji ardhini na kutokuwa na vyanzo vya kutosha vya maji.

Alisema msaada wa kuwasaidia wakazi wa wilaya hiyo ni kupitia kujengewa mabwawa katika maeneo yenye uwezo wa kujengwa na kupata maji kutoka katika vyanzo kama vile Ziwa Victoria na mito iliyokaribu.

# Shule zinazoanzishwa kiholela kufutwa

**Na Sabato Kasika**

BARAZA la Usimamizi la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), limesema serikali itazifuatilia na kuzibaini shule huria zinazoanzishwa kinyume cha taratibu na kuzichukulia hatua ikiwamo kuzifunga.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Dk. Naomi Katunzi, kwenye mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Brothers Academy.

Alisema shule huria ni mkombozi wa watu wengi wenye ndoto zao kitaaluma zilizokwamishwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo za mimba, familia kushindwa gharama za masomo.

"Wengine wamekwama kwa kufukuzwa au kushindwa katika mitihani, lakini ni kwamba serikali itazifuatilia na kuzibaini shule huria zinazoanzishwa kinyume cha taratibu na kuzichukulia hatua ikiwamo kuzifunga," alisema Dk. Katunzi.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kuambiwa na uongozi wa shule hiyo kuwa uwepo wa shule huria zilizoanzishwa bila kukidhi vigezo, unachafua sifa ya huduma zitolewazo katika shule zilizokidhi vigezo na kusajiliwa kihalali.

"Hampo kwenye shule ya kitapeli; hapa mpo kihalali, hata katika mtihani zingatieni uadilifu, uaminifu na kufuata maagizo na taratibu za mtihani, msisahau kumtanguliza Mungu kama anavyosisitiza Rais John Magufuli siku zote na kuwa wakweli," alisema.

Uongozi wa Shule Huria ya Brothers Academy uliiambia (TEWW) kuwa shule za aina hiyo haziwezi kuwa na usimamizi mzuri, uratibu na maadili.

"Baadhi ya watu wanahukumu shule zote huria kuwa hazisaidii, bila kuangalia kuwa zipo zisizozingatia vigezo na ni kama kenge katika msafara wa mamba, hizo ndizo zenye shida," alisema Mkuu na Mkurugenzi wa shule hiyo, Robert Rwezaula.

Rwezaula alisema, shule hiyo ni karakana ya waliofeli mtihani na ambao hawakufikia ndoto zao katika mfumo rasmi kwa sababu mbalimbali na wamelenga kwamba wanaohitimu shuleni hapo wasiwe na ufaulu wa chini ya daraja la tatu.

"Tunamshukuru Mungu kwamba, vijana wetu wanafanya vizuri na wengi wapo vyuo vikuu, wamehitimu na wengine wanafundisha katika shule mbalimbali," alisema.

Awali, akisoma risala ya uongozi wa shule hiyo, mwalimu Christopher Marko alisema, kumekuwa na ongezeko la vituo vinavyoanzishwa kiholela na bila kufuata taratibu zilizowekwa hivyo kusababisha shule huria zilizosajiliwa kihalali kuonekana zinajiendesha kiholela.




Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwa katika foleni ya kukata tiketi kwa ajili ya usafiri wa mabasi ya mwendokasi, katika Kituo cha Kimara Korogwe, jijini humo jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanawake 102 wapata fursa ya mafunzo ya udereva NIT

**Na Anaeli Mbise**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimefanya uzinduzi wa mafunzo maalum kwa madereva wanawake 102 ambao watapatiwa mafunzo ya uendeshaji wa mabasi ya abiria pamoja na malori ya mizigo yakiwa na lengo ya kuwainua kiuchumi.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe amesema hayo alipokuwa anazindua mafunzo hayo na kusema kuwa yatakuwa muhimu kwa wanawake katika kipindi hiki ambacho nchi inaelekea katika uchumi wa kati ifikapo 2025.

"Haya mafunzo yamekuja kwa wakati sahihi ambapo sasa tutapata madereva ambao watakuwa na uwezo wa kuendesha mabasi pamoja na kusafirisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia malori ili kufikisha bidhaa zitakazo tumiwa kwenye viwanda vyetu vya ndani," amesema Kamwelwe.

Aidha, Kamwelwe alisema kuwa mafunzo hayo yatasaidia katika kupunguza ajali za barabarani kutokana na utafiti kuonyesha wanawake ni watu makini wanapokuwa wanaendesha vyombo vya moto na kuongeza kuwa kwa sasa yameanzia katika Jiji la Dar es Salaam, lakini ameahidi kuyasogeza pia katika mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha ili kupata madereva wengi zaidi.

Mkuu wa NIT, Prof. Zakaria Mganilwa, alisema kuwa jumla ya madereva 102 watapatiwa mafunzo hayo ambayo yatadumu kwa wiki saba.

Prof. Mganilwa alisema kuwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Mamlaka ya Usimamizi wa Isafiri wa Nchi Kavu (LATRA) pamoja na serikali wameanzisha mafunzo hayo ili kutoa fursa kwa wanawake kujifunza pia sheria mbalimbali za usalama barabarani.

"Mafunzo hayo yatatoa chachu na hamasa kwa wanawake wengine kushiriki katika mafunzo ya udereva wa mabasi pamoja na malori kwani lengo letu pamoja na serikali ni kukuza uchumi wa kinamama pamoja na kuwatafutia fursa za ajira," alisema Prof. Mganilwa.

Mmoja wa wadau wa usalama barabarani ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema mafunzo hayo yatapunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani kutokana na umakini ambao wanawake wengi wanao wanapokuwa wanaendesha vyombo vya moto.

**HABARI KIMATAIFA**

## Iran kupunguza ahadi mkataba wa nyuklia

**TEHRAN,** Iran

IRAN imesema itachukua hatua mpya katika kupunguza ahadi ilizotoa katika mkataba wa kihistoria wa nyuklia wa 2015 kuanzia leo.

Imesema lengo ni kuongeza gesi kwenye mitambo yake 1,044 ya urutubishaji Urani katika kiwanda chake cha Fordow.

Katika hotuba yake iliyorushwa jana kwenye televisheni, Rais Hassan Rouhani alisema hatua hiyo ni majibu ya moja kwa moja kwa Rais wa Marekani, Donald Trump kuiondoa Marekani katika makubaliano ya nyuklia yaliotiwa saini mwaka 2015.

Katika makubaliano hayo, Iran inaruhusiwa kuongeza viwango vya kurutubisha madini ya Urani japo bila kuongeza gesi kinyume na tangazo lililotolewa na Rouhani.

Juzi, Iran ilizindua mitambo aina ya 30 IR-6 ya kurutubisha madini ya Urani na kwa sasa taifa hilo lina mitambo 60 ya kisasa hali inayoonyesha upeo na azma yake.

Mkuu wa Shirika la Nishati ya Atomiki nchini humo, Ali Akbar Salehi alisema Iran iliyokuwa inazalisha gramu 450 sawa na pauni moja ya madini ya Urani kwa siku, sasa itazalisha kilo tano ambayo ni sawa na pauni 11 kwa siku. **DW**

## Korea Kaskazini yaikosoa Marekani

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imesema kuwa hatua ya Marekani kuirejesha kwenye orodha ya nchi zinazofadhili ugaidi inahujumu matarajio ya juhudi za kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili.

Taarifa hiyo imekuja wakati nchi hiyo ikiendeleza shinikizo kwa Marekani kuhusiana na mkwamo wa mazungumzo ya nyuklia.

Wiki iliyopita, ilifyatua makombora iliyoyataja kuwa ya kisasa ikiwa ni tukio la kwanza la jaribio la makombora kufanywa katika mwezi mmoja.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Korea Kaskazini ilisema jana kuwa ripoti ya ugaidi iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani wiki iliyopita inadhihirisha kwa mara nyingine kuwa nchi hiyo inatekeleza sera ya uhasama kuelekea Korea Kaskazini.

Korea Kaskazini imekuwa kwenye orodha mbaya ya ugaidi kwa miongo miwili baada ya majasusi wake kulaumiwa kwa ulipuaji bomu wa ndege ya Korea Kusini ambao ulisababisha vifo vya watu 115 katika mwaka wa 1987.

Iliondolewa 2008 wakati Marekani ikijaribu kuishawishi Korea Kaskazini kufikia makubaliano ya nyuklia. **DW**

# Mamia waokolewa msikitini na minyororo

**ABUJA,** Nigeria

POLISI nchini Nigeria imewaokoa watu 259 kutoka katika kituo kisichokubalika kisheria kilichopo ndani ya msikiti wa mji wa Ibadan, uliopo Jimbo la Kusini Magharibi mwa nchi hiyo la Oyo.

Msemaji wa Polisi, Gbenga Fadeyi, alisema miongoni mwa waliookolewa katika uvamizi wa polisi, wengi walikuwa wamefungwa kwa minyororo katika eneo la msikiti.

Katika kipindi kilichopita, zaidi ya watu 1,000 waliokolewa kutoka kwenye vituo vya kidini ambako mara kwa mara watu wamekuwa wakishikiliwa.

**Katika kipindi kilichopita, zaidi ya watu 1,000 waliokolewa kutoka kwenye vituo vya kidini ambako mara kwa mara watu wamekuwa wakishikiliwa.**

Wazazi wamekuwa wakiwatuma watoto wanaowasumbua kitabia na vijana wanaoaminiwa kuwa na uraibu wa dawa za kulevya au wale waliopatikana na makosa madogo katika vituo vya Koran vya kurekebisha tabia.

Lakini, maofisa wamevifananisha vituo hivyo na vituo vya ukatili ambapo watu wanafungwa minyororo, kufungwa pamoja na kufanyiwa dhuluma.

Waliotekwa waliachiliwa Jumatatu jioni baada ya polisi kupewa taarifa na kijana mwenye umri wa maika 17 ambaye alikuwa ametoroka kutoka katika mahabusu hiyo na vijana wengine wanane wamekamatwa.

Gazeti la Punch la nchini humo, limeripoti kwamba mmiliki wa mahabusu hiyo na watu wengine wanane wamekamatwa.

Kamishna wa polisi wa jimbo hilo, Shina Olukolu, alinukuliwa akisema kwamba baadhi ya waathiriwa wa utekaji huo wamesema wamekuwa wakishikiliwa kwa miaka kadhaa.

"Hali katika msikiti huo ilikuwa ni mbaya kwa binadamu kuishi na baadhi ya vifo vya waathirika vilivyotokea ambavyo havikuripotiwa," alinukuliwa akisema.

Huu ni mojawapo ya uvamizi wa wa hivi karibuni wa vituo vinavyoitwa "'Vituo vya kurekebisha tabia" nchini Nigeria ambapo watu wanashikiliwa wakiwa katika hali mbaya ikiwemo kufungwa na minyororo.

Wengi husajiliwa kwenye taasisi hizo na ndugu zao ili kupata usaidizi wa kiroho na kurekebisha tabia kwa wanaotumia dawa za kulevya.

Mwezi uliopita polisi nchini Nigeria waligundua zaidi ya vijana 70 wakiwa wamefungwa katika shule binafsi ya kiislamu Kaskazini mwa Nigeria.

Mamia ya vijana wametoroka katika shule mbalimbali za dini ya kiislamu katika siku za hivi karibuni.

Shule za bweni za kiislamu zinazojulikana kama Almajiris ni maarufu sana kwa waislamu wengi Kaskazini mwa Nigeria. **BBC**



Wanawake walikuwa ni miongoni mwa watu waliookolewa mwezi Oktoba, mwaka huu kutoka kwenye kituo cha kurekebisha tabia cha kiislamu nchini Nigeria. **PICHA: REUTERS**

## Marekani kujiondoa makubaliano ya Paris

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imeanza rasmi mchakato wa kujitoa kutoka katika makubaliano ya Paris ya mazingira, kulingana na Waziri wa Mambo ya Kigeni, Mike Pompeo.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alikuwa mpinzani mkubwa wa makubaliano hayo wakati alipokuwa anawania kiti cha urais.

Utawala wake umekuwa ukifanya kila liwezekanalo kubadilisha sheria za mazingira, ukisema zinazuwia biashara na kutoa kwa nchi nyingine nguvu ya ushindani.

Waziri Pompeo wakati akitangaza Marekani kujitoa huko alielezea kuhusu kile alichokiita "Mzigo usio wa haki wa kiuchumi uliowekwa kwa wafanyakazi wa Marekani, biashara na walipa kodi, kwa ahadi za Marekani zilizotolewa chini ya makubaliano hayo. "Mfano bora na wenye uhalisia" utapendekezwa na Marekani kupinga makubaliano hayo ya dunia.

Makubaliano ya mwaka 2015 yalitiwa saini na karibu nchi zote na kuuweka utawala wa Trump karibu washirika wake wote pamoja na washindani wake wakuu kuhusiana na suala la mabadiliko ya tabia nchi.

Trump binafsi ni mtu mwenye shaka na mabadiliko ya tabia nchi.

Utawala wa Trump uliuarifu rasmi Umoja wa Mataifa hatua yake hiyo ya kujitoa siku ya Jumatatu, ukianza mchakato wa mwaka mmoja ambao utakamilika siku moja baada ya uchaguzi wa Rais huyo mwakani.

Msemaji wa Umoja wa Mataifa alilithibitishia Shirika la Habari la Ujerumani DPA kuwa taasisi hiyo ya dunia imepokea barua ya Marekani.

Katika mikutano yake ya kisiasa, Rais Trump kwa kawaida hutumia hotuba kuonyesha mapenzi yake kwa hewa safi na majisafi na salama.

"Tuna hewa safi kabisa katika dunia hapa Marekani," ni neno linalojirudia kila mara kutoka kwa Rais Trump.

Hata hivyo, uchunguzi umeonyesha kuwa tangu mwaka 2016 baadhi ya aina ya uchafuzi wa hewa unaongezeka.

Duniani, kwa ujumla wanasayansi wana wasiwasi kuwa ongezeko la joto unaosababishwa na utoaji wa gesi chafu wa binadamu utasababisha hali mbaya kwa maisha katika sayari hii.

Wakati huo huo, Ufaransa imelalamikia uamuzi huo wa Marekani kuarifu rasmi Umoja wa Mataifa kuwa inajitoa kutoka katika mkataba huo wa Paris. Wakati hatua hiyo ilikuwa ikitarajiwa, "Tunasikitika inaufanya ushirika wa Ufaransa na China kuhusu mazingira na bio anuai kuwa muhimu zaidi," Ofisi ya Rais wa Ufaransa imesema wakati Rais Emmanuel Macron akiwa katika ziara rasmi nchini China. **DW**

HABARI KITAIFA

# Kilio upinzani uchaguzi mitaa

INATOKA UK. 2

ombea wa vyama vya upinzani hawakujitokeza kuchukua fomu katika vijiji hivyo 12, hivyo wenyeviti wake wamepita bila kupingwa na Chama kilichochukua fomu ni CCM.

Kwa mujibu wa Masatu, katika vitongoji 294 vilivyoko katika Wilaya ya Hai, wenyeviti wake 110 ambao ni wa CCM, wamepita bila kupingwa kwa madai kuwa vyama vingine vya upinzani havikujitokeza kuchukua fomu.

Wakati hayo yakiendelea, Chama cha NCCR-Mageuzi Jimbo la Vunjo kimelalamika kuhusu kile kilichodai sarakasi za mwenendo wa uchaguzi huo, kikidai vituo vya uchaguzi katika jimbo hilo kufungwa kwa siku nne mfululizo.

Katibu wa Jimbo la Vunjo wa chama hicho, Mathew Temu, alisema jana kuwa kufungwa kwa ofisi hizo kumesababisha wagombea wao katika ngazi za vijiji, vitongoji na wajumbe wa halmashauri, kushindwa kuchukua na kurudisha fomu. Alibainisha kuwa, kati ya wagombea wao 1,968, waliofanikiwa kuchukua na kurudisha fomu ni 1,008, hivyo 960 walinyimwa fursa ya kuchukua na kurudisha fomu.

Temu alisema Chama cha NCCR Mageuzi kinatoa rai kwa wagombea wake wote katika jimbo hilo kuwa watulivu wakati suala hilo linafuatiliwa ili haki ipatikane.

### CUF KORTINI

Chama cha Wananchi (CUF) kimetangaza kumshitaki mahakamani Waziri Jafo na wasimamizi wa uchaguzi endapo hatasimamisha mchakato wa uchaguzi huo ili kufanyia kazi dosari zilizojitokeza.

Makamu Mwenyekiti wa CUF Tanzania Bara, Maftah Nachuma, aliyasema hayo jana wakati wabunge wa chama hicho walipozungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya hoja yao kuhusu uchaguzi huo kukataliwa kujadiliwa bungeni.

Alisema wamefikia hatua hiyo baada ya wagombea wao katika uchaguzi huo nchini kunyimwa fomu, wengine kuzuiwa kuzirudisha huku wengine wakienguliwa bila sababu za msingi.

Wakati wa mjadala bungeni, Maftah ambaye ni Mbunge wa Mtawara Mjini, aliomba mwongozo kwa Spika na kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili hoja ya uchaguzi huo kutawaliwa na rafu.Maftaha alidai asilimia 99 ya wagombea wa CUF katika baadhi ya maeneo kama vile Jimbo la Liwale, Kigoma, Kwimba na Ubungo wamenyimwa fomu au kuzuiwa kurudisha na wengine kuenguliwa bila sababu za msingi.

Spika Job Ndugai alikataa hoja hiyo, akitaka ushahidi kwanza wa kile kilichoelezwa na mbunge huyo.

### WANANE MBARONI

Jijini Mbeya, Jeshi la Polisi linawashikilia watu wanane, akiwamo Katibu wa Chadema, Kata ya Itawa, Mwawa Posta (40), kwa tuhuma za kuvunja Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji na kuiba nyaraka za serikali zikiwamo fomu za wagombea wa nafasi mbalimbali za serikali za mitaa.

Akizungumza na wandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kufanya tukio hilo Oktoba 31, mwaka huu saa 1:50 usiku.

Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Enock Mwasile (25), Alex Mwasile 21), Amon Mwasile (40), Aluwa Ngeleka (37), Bahati Yanjile (45) Mosca Mwasele (32) na Charles Mwasele (31) ambao wote ni wakazi wa Kijiji cha Pashungu.

### AGIZO LA JAFO

Akizungumzia kuhusu malalamiko hayo jana, Waziri Jafo alisema ameshatoa maelekezo kwa kamati za rufani kuhakikisha zinatenda haki kwa wale wote walioonekana kunyang'anywa haki zao.

"Nimeshatoa maelekezo kwa kamati za rufani ambazo zinaongozwa na makatibu tawala wa wilaya wahakikishe wanasimamia haki ya mtu yeyote, ikionekana haki yake ilitaka kunyang'anywa kwa makusudi, lazima irejeshwe," alisema.

Uchaguzi huo umepangwa kufanyika Novemba siku 18 zijazo, ukitarajiwa kuhusisha zaidi ya wapigakura milioni 19.

***Imeandikwa na Enock Charles (DAR), Gwamaka Alipipi (DODOMA), Nebart Msokwa (MBEYA) na Godfrey Mushi (KILIMANJARO).**

Distributed via ippmedia

# CAG Assad ampa angalizo mrithi wake

INAENDELEA UK.2

wetu, tukakutana TRA, siyo mtu mgeni kwangu, akihitaji kitu chochote kutoka kwangu kutokana na uzoefu wangu wa miaka mitano nitampatia, muda wowote atakapohitaji ushirikiano nipo tayari," alisema.

Prof. Assad aliulizwa na waandishi wa habari kuhusu vikwazo kwenye Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi aliyokuwa mkuu wake, akasema vipo vingi lakini hakuwa tayari kuvitaja kutokana na kile alichokisema kuwa ni kuepusha ukakasi.

"Changamoto (vikwazo) nilizopitia ni nyingi na mnazijua, mnachokitaka hapa mnataka niweke ukakasi, hakuna haja katika hilo," Prof. Assad alisisitiza.

Mtaalamu huyo wa uhasibu wa udhibiti wa fedha, alisema anapenda shughuli za kilimo na kwa kuwa sasa anaondoka katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, anakwenda kuwekeza nguvu nyingi shambani, lakini atakuwa anarejea mjini akihitajika.

"Kichwani kwangu napenda nipande bamia, niisimamie iote niivune, niingie jikoni nile.

Nimeingia katika ukulima miezi mitatu, nilikuwa naandaa mashamba, hivyo naenda kuishi shambani kwangu na kufanya shughuli za kilimo, watu wa mjini wakinihitaji nitakuja," alisema.

### KAULI YA KICHERE

Katika hafla hiyo, Kichere alimshukuru Prof. Assad kumkabidhi ofisi hiyo na kuahidi kushirikiana na timu aliyoikuta.

Alisema anajiunga na ofisi hiyo kufanya kazi ya wananchi kwa kuhakikisha mapato ya nchi yanatumika katika masuala ya maendeleo.

Kichere alisema kazi kubwa ya CAG ni kuhakikisha mapato ya nchi yanatumika kwa vizuri kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

"Niwaahidi kuwa nitaendelea kuifanya hii kazi ambayo imefanywa na Prof. Assad pamoja na timu yake, nitashirikiana na timu yake kufanya kazi hiyo kwa umahiri wa hali ya juu.

"Nitafanya kazi hii kwa kuzingatia weledi, uadilifu kama alivyosema Prof. Assad, CAG si anayefanya kazi, anachukua jukumu la kutia saini ripoti ambazo zinaanzia chini kwa wafanyakazi na kufikia uongozi wa juu," alisema.

Kichere alisema atajenga timu nzuri kwa kuhakikisha kuanzia ngazi ya chini kunakuwa timu yenye ushirikiano kwa anaamini huwezi kuwa na watu ambao wamesambaratika na ukawa na matarajio ya kuwa na kazi bora.

"Hautafurahi kuona mwanafunzi wako amesambaratisha taasisi ambayo umekuwa katika miaka mitano. Kama kutakuwa na mabadiliko, yatafanyika kwa umakini mkubwa bila kuathiri taasisi," alisema.

Alisema amefanya kazi katika Mamlaka ya Mapato (TRA) na anajua ugumu wa ukusanyaji wa mapato, hivyo atahakikisha anayalinda mapato na atawaumbua wale wanaotumia vibaya mapato hayo.

Kichere pia alisema atakwenda kuimarisha uhusiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Bunge ambao hivi karibuni uliingia dosari baada ya Bunge kutangaza kutofanya kazi na Prof. Assad.

"Nitaendeleza uhusiano mzuri, kama kulikuwa na kulegalega kwa uhusiano, ni lazima niuimarishe, huwezi kufanya kazi bila Bunge kwani Bunge limepewa kazi ya kuiangalia serikali," alisema.

# Mbowe akana kuwapo

INATOKA UK.2

Akwiline, aliyepigwa risasi katika maandamano hayo kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari na kwamba polisi inawashikilia askari kuhusu tukio hilo.

Alidai kuwa hajawahi kula njama na washtakiwa wenzake bali waliitwa kwa nyakati tofauti kwenda polisi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya.

Wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji jinai kati ya Februari Mosi na 16, 2018, Dar es Salaam.

# Deni la Taifa

INATOKA UK. 3

Taifa kutoka Sh. trilioni 33.105 mwaka 2019/20. Alisema matumizi ya kawaida pia yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.7 hadi Sh. trilioni 21.660, sawa na asilimia 13.7 ya Pato la Taifa na matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 12.699, sawa na asilimia nane ya Pato la Taifa.

Alisema mwaka 2020/21, mapato ya ndani (yakijumuisha mapato ya halmashauri) yanakadiriwa kuongezeka hadi Sh. trilioni 23.456 mwaka 2020/21 kutoka makadirio ya Sh. trilioni 23.045 mwaka 2019/20 na kukadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 8.8 katika muda wa kati.

"Uwiano wa mapato ya ndani kwa mapato yote unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 68.3 ya bajeti ya mwaka 2020/21 hadi asilimia 73.7 mwaka 2022/23.

Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.3 hadi Sh. trilioni 19.761 mwaka 2020/21 kutoka Sh. trilioni 18.955 mwaka 2019/20 na kukua kwa wastani wa asilimia 8.9 katika muda wa kati.

"Mapato yasiyo ya kodi (yakijumuisha mapato ya halmashauri) yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 3.601 mwaka 2020/21 na kuongezeka kufikia Sh. trilioni 4.34 mwaka 2022/23," Dk. Mpango alisema.

Mtaalamu huyo wa uchumi alisema mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mpango.

Naibu Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, David Silinde, akisoma maoni ya upinzani kuhusu mapendekezo ya mpango huo umefeli kwa kuwa unaingia sasa mwaka wa mwisho wa utekelezaji wake ilhali malengo yake makubwa hayajafikiwa hata robo.

Alisema lengo kuu la Mpango wa Pili lilikuwa kuhakikisha Tanzania inaingia katika uchumi wa kipato cha kati.

Silinde ambaye pia ni Mbunge wa Momba (Chadema), alisema serikali inapaswa kujipima kama imefikia lengo hilo.

# Mtendaji mbaroni tuhuma za rushwa

INATOKA UK.3

mtoa taarifa aliingia ofisini kwa mtuhumiwa lakini hakuandikiwa barua kwa kisingizio kwamba mihuri ilikuwa nyumbani.

"Baada ya harakati hizo, Takukuru ilimkamata na anatarajiwa kufikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka ya kushawishi na kupokea rushwa.

Katika hatua nyingine, Takukuru imemfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Kongwa, Mary Lema (34), mkazi wa Kibaigwa Kongwa, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Miembeni wilayani Kongwa kwa tuhuma za kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 6.959.

Taasisi hiyo inadai mwalimu huyo alijipatia fedha hizo zikiwa ni mishahara kuanzia Januari, 2014 hadi Februari, 2016 kinyume cha taratibu kwa kuwa uchunguzi umethibitisha kwamba katika kipindi tajwa, hakuwa kazini bila taarifa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

**2 ACRE YARD FOR RENT Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: gold@goldtz.net**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMANUEL WILBARD ASSEY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0920-0092** kilichotolewa na **PAKULA SEKONDRI** mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/256330/2019.**

115501502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;214/2019**

**Ombi la SAKINA KASSIM KULOLELA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAJI MOHAMED NGATUMBURA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/10/2019

11550202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MVOMERO ILIYOPO MVOMERO**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 8/2019**

**HUSSEIN R. KILALAMA (UNSOUND MIND).......... MDAI**
**KAIMU RAJABU (NEXT FRIEND)**

**DHIDI YA**
**MTIBWA SUGAR ESTATE CO.LTD.........1.MDAIWA**
**MASANJA KUTIKA.............2.MDAIWA**

**MTIBWA SUGAR ESTATE CO.LTD** na **MASANJA KUTIKA** mnaamriwa/inaamriwa/unaamriwa na **MAHAKAMA** hii kuhudhuria wewe/wao/nyiye wenyewe binafsi au wakili wako/wenu,mnamo tarehe 25/11/2019 kwenye shauri la madai namba 8/2019.Hivyo mnatakiwa kufika bila kukosa tarehe hiyo.Tambua kuwa kukosa kufika ktk shauri hilo,itapelekea shauri hilo kusikilizwa bila nyiye/weye/wao kuwepo.

Hati hii imetolewa leo tarehe 30/10/2019 mbele ya **MAHAKAMA ya wilaya MVOMERO.**

115501002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BAHATI LUCAS MASILA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 946 ALP TOYOTA COROLLA SALOON. Chassis namba EE1013121185.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/STA/RB/443566/2019.

115502401

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI


**IBRAHIM AMIN HERRY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili T 934 CAK HONDA. Chassis namba MD90E2413927. Engine namba MD902409827.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **TAN/RB/9088/2016.**

115502202

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**JOFREY JONAS DIANGE** anatangaza kupotea kwa result slip ya kidato cha sita yenye **index namba S0128/0542** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari Malangali. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi . Polisi Taarifa: **MOR/MVR/438476/2019**

115502602

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP




**DICKSON MILLE ABDUELY** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha sita yenye **index namba S0906/0534/2019** iliyotolewa na **VUDOI HIGH SCHOOL** mwaka 2019.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: UD/RB/2173/09.**

115500602

## KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA

Distributed via ippmedia



**Berno Kalunde Batinamani** anatangaza kupotea kwa Passport/ Hati ya kusafiria yenye namba AB170410 iliyotolewa mwaka 2006 na Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

*Polisi Taarifa: W/KN/09*

115501202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**YAH: KUOMBA URAIA**



**STEFANUS ERASMUS ALBERTUS VONSTADE**
Mwenye picha hapo juu, anaomba Uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni Afrika ya kusini. ***Nchi atokayo ni*** Afrika ya kusini. ***Anwani ya mwajiri wake S.L.P 60602*** DAR ES SALAAM.

Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwa nini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512,Dar es Salaam.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**As Logistics LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Aina ya trailer yenye namba za usajili **T 821 BLM. Chasis no. KW433917** rangi multicolore. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOD/TR/431722/2019.**

115502302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 18/04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI** tarehe 07/11/2019 kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KURASINI DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA**, gari hilo lenye namba za usajili: **T 950 CPR/ T 904 DDB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 21 |
| Upana | - mita | 3.3 |
| Kimo | - mita | 5.2 |

3. **Njia itakayotumika: KURASINI** hadi **TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA, MAKAMBAKO** Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni) Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215501102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo CHAMWINO MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;68/2019**

**Ombi la PETER RICHARD Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RICHARD MWANGUNULE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/11/2019**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ICARDI SASA ATAKA KUCHEZA NA CAVANI




**PARIS,** Ufaransa

MAURO Icardi anaamini atakuwa na upatina mzuri zaidi na Edinson Cavani katika klabu ya Paris Saint-Germain, na kwamba kocha Thomas Tuchel anatakiwa kuwatumia washambuliaji hao wawili kwenye kikosi cha kwanza kwa pamoja.

Akiwa amehamia hapo jijini Paris akitokea Inter Milan kwa mkopo wa muda mrefu, Icardi tayari amefunga mabao saba kwenye mashindano yote aliyoichezea PSG. Ujio wake ulikuwa muhimu hasa ikizingatiwa kwamba, Cavani ambaye ni mchezaji wa zamani wa Napoli aliumia na kulazimika kukaa nje kwa wiki sita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay ametokea benchi katika mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, ukiwamo ule wa Ijumaa ambapo PSG ilifungwa mabao 2-1 na Dijon, lakini kocha Tuchel bado hajawatumia Cavani na Icardi kwa pamoja.

Kwa mujibu wa Icardi, wawili hao wanajuana vizuri zaidi wakiwa wanacheza pamoja kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A na hivyo wakichezeshwa pamoja wanaweza kufanya vizuri zaidi.

"Nimemjua Edi kwa muda mrefu uliopita, tumekuwa pamoja nchini Italia kwa kipindi kirefu. Edi ni mchezaji wa aina yake ambae ameweka historia PSG, amefanya makubwa hapa," alisema Icardi akiiambia RMC.

"Nataka kutengeneza mchango wangu hapa, lakini ni kocha ambaye ataamua nani wa kucheza."Wote tunaweza kucheza pamoja na kuifanya timu kuwa vizuri, na hicho ndicho tunachozungumza wenyewe tukiwa ndani ya dimba au nje.

"Edi na mimi ni washambuliaji wawili ambao tunapenda kufunga mabao, tunaweza kucheza pamoja, lakini maamuzi hayapo juu yetu. Mwisho wa siku kocha ndiye mwenye maamuzi."

Distributed via ippmedia

# Mrithi wa Kovac Bayern ndani ya wiki tatu

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa Klabu ya Bayern Munich, Uli Hoeness amesema mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, watajua zaidi kuhusu nani wa kuchukua mikoba ya kocha Niko Kovac ndani ya wiki tatu.

Kocha Kovac alifukuzwa juzi baada ya Bayern kufungwa mabao 5-1 na Eintracht Frankfurt, na kuiacha timu hiyo kuwa nafasi ya nne kwenye msimamo na ikipitwa pointi nne na vinara wa ligi hiyo.

Hans Flick amepewa nafasi ya kuiongoza timu hiyo kwa muda kuelekea mchezo wa leo Jumatano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Olympiacos na ule wa Ligi Kuu wa Jumamosi dhidi ya Borussia Dortmund.

Alipoulizwa kuhusu kocha mpya wa kuchukua nafasi ya Kovac na huku kukiwa na uvumi wa kuhusishwa na makocha kama Ralf Rangnick, Erik ten Hag wa Ajax, Arsene Wenger, Massimiliano Allegri na Jose Mourinho, Hoeness aliwaambia waandishi wa habari: "Kila kitu kimeshasemwa tayari kuhusu hili.

"Nafikiri taarifa yetu ya Jumapili jioni ilikuwa na maelezo ya kutosha.

"Siwezi kusema nini kitakachotokea ndani ya wiki tatu zijazo. Si muhimu kwa sasa, tuna wiki tatu zijazo kuangalia nani atachukua mikoba. Nafikiri tulifanya vizuri.

"Tulikuwa na uhusiano mzuri na Niko Kovac. Tulikuwa na makubaliano mazuri. Hakuna chochote kibaya. Nilimpigia simu na kila kitu kipo sawa. Kwa sasa hana tena presha, yupo huru."





# Alisson akerwa mabao wanayofungwa Liver

**LIVERPOOL,** England

GOLIKIPA wa Liverpool, Alisson Becker amesema anakasirishwa na idadi ya mabao ya "kipuuzi" waliyofungwa Liverpool msimu huu.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kimecheza mechi tatu tu kati ya 18 bila kuruhusu bao.

Mabingwa hao wa Ulaya walipata ushindi wa 2-1 pale kwenye dimba la Villa Park, lakini Alisson amechukizwa na jinsi mambo yanavyokuwa magumu.

"Inanifanya niwe na hasira kwa jinsi tunavyofungwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari." Mabao ya kipuuzi! Wakati tukifungwa inanifanya nikasirike.

"Mara zote tumekuwa na mabao yanayofanana tukiwa tunapata ushindi. Unakaribia kushinda bila kuruhusu bao na mara zote unatoka sare.

"Unaporuhusu kufungwa, mchezo unakuwa mgumu zaidi. Tunahitaji kufanya kazi vizuri kama tunataka mambo yaende vizuri."

# Lampard: Sijaathirika Chelsea kuzuiwa kusajili

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza "ana furaha sana" na wachezaji wake hasa wakati huu ambapo Chelsea imefungiwa kufanya usajili na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.

Timu hiyo ya Ligi Kuu ya England ilifungiwa kufanya usajili wa wachezaji wapya kwa madirisha mawili Februari baada ya kuvunja kanuni.

Chelsea waliruhisiwa kuwaandikisha wachezaji chini ya umri wa miaka 16, lakini klabu hiyo ilitangaza kukata rufani kwenye Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS) na tarehe ya kusikilizwa kwake imepangwa kuwa Novemba 20, mwaka huu.

Lampard amesema hana tatizo na hali ya kufungiwa kufanya usajili kwa klabu hiyo, hasa ikizingatiwa kwamba wachezaji vijana kutoka kwenye akademi yao, Tammy Abraham, Mason Mount na Fikayo Tomori wakiwa wanafanya vizuri kwenye kikosi cha kwanza msimu huu.

Alipoulizwa kuhusu maoni yake na waandishi wa habari kuelekea mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax uliopigwa jana Jumanne, Lampard alisema: "Sina tatizo, lakini sijui sana kuhusu hiyo kesi.

"Inaweza kutuathiri kwa kile tunachoweza kufanya, lakini kwa kiasi kidogo tu. Kwa sasa nafikiri zaidi mchezo wangu dhidi ya Ajax na baadaye Crystal Palace.

"Tupo kwenye hali nzuri. Mara zote tutaangalia jinsi ya kujiimarisha, lakini nina furaha na kile tulichonacho."

Baada ya kufungwa na Valencia kwenye mchezo wao wa kwanza wa Kundi H, Chelsea imeshinda mechi mfululizo dhidi ya Lille na Ajax.





Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano ya Gofu ya Hisani yaliyoandaliwa na Klabu ya Rotari ya Bahari, Hemaly Jethwa (kulia), akikabidhi cheti kwa Mkuu wa Kitengo cha Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati wa Benki ya NBC, Evance Luhimbo (katikati) kwa kutambua udhamini wa benki hiyo katika mashindani hayo yaliyofanyika katika viwanja cha Gofu vya Gymkhana jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Mashindano hayo yaliyowashirikisha wacheza gofu 104, yalikuwa na lengo la kukusanya fedha kusaidia watu wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na mradi wa kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama, vyoo na kituo cha mafunzo kwa njia ya mtandao katika Shule ya Sekondari Mtakuja iliyopo Kunduchi jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Meneja Uhusiano wa NBC, Joseph Lema. **NA MPIGAPICHA WETU**




# GUARDIOLA: LIVERPOOL HAINIUMIZI KICHWA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesisitiza safari ya Manchester City kwenda kucheza na Liverpool wikendi ijayo haijakifanya kikosi chake kupoteza matumaini ya kutwaa taji la Ligi Kuu.

Mabingwa hao watetezi watakwenda kucheza pale Anfield wakiwa wamepitwa pointi sita na Liverpool waliopo kileleni baada ya timu zote hizo kushinda mechi zao za wikendi iliyopita.

City walipata ushindi wa 2-1 nyumbani dhidi ya Southampton shukrani kwa bao la dakika za majeruhi la Kyle Walker, huku Liverpool wao wakishinda dhidi ya Aston Villa.

Hata hivyo, Guardiola hatapaniki kama wakishindwa kupunguza pengo kwenye mchezo huo wa Jumapili, ambapo walipitwa pointi saba msimu wa 2018-19 na wakaweza kuwapiku Liverpool na kutwaa ubingwa.

Alipoulizwa kama atamaliza kipindi cha miaka 15 cha kusubiri ushindi kwenye Uwanja wa Anfield ili kuwa na matumaini ya ubingwa, Guardiola alisema: "Tunakwenda kujaribu, lakini sidhani. Ni karne ngani hawajapoteza kwenye uwanja wa Anfield?

"Tunajua nini kilichotokea Jumamosi - waliwavunja Aston Villa dakika za mwisho. Kuna mechi nyingi za kucheza.

"Mambo mengi yanakwenda kutokea na kuna mechi nyingi za kucheza."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID KUMTOA BALE, BIL. 207/- KWA STERLING

●●● Hajafanya siri yoyote kuhusu matamanio yake ya kucheza La Liga, lakini...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inajiandaa kutesti 'zari' la kumsajili winga wa Manchester City, Raheem Sterling kwa kuipa kiungo mshambuliaji Gareth Bale pamoja na ofa ya pauni milioni 70 sawa na Sh. bilioni 207.6 za Tanzania ili kupata huduma ya Muingereza huyo.

**Sky Sports News inatambua wawakilishi wa Real watasafiri kwenda kutazama kiwango cha Sterling baadaye mwezi huu wakati England ikiwa nyumbani dhidi ya Montenegro na baadaye ugenini dhidi ya Kosovo, kabla ya kutoa uamuzi wa mwisho wa kina wa mapendekezo ya ofa kwa City.**

Wawakilishi wa Sterling, walikutana na Mkurugenzi Mkuu wa Real, Jose Angel Sanchez majira ya joto waliposhindwa kutoa ofa ya kujaribu kumhamishia mshambuliaji huyo wa City katika dimba la Bernabeu.

Hata hivyo, Rais wa Real, Florentino Perez anajua miezi mingine 12 bila kuwapo na dili kutashuhudiwa thamani ya pauni milioni 150 kwa Sterling kwa sasa ikiongezeka zaidi.

Binafsi City na hasa Pep Guardiola, wanaeleweka kwa kutovutiwa kumsajili mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Wales mwenye umri wa miaka 30, Bale.

Kwa usawa, kama Bale atachagua kuondoka, kubaki na Real, kisha Perez atapaswa kuachana na kiasi kinachokaribia rekodi ya dunia ya pauni milioni 200 zilizolipwa kwa Barcelona na Paris Saint-Germain ilipomsajili Neymar.

Sterling hajafanya siri yoyote kuhusu matamanio yake ya kucheza La Liga, lakini kuwapo kwa taarifa nyingi Jumatatu nchini Hispania kwamba Bale anataka kumalizia soka lake La Liga, Perez anaamini dili linalohusisha majina makubwa mawili katika ulimwengu wa soka, linaweza kukubaliwa na City.

Real kuvutiwa na Sterling kunajulikana vizuri nyuma ya pazia hapo Etihad. Kwa upande wao City wanatamani kuendelea kumbakisha mchezaji waliyemnunua kutoka Liverpool mwaka 2015 kwa pauni milioni 49 - ambayo iliweka rekodi kwa mchezaji wa Kiingereza.

Wakati huo huo, Leroy Sane alishindwa kukubaliana dili na City na Rais wa Bayern, Uli Hoeness ameongeza kujiamini kuhusu kuinasa saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani, jambo ambalo litashuhudiwa mawinga wanne wakipungua na kuwa wawili ifikapo mwishoni mwa msimu.

Kwa Perez, presha imeongezeka ikiwa ni kutokana na kuondoka kwa Cristiano Ronaldo na kujiunga na Juventus Julai 2018.

## ZISIKUPITE

### ZAHA, WERNER RADA CHELSEA

CHELSEA imewaweka mshambuliaji wa Crystal Palace, Muivory Coast Wilfried Zaha, 26, na straika wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, 23, katika orodha ya wachezaji inaotaka kuwasajili dirisha la Januari kama wataondolewa kifungo cha usajili. ***(Express)***

### WENGER ATAJWA BAYERN

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger ni miongoni mwa waliopo katika orodha ya kuinoa Bayern, wakati huu ikitafuta mrithi wa Niko Kovac, ambaye ameondoka kwa mabingwa hao mwishoni mwa wiki. ***(Guardian)***

### POGBA WIKI NNE ZAIDI NJE

MANCHESTER United itaendelea kumkosa kiungo wa kimataifa wa Ufaransa Paul Pogba, 26, kwa angalau wiki nne kwa sababu ya majeraha ya kifundo cha mguu. ***(ESPN)***

### LAMPARD KUJAZWA NOTI

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, atapewa hadi pauni milioni 150 za kutumia kununua wachezaji katika dirisha la Januari kama klabu hiyo itaruhusiwa tena kusajili. ***(Telegraph)***

### LIVERPOOL, UNITED ZAONYWA

MANCHESTER United na Liverpool pia zimekuwa zikihusishwa na Timo Werner, 23, lakini klabu hizo za England zimeonywa na RB Leipzig kwamba hatakuwa tayari kumwacha straika huyo aondoke. ***(Mirror)***

### AMTAKA MOURINHO

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho anaweza kuvutiwa kuinoa Bayern, kwa mujibu wa kiungo Mjerumani Bastian Schweinsteiger, ambaye alicheza chini ya Mreno huyo wakati akiwa Old Trafford. ***(Evening Standard)***

### RICE ANUKIA JANUARI UTD

MANCHESTER United imepania kumsajili kiungo wa West Ham na England, Declan Rice, 20, majira yajayo ya joto, lakini anaweza akanunuliwa klabuni hapo mapema Januari. ***(Goal)***

### CHELSEA NAYO KWA DEMBELE

CHELSEA imeingia katika mbio za kuiwania saini ya mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 23, na nyota huyo wa zamani wa Celtic pia anatakiwa na Manchester United. ***(Mail)***

### YAZIFUATA CITY, ARSENAL

WOLVES inaandaa ofa ya pauni milioni 13 kwa kiungo wa Atalanta, Msweden Dejan Kulusevski, 23, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester City na Arsenal. ***(Sport Witness)***

### ROMA YAGOMEWA SMALLING

MANCHESTER United imekataa ofa ya pauni milioni 13 kutoka Roma ambayo inataka kumsajili beki Chris Smalling, 29, anayeichezea kwa mkopo kwa sasa. ***(Star)***

### DWIGHT AGOMBEWA TIMU EPL

LEICESTER, Wolves na Everton zote zinamfukuzia winga wa Burnley, Muingereza Dwight McNeil, 19. ***(Teamtalk)***

HABARI MICHEZO

# DStv yaja na Shangwe za Sikukuu

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania imetangaza kuzindua rasmi kampeni yake ya msimu wa sikukuu ijulikanayo kama 'Shangwe za Sikukuu na DStv' huku ikitangaza ofa kabambe kwa wateja wake wapya wanaojiunga na DStv katika msimu huu.

Mkuu wa Mauzo wa MultiChoice Tanzania, Salum Salum amesema ofa hiyo kabambe na ambayo ilikuwa ikisubiriwa kwa hamu na Watanzania wengi, imeanza rasmi tangu Novemba Mosi na itadumu hadi Desemba 31, mwaka huu, ambapo wateja wote wapya wa DStv wataunganishwa kwa Sh. 99,000/- huku wakipatiwa ufundi pamoja na kifurushi cha DStv Compact cha mwezi mmoja bila malipo ya ziada.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Masoko, Baraka Shelukindo alisema kampuni ya MultiChoice imekuwa na utamaduni wa kushiriki na wananchi katika kunogesha msimu wa sikukuu na kwa mwaka huu wamekuja na kampeni ijulikanayo kama 'Shangwe za Sikukuu na DStv' ambapo ofa ya mwaka huu inahusisha kifurushi cha Compact cha mwezi mmoja pamoja na kufungiwa bila gharama yoyote ya ziada.

"Kila mwisho wa mwaka tunahakikisha tunakuja na kitu kipya ili kuwahakikishia Watanzania sikukuu yenye furaha zaidi. Sote tunafahamu wakati huu wa msimu wa sikukuu familia nyingi hujumuika pamoja ambapo shule huwa zimefungwa na watu wengi wakiwa katika mapumziko, huu ndio wakati muafaka wa kuwa na DStv nyumbani ambapo kuna burudani kwa kila mtu," alisema Shelukindo.

Kwa ofa hiyo mteja ana uhakika wa kifurushi cha Compact cha mwezi mzima bila malipo hivyo kuweza kushuhudia burudani kabambe zikiwamo ligi kubwa ulimwenguni, katuni motomoto kwa watoto, tamthiliya kabambe kama Huba, Kapuni na vipindi vingine mbalimbali bila kusahau chaneli za ndani kama vile TVE, Clouds Plus, Wasafi TV na nyinginezo.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 8 | 7 | 0 | 1 | 16 | 3 | 21 |
| 2. Tanzania Prisons | 10 | 4 | 6 | 0 | 13 | 8 | 18 |
| 3. Kagera Sugar | 9 | 5 | 2 | 2 | 12 | 7 | 17 |
| 4. Lipuli | 9 | 4 | 3 | 2 | 13 | 9 | 15 |
| 5. Ruvu Shooting | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 6. Polisi Tanzania | 8 | 4 | 1 | 3 | 9 | 9 | 13 |
| 7. Namungo | 9 | 4 | 1 | 4 | 7 | 7 | 13 |
| 8. Mtibwa Sugar | 10 | 3 | 3 | 4 | 9 | 11 | 12 |
| 9. Coastal Union | 9 | 3 | 2 | 4 | 8 | 8 | 11 |
| 10. Alliance | 9 | 2 | 5 | 2 | 7 | 7 | 11 |
| 11. Mbao | 10 | 2 | 5 | 3 | 8 | 9 | 11 |
| 12. Mwadui | 10 | 2 | 5 | 3 | 7 | 9 | 11 |
| 13. Azam | 6 | 3 | 1 | 2 | 5 | 3 | 10 |
| 14. JKT Tanzania | 8 | 2 | 3 | 3 | 5 | 7 | 9 |
| 15. Kinondoni MC | 7 | 2 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 |
| 16. Biashara United | 9 | 2 | 2 | 5 | 5 | 9 | 8 |
| 17. Mbeya City | 9 | 1 | 5 | 3 | 7 | 15 | 8 |
| 18. Young Africans | 4 | 2 | 1 | 1 | 5 | 4 | 7 |
| 19. Ndanda | 8 | 1 | 4 | 3 | 6 | 8 | 7 |
| 20. Singida United | 10 | 0 | 4 | 6 | 3 | 10 | 4 |

# MAYANJA AKALIA KUTI KAVU KMC

**Na Focus Nicus**

HUKU juzi kikao maalum kikiketi kujadili mwenendo wa kujisuasua pamoja na benchi la ufundi, kabla ya KMC FC kushuka dimbani siku hiyo na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Biashara United, ni dhahiri sasa Kocha Mkuu wa timu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni, Mganda Jackson Mayanja, amekalia kuti kavu.

Kwa matokeo ya mechi hiyo ya juzi iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, KMC sasa imefikisha pointi nane baada ya kushuka dimbani mara saba na kushinda michezo miwili, sare mbili na kupoteza tatu huku ikiwa katika nafasi ya 15 kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

**Kabla ya mechi hiyo, uongozi wa KMC ulifanya kikao, na kuonyesha kwamba kuna hatua imechukuliwa, Mayanja hakuiongoza timu hiyo dhidi ya Biashara United wakati ikipata ushindi wake wa pili msimu huu.**

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bodi ya KMC FC, Mstahiki Meya Benjamin Sitta, akizungumzia kuhusu kikao hicho na hatima ya Mayanja aliyerithi mikoba hiyo kutoka kwa Etienne Ndayiragije anayeinoa Taifa Stars kwa sasa akitokea Azam FC, alisema kilikuwa cha kawaida huku akifafanua kwamba kocha bado yupo.

"Kikao kilikuwa cha kawaida tu, suala la kocha kutokuwapo katika benchi ni "coincidence" ( bila kutarajiwa), lakini kocha bado yupo," alisema.

Alipoulizwa endapo kutokuwapo kwa kocha huyo kumechangia kupatikana kwa matokeo katika mechi hiyo, Sitta hakutaka kuwa muwazi katika hilo zaidi ya kusema huenda limechangia.

Katika mechi hiyo, mabao ya KMC ambayo msimu uliopita ilimaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, yalifungwa na Serge Tape dakika ya 30 na Kenny Ally dakika ya 58, wakati la kufutia machozi kwa Biashara United likifungwa na Ramadhan Chombo 'Redondo' dakika ya 65.




Kulia ni mshindi wa gari wa Promosheni ya Faidika na Jero, Yusuph Jackson, baada ya kukabidhiwa gari aina ya Renault Kwid, akifuatiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, Mtaalamu wa Huduma za Kidigitali kutoka Tigo, Ikunda Ngowi na mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubashiri Tanzania, Abdalla Ahmed. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mshindi gari Sportpesa na tiGO akabidhiwa*

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE mkazi wa Mugumu, Serengeti mkoani Mara, Yusuph Jackson, amekabidhiwa rasmi gari yake aina ya Renault Kwid baada ya kuibuka mshindi kwenye Promosheni ya Faidika na Jero iliyokuwa ikiendeshwa na Kampuni ya SportPesa kwa kushirikiana na Tigo.

Katika promosheni hiyo iliyodumu kwa siku 40, watumiaji wa mtandao wa Tigo kupitia huduma ya TigoPesa walipata nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo smartphone kila siku na siku ya mwisho zawadi ya gari ikatolewa ambalo liliangukia kwa Jackson.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Jackson alisema: "Ukirudia mazungumzo yangu siku ya kwanza wakati napigiwa simu, utagundua kwamba nilikuwa siwaamini walionipigia kama ni kweli ni SportPesa maana siku hizi mjini watu hawatabiriki. Nilikuwa nacheza tu, lakini sikutarajia bahati hii ya ushindi wa gari itanidondokea mimi.

"SportPesa wamenipa mapokezi mazuri ikiwamo kusimamia gharama zote kuanzia usafiri wa ndege, malazi pamoja na matumizi ya siku nzima na kuhakikisha gari langu linapata usajili kupitia jina langu na kukabidhiwa.

"Sijui nisemeje, lakini nawashukuru sana SportPesa, mimi ni mwajiriwa kwenye kampuni kama fundi welder (wakuchomea) na sikutarajia kama siku ningeweza kushinda zawadi ya gari," alisema na kuongeza.

"Nawasihi vijana wenzangu wacheze na SportPesa maana kwa sasa nawaona hawana mpinzani, na si kama unapoteza pesa. Mimi nilikuwa nacheza na kushinda kwa kubashiri mechi kama sehemu ya burudani, lakini leo nimejionea dhahiri kuwa kuna zaidi ya ushindi."

Kwa upande wa SportPesa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema: "SportPesa inazidi kuwafungulia dunia wateja wake hasa kwa kupitia promosheni mbalimbali, kupitia simu ya mkononi unaweza kufanya maajabu yanayoweza kubadili maisha yako.

"Napenda kumpongeza sana sana Yusuph kwa ushindi wake na kujinyakulia gari mpya aina ya Renault Kwid na kuweza kuitumia kujiingizia kipato na shughuli nyingine za kujenga taifa."

Mwakilishi kutoka Tigo, Ikunda Ngowi naye alisema "Kwa mara nyingine tena ningependa kumpongeza mshindi wetu na kuwahasa Watanzania waendelee kucheza na SportPesa kupitia mtandao wa Tigo maana mambo mazuri ni mengi."

# Michezo

Jumatano Novemba 6, 2019

Nipashe



Madrid kumtoa Bale, bil. 207/- kwa Sterling UKURASA 30

**WALETENI HAO...**



Distributed via ippmedia

Baadhi ya wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana asubuhi, kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons itakayopigwa Uwanja wa Uhuru kesho. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba, Prisons vita vya rekodi

**Na Focus Nicus**

WAKATI Simba ikiwakaribisha 'Wajelajela' wa Tanzania Prisons katika Uwanja wa Uhuru kesho, vita kubwa inaonekana itakuwa ni kutaka kuvunja na kulinda rekodi kwenye mchezo huo unaotarajiwa kuwa mkali na wakuvutia.

Kwanza Tanzania Prisons ambayo itakuwa ikishuka dimbani mara ya 11, itawania kulinda rekodi yake ya kutopoteza mechi msimu huu huku Simba ikitaka kuwa klabu ya kwanza kuivunja kwa kuwatembezea kichapo Wajelajela hao.

Lakini, Simba iliyopo kileleni mwa ligi hiyo, kama itatoka sare Prisons itakuwa timu ya kwanza kupata matokeo kama hayo kufuatia kikosi hicho cha Mbelgiji Patrick Aussems kushinda michezo saba kati ya nane iliyocheza huku ikipoteza mmoja tu wakati huu kikiwa na alama 21 kileleni.

Prisons iliyopo nafasi ya pili ikiwa na pointi 18 baada ya kushuka dimbani mara 10, huku ikishinda mechi nne na sare sita, imekuwa katika kiwango kizuri msimu huu na tayari kiungo wa timu hiyo, Cleoface Mkandala amesema wanataka kuweka rekodi kwa kuifunga Simba nyumbani.

"Kweli tunaiheshimu Simba, lakini hatuiogopi na kuifunga kwao ni kitu kinachowezekana," alisema.

Lakini Aussems aliliambia gazeti hili kuwa wanataka kuendeleza ushindi na anatambua mchezo huo utakuwa mgumu kwa kila upande hasa kutokana na ubora walionao wapinzani wao.

# *Zahera amwaga upupu akitimuliwa*

**Shufaa Lyimo na Jumanne Juma**

●●● Asema anaidai Yanga mamilioni na hakuwahi kupewa malengo katika klabu hiyo, Mkwasa apewa timu huku...

BAADA ya uongozi wa Yanga kutangaza kuachana na Kocha wao Mkuu, Mwinyi Zahera, Mkongomani huyo amemwaga 'upupu' akieleza hafahamu chochote kuhusu kutimuliwa kwake na kwamba kwanza klabu hiyo ilipaswa kwanza kumlipa mamilioni yake anayoidai na kufuata utaratibu uliopo katika mkataba wake vinginevyo atawashtaki.

**Uongozi wa Klabu ya Yanga kupitia kwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla akiambatana na Makamu Mwenyekiti wake, Fredrick Mwakalebela, jana ulitangaza kuachana rasmi na Zahera pamoja na kuvunja benchi zima la ufundi na nafasi ya kocha huyo mkuu sasa itachukuliwa kwa muda na Boniface Mkwasa.**

Lakini Nipashe lilipomtafuta Zahera, baada ya Yanga kutoa taarifa hiyo, alisema kama angekuwa ana taarifa ya kuvunjiwa mkataba wake asingefanya mazoezi ya asubuhi na timu hiyo aliyokuwa akiiandaa kuelekea mechi yao dhidi ya Ndanda FC.

"Mimi sijapata barua yoyote kutoka Yanga kuwa wameachana na mimi kwa sababu nilikuwa kwenye mazoezi ya asubuhi na wachezaji wangu nikijiandaa na mchezo wetu wa Ligi Kuu dhidi ya Ndanda FC ambao tulikuwa tucheze Novemba 8, mwaka huu," Zahera alisema.

"Binafsi sijaona sababu ya Yanga kunivunjia mkataba wangu kwani hawajakaa na kuzungumza na mimi chochote wakati bado nina madeni yangu mengi ambayo hawajanilipa na niliyowalipia wachezaji, iweje watangaze kuvunja mkataba bila kufuata taratibu mtu akikuvunjia mkataba lazima utaratibu wa mkataba ufuatwe.

"Ninataka nipewe barua iliyoambatanishwa na sababu zilizowafanya wao kwa nini waamue kuvunja mkataba na baada ya hapo nitazungumza kwa kina na vyombo vya habari, ili wadau na mashabiki wa timu hii wajue kile kilichokuwa kinaendelea baina yetu na uongozi."

Alisema hata walipokuwa kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika nchini Misri, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Dk. Msolla alimwahidi kutokumfukuza hata kama wakitolewa kwenye michuano hiyo.

Zahera alisema wakati anasaini mkataba wa kuitumikia klabu hiyo hajapewa malengo yoyote ya kuhakikisha timu hiyo inapata ubingwa kwenye mashindano ya kimataifa na kudai siku zote alizokaa na klabuni hapo hajaona dalili kama angekuja kufanyiwa hivyo.

"Tangu nirudi au leo asubuhi sijaona wala kusikia fununu yoyote ile kuwa ninafukuzwa ndani ya Yanga ndio maana naomba mvute subira mpaka nitakapopata barua nitasema yote kwa sababu nikisema mengi sasa hivi watanigeuzia maneno," alisema.

Awali akitangaza uamuzi wa kuachana na Zahera na kuvunja benchi zima la ufundi, Dk. Msolla alisema wameamua kuachana na Zahera baada ya kuona timu inakwenda vibaya.

"Tumeamua kuachana na Zahera baada ya Kamati yetu ya Utendaji kukutana kwa pamoja na kukubaliana na maamuzi hayo," alisema Msolla na kufafanua. "Tumeachana na Zahera kwa amani kabisa hila chuki yoyote lengo ni kupata kocha mzuri mwenye vigezo."

Aliongeza kuwa mkataba wa Zahera ulikuwa umalizike Septemba mwakani na wa Kocha Msaidizi, Noel Mwandila unatarajiwa kumalizika Desemba 3, mwaka huu.

Yanga ambayo imetolewa na Pyramids ya Misri kwa jumla ya mabao 5-1 kwenye mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, inashika nafasi ya 17 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi saba baada ya kushuka dimbani mara nne ikishinda michezo miwili, sare moja na kupoteza mmoja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >